# UHAKIKI WA MAKOSA KATIKA MAANDISHI YA WANAFUNZI WA SHULE ZA UPILI NA BAADHI YA VITABU VYA KIADA WANAVYOTUMIA SHULENI

**NA**

**WAFULA, ENOS BARASA**

TASNIFU HII IMEWASILISHWA KATIKA KITIVO CHA SANAA NA SAYANSI, IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA NYINGINE ZA KIAFRIKA KWA MINAJILI YA KUTIMIZA BAADHI YA MAHITAJI YA UZAMILI KATIKA KISWAHILI

CHUO KIKUU CHA MOI

**2021**

# UNGAMO

**Ungamo la Mtahiniwa**

Tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na haijawahi kuwasilishwa na/au kutahiniwa katika Chuo Kikuu chochote kwa minajili ya kutimiza mahitaji ya Shahada ya Uzamili au Shahada nyingine yoyote.

Sahihi:____________________ Tarehe:____________________

**Wafula, Enos Barasa**
**SASS/PGK/08/09**

**Ungamo la Wasimamizi**

Tasnifu hii imetolewa kwa ajili ya kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa Chuo Kikuu cha Moi.

Sahihi:____________________ Tarehe:____________________

**Dkt. Samuel M. Obuchi**

Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika,

Chuo Kikuu cha Moi, Eldoret, Kenya.

Sahihi:____________________ Tarehe:____________________

**Dkt. Mosol Kandagor**

Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika,

Chuo Kikuu cha Moi, Eldoret, Kenya.

# TABARUKU

Tasnifu hii imetolewa kwa hadhi ya wazazi wangu Julius Lukuto Katienyi (Omukibeti) na Teresia Nafula Nalianya (Omuyumbu), mke wangu mpendwa, raufu na mtulivu, Ruth Muyoka Makokha (Omuchekeleyi), na watoto wangu Simeon Mvuli, Patience Nafula, Peace Lukuto, Sunday Barasa Nandasaba, Pater Gift Mutoro Barasa na Damaris N. Pendo Barasa (Bakibeti). Hawa wote ni watu wazuri sana kwangu - kwa maneno ya Paroko wetu, Padri Peter Nyaki.

## SHUKRANI

Namshukuru Maulana kwa kunijalia nguvu, akili, muda na hekima ambavyo viliniongoza muda wote katika harakati za kuandaa tasnifu hii. Hakika uwezo ni wa Mungu pekee; sisi ni manokoa.

Likikwama matopeni huhitaji roho ya wenye mapenzi, imani na uvumilivu uliokithiri mipaka ya mazoea ili kujitolea sabili kulikwamua bila hofu ya kurukiwa na maji na matope machafu ajabu. Wasimamizi wangu, Dkt Samuel Obuchi na Dkt Mark Kandagor, wanastahiki shukrani zisizomithilishwa kwa kujitolea kwa dhati kunielekeza na kunihimiza pale nilipolegea hata nikakamilisha tasnifu hii. Hakuna kizingiti kilichowashinda. Familia yangu ikiongozwa na mke wangu Ruth na watoto wetu wote waliozoea kunikejeli wakisema 'rudi shuleni umalize masomo' inastahiki shukrani tele. Walinivumilia niliposhinda nikisoma hadi usiku wa manane na kurauka alfajiri mbichi kuendelea kuandika. Walinitengea kiti walichokiita 'kiti cha mzamili' na baadaye kunihamishia kwenye nyumba maalum ili kupunguza bughudha za runinga na kuibandika jina la 'ofisi'. Nawashukuru pia wahadhiri wangu katika kiwango cha uzamili Prof. Ogechi, Prof. Mwamzandi, Dkt. Opijah, Dkt. Oduori, Mwl. Munyua, Dkt. Mwanakombo na Mwl. Mumbo. Hawa walinifumbua macho na matongo yalipobanduka nikaona umuhimu wa kutafiti kwa kusoma kwa kina na mapana. Walinisaidia kuwa mtafiti badala ya kuwa mwanaharakati. Natoa shukrani za dhati kwa wazamili wenzangu: Dkt Mahero Toboso, Bi. Lilian Momanyi, Bw. Makori na Bw. Zachariah Kasavuli. Hawa tulipambana nao hasa hali ilipokuwa nzito tukitiana joto kama vifaranga wa mamakuku aliyenyakuliwa na mbweha.

Hali kadhalika, ningependa kuwashukuru wahadhiri wangu wakati wa shahada ya kwanza katika Chuo Kikuu cha Egerton kama vile Prof. James Onyangoh Ogollah

aliyezoea kutwambia kwamba kila mara ni lazima kuuliza kwa nini na kwa sababu gani?, Mwl Augustine Muindi, Mwl Siteti wa Ngero, Dkt Njoroge Kimani, Mwl Henry Wanjala na wengineo. Hawa walinyunyizia maji mche wa Kiswahili uliooteshwa ndani yangu katika shule ya upili na kuhakikisha kwamba haunyauki. Nawashukuru pia walimu wangu wa Kiswahili nilipokuwa kwenye Shule ya Upili ya St. Peter’s Mumias, Bi. Grace Kio Malombo Mwawasi na Mwl Jacob Akhonya kwa kunihimiza niendelee kusoma Kiswahili baada ya kupokezwa kijiti na Mwl Makokha Odongo wa Shule ya Upili ya Emusire. Ari yangu ya kupenda kusoma iliasisiwa na Mwl David Ssula aliyenichagua kuwa mkutubi nilipokuwa katika kidato cha kwanza huko Emusire. Nampa shehena ya shukrani. Nampongeza mpwa wangu, Benedette, ‘Benee’ kwa kupasa moto ile ‘afisi’ yangu ili kukabiliana na baridi kali iliyotaka kunihujumu, bila kujua ni nini kilichonishughulisha humo mchana na usiku katika siku hizo zote.

Hatimaye, ninatoa shukrani kwa watu wengine wenye nia safi waliojitolea kuniauni katika mchakato mzima wa kupata mali ghafi ya kuandikia tasnifu hii. Ninawaombea heri maishani ili waendelee kuwafaa watafiti wengine.

## IKISIRI

Ukiukaji wa kanuni za kitahajia na kisarufi katika lugha husababisha makosa. Makosa yanayofanywa na wanafunzi wa shule husababisha matokeo duni katika mitihani. Baraza la Mitihani ya Kitaifa (KNEC) hutathmini watahiniwa katika kiwango cha Elimu ya Msingi na Kiswahili ni kati ya masomo ya lazima yanayotahiniwa katika kiwango hiki. Katika siku za hivi karibuni, hasa kati ya 2016 na 2018, utendaji wa wanafunzi katika somo la Kiswahili umekuwa ukizorota na makosa ya kitahajia na kisarufi ni sababu mojawapo ya kudorora huku. Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa kuhakiki makosa katika maandishi ya wanafunzi wa shule za upili katika kaunti ndogo ya Likuyani, kaunti ya Kakamega na katika baadhi ya vitabu vya kiada vya Kiswahili. Malengo mahsusi yalikuwa ni kutambua na kuchanganua makosa ya kitahajia na kisarufi katika maandishi ya wanafunzi na vitabu vya kiada. Tuliongozwa na nadharia tete kwamba makosa katika maandishi na vitabu vya kiada hujidhihirisha kwa namna mbalimbali na kwamba makosa kwenye maandishi ya kiada huigwa na wanafunzi. Tuliongozwa na Nadharia ya Uchanganuzi Makosa iliyofasiliwa na S. P. Corder. Utafiti huu ulifanywa nyanjani na maktabani ambapo tulizuru Shule tisa za Upili katika eneo la utafiti na kusoma vitabu vitatu vya kiada maktabani. Mazoezi matatu ya kuandika yenye Viasho, Jozi za Mlinganuo Finyu na Insha, yalitumiwa ili kupata data ya uchanganuzi. Kwa kufanya utafiti maktabani, tulipata data ya makosa katika vitabu vya kiada. Data ilichanganuliwa kwa kuzingatia utukiaji wake chini ya vipengele vya udondoshaji, uchopekaji na ubadilishaji wa herufi na maneno. Aidha, tulizingatia utenganishaji na uunganishaji wa maneno katika kitengo cha makosa ya kitahajia. Upatanisho wa kisarufi, minyambuliko na uambishaji ni vipengele vingine tulivyozingatia katika kuchanganua data kuhusu makosa ya kisarufi. Matokeo ya utafiti yalidhihirisha kwamba wanafunzi walifanya makosa yanayofanana na makosa yanayopatikana kwenye vitabu vya kiada. Makosa mengine yalitokana na athari za lugha ya kwanza ya wanafunzi. Tunapendekeza kwamba kadiri tunavyojitahidi kukabiliana na athari za lugha ya kwanza kama sababu kuu ya makosa katika Kiswahili, ni sharti kuwe na umakinifu katika uandishi wa vitabu vya kiada kwani makosa yanapokuwamo, huwa na athari hasi kwa wanafunzi. Kushughulikiwa kwa visababishi hivi kutapunguza makosa ya wanafunzi na kuimarisha utendaji wa wanafunzi katika mitihani ya Kiswahili.

## ABSTRACT

Deviating from spelling and grammar rules of any language constitutes errors. Errors committed by learners in language within the school system lead to poor performance in examinations. The Kenya National Examinations Council conducts evaluation of the learners at the Basic Education Level and Kiswahili is one of the compulsory examinable subjects at this level. In the recent past, specifically between 2016 and 2018, there has been a decline in the Form Four candidates' performance in Kiswahili and the identified errors could be responsible for this decline. We therefore, sought to analyse the type and source of the errors among students' written works in Likuyani Sub-County, Kakamega County and some Kiswahili course books. The objectives of this study were to: identify and analyze the spelling and grammatical errors in the written works of students and Kiswahili course books, identify students' errors that are similar to those found in Kiswahili course books and evaluate the sources of these errors. The study was guided by the hypotheses that errors in written works of learners and Kiswahili course books manifest themselves through various forms and that such errors arise from different sources. It was also hypothesized that some errors appearing in Kiswahili course books were replicated by learners in their written works. The study was guided by the Error Analysis Theory that was expounded by S. P. Corder. We conducted a field study in a sample of Form Two students from nine (9) Secondary Schools in the area of study and a library research in three (3) secondary school Kiswahili course books. Three written tests of a Cloze Test, Minimal Pairs and an Essay were administered to students in order to obtain the research data. Through library research, we identified errors from sampled course books. These errors were analyzed based on such research issues as: omissions, insertions, interchange of letters or words, and word separation and joining of separate words. Other categories used to analyse grammatical errors were subject agreement in respect of other types of words, word expansion and affixation. The results of the research showed that learners committed some errors which were similar or identical to those found in course books while other errors were as a result of the interference from their first language. We recommend that as efforts are made to contain errors caused by first language influence, course books should be carefully written in order to prevent errors occurring in such publications since they negatively impact on students. Once the causes have been addressed, these errors would be minimized and the net effect would be improvement in the performance of students in Kiswahili in the national examinations.

# YALIYOMO

UNGAMO....ii
TABARUKU .... iii
SHUKRANI....iv
IKISIRI ....vi
ABSTRACT....vii
YALIYOMO.... viii
ORODHA YA JEDWALI ....xii
ORODHA YA PICHA.... xiii
MAELEZO YA VIFUPISHO....xiv
**SURA YA KWANZA ....1**
**MISINGI YA UTAFITI ....1**
1.0 Utangulizi....1
1.1 Usuli wa Suala la Utafiti....1
1.2 Suala la Utafiti ....6
1.3 Malengo ya Utafiti ....7
1.4 Nadharia Tete....7
1.5 Sababu za Uteuzi wa Mada....8
1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti....10
1.7 Hitimisho....14
**SURA YA PILI....15**
**KIUNZI CHA NADHARIA NA MAPITIO YA MAANDISHI....15**
2.0 Utangulizi....15
2.1 Maandishi Kuhusu Aina za Makosa ....15
2.1.1 Maandishi kuhusu makosa ya tahajia....15
2.1.2 Maandishi kuhusu makosa ya kisarufi ....19
2.2 Tahakiki kuhusu Asili ya Makosa na Jinsi ya Kuyakabili....24
2.3 Misingi ya Kinadharia....27
2.3.1 Nadharia ya Uchanganuzi Makosa....27
2.3.2 Mihimili ya Nadharia ya Uchanganuzi Makosa....29
2.4 Hitimisho....33
**SURA YA TATU....34**
**MBINU ZA UTAFITI....34**

3.0 Utangulizi....34
3.1 Muundo wa Utafiti....34
3.2 Eneo la Utafiti....34
3.3 Vifaa vya Utafiti....36
3.3.1 Zoezi la viasho....36
3.3.2 Zoezi la jozi za mlinganuo finyu....37
3.3.3 Zoezi la insha....38
3.4 Ukusanyaji wa Data....39
3.5 Uwasilishaji wa Data....40
3.6 Uchambuzi wa Data....41
3.7 Hitimisho....42
**SURA YA NNE....43**
**UHAKIKI WA MAKOSA YA KITAHAJIA....43**
4.0 Utangulizi....43
4.1 Kudondosha Herufi....44
4.1.1 Kudondosha konsonanti: maandishi ya wanafunzi....44
4.1.2 Kudondosha konsonanti: vitabu vya kiada....48
4.1.3 Kudondosha silabi: maandishi ya wanafunzi....50
4.1.4 Kudondosha silabi: vitabu vya kiada....51
4.2 Kuchopeka Herufi....54
4.3 Kubadilisha Herufi....56
4.3.1 Kubadilisha herufi: maandishi ya wanafunzi....57
4.3.2 Kubadilisha herufi: vitabu vya kiada....64
4.4 Kutenganisha neno: maandishi ya wanafunzi....66
4.5 Kuunganisha Maneno....68
4.5.1 Kuunganisha maneno: maandishi ya wanafunzi....68
4.5.2 Kuunganisha maneno: vitabu vya kiada....70
4.6 Hitimisho....71
**SURA YA TANO....73**
**UHAKIKI WA MAKOSA YA KISARUFI....73**
5.0 Utangulizi....73
5.1 Kudondosha Maneno: Maandishi ya Wanafunzi....73
5.2 Kudondosha Maneno: Vitabu vya kiada....75
5.3 Kuchopeka Maneno: maandishi ya wanafunzi....79

5.4 Kuchopeka Maneno: vitabu vya kiada ......85
5.5 Upatanisho wa Kisarufi ......95
5.5.1 Upatanisho katika vitenzi: maandishi ya wanafunzi ......95
5.5.2 Upatanisho katika vitenzi: vitabu vya kiada ......98
5.5.3 Upatanisho wa vivumishi, vihusishi na virejeshi: maandishi ya wanafunzi ......100
5.5.4 Upatanisho katika vivumishi, vihusishi na virejeshi: vitabu vya kiada ......105
5.6 Minyambuliko Isiyokubalika ......108
5.6.1 Mnyambuliko usioafikiana na muktadha: maandishi ya wanafunzi ......109
5.6.2 Mnyambuliko usioafikiana na muktadha: vitabu vya kiada ......111
5.6.3 Kushindwa Kunyambua ......114
5.7 Makosa ya Uambishaji ......116
5.7.1 Makosa ya uambishaji: maandishi ya wanafunzi ......116
5.7.2 Makosa ya uambishaji: vitabu vya kiada ......119
5.8 Hitimisho ......120
**SURA YA SITA ......122**
**VYANZO VYA MAKOSA KATIKA MAANDISHI ......122**
6.0 Utangulizi ......122
6.1 Sababu za Makosa katika Maandishi ya Wanafunzi ......122
6.1.1 Makosa yaliyotokana na athari za lugha ya kwanza ......122
6.1.1.1 Makosa ya wanafunzi wa Kikalenjin ......123
6.1.1.2 Makosa ya wanafunzi Wakikuyu ......124
6.1.1.3 Makosa ya wanafunzi wa Kiluo ......125
6.1.1.4 Makosa ya wanafunzi wa Kiteso ......126
6.1.1.5 Makosa ya wanafunzi wa Kiluhya ......126
6.1.2 Makosa yanayotokana na vitabu vya kiada ......127
6.1.3 Makosa yanayotokana na ujumlishaji unaopita kiasi ......128
6.1.4 Makosa yanayotokana na athari za kijamii ......129
6.1.5 Makosa ya ulegevu wa kujiandaa ......130
6.2 Vyanzo vya Makosa katika Vitabu vya Kiada ......131
6.3 Hitimisho ......135
**SURA YA SABA ......136**
**MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI ......136**
7.0 Utangulizi ......136
7.1 Muhtasari wa Tasnifu ......136

7.2 Hitimisho la Utafiti ........ 137
7.2.1 Makosa ya kitahajia ........ 137
7.2.2 Makosa ya kisarufi ........ 139
7.2.3 Vyanzo vya makosa ........ 141
7.3 Mchango wa Utafiti ........ 143
7.4 Mapendekezo ya Utafiti ........ 144
MAREJELEO ........ 147
VIAMBATISHO ........ 152
Kiambatisho A: Makosa Katika Maandishi ya Wanafunzi ........ 152
Kiambatisho B: Makosa Katika *Uhondo Wa Kiswahili* ........ 157
Kiambatisho C: Makosa Katika *Kiswahili Kitukuzwe Kidato Cha Pili* ........ 160
Kiambatisho D: Makosa Katika *Kiswahili Fasaha Kidato Cha Pili Toleo Jipya 2015* ........ 162
Kiambatisho E: Zoezi la Kwanza: Viasho ........ 166
Kiambatisho F: Zoezi la Pili: Utungaji wa Sentensi ........ 167
Kiambatisho G: Zoezi la Tatu: Kuandika Insha ........ 168
Kiambatisho H: Idhini ya Utafiti ........ 169

# ORODHA YA JEDWALI

Jedwali 1.1: Matokeo ya Kiswahili ya KCSE ya kaunti ndogo ya Likuyani ................. 3
Jedwali 4.1: Konsonanti za Nandi na Kipsigis ........................................................... 46
Jedwali 7.1 : Makosa ya kisarufi: Utukiaji katika MYW .......................................... 139
Jedwali 7.2: Makosa katika MYW yaliyohusiana na VVK ....................................... 142
Jedwali 7.3: Idadi ya makosa katika kila kitabu dhidi ya idadi ya kurasa ................. 143

# ORODHA YA PICHA

Mchoroduara 7.1: Ulinganishaji wa makosa ya hijai katika VVK ............................138
Mchoroduara 7.2: Ulinganishaji wa makosa ya kisarufi katika VVK ........................140
Mchoroduara 7.3: Ulinganishaji wa makosa kijumla katika VVK............................141

## MAELEZO YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| **KCSE** | Kenya Certificate of Secondary Education |
| **KF** | Kiswahili Fasaha |
| **KICD** | Kenya Institute of Curriculum Development |
| **KK** | Kiswahili Kitukuzwe |
| **MYW** | Maandishi Ya Wanafunzi |
| **Uk** | Ukurasa |
| **UWK** | Uhondo wa Kiswahili |
| **VVK** | Vitabu Vya Kiada |
| **Λ** | Alama inayomaanisha neno limedondoshwa |

# SURA YA KWANZA

# MISINGI YA UTAFITI

## 1.0 Utangulizi

Katika sura hii tumeshughulikia usuli wa suala la utafiti na malengo ya utafiti wetu. Aidha tumetambua nadharia tete, tukaeleza sababu za uteuzi wa mada hii na kuonyesha upeo na mipaka ya utafiti wetu.

## 1.1 Usuli wa Suala la Utafiti

Lugha inaelezwa kwa namna mbalimbali. *Kamusi ya Karne ya 21* inaeleza lugha kuwa mfumo wa sauti nasibu unaotumiwa na jamii fulani kuwasiliana (uk.269). Nayo *Kamusi ya Kiswahili Sanifu TUKI Toleo la 4***,** (uk.332) inafafanua lugha kama mpangilio wa sauti na maneno unaoleta maana na ambao hutumiwa na watu wa taifa au kundi fulani kwa ajili ya kuwasiliana. Kutokana na fafanuzi hizi, tunatambua kwamba kila lugha ina vipengele vitatu. Kwanza, ina kundi la watu wanaoizungumza, pili, huwasilisha ujumbe kwa kuwezesha mawasiliano kutokea baina ya wanajamii husika na tatu, ina mpangilio wake. Mpangilio huu ndio hujumuisha kanuni zinazostahili kuzingatiwa na yeyote anayeitumia lugha husika. Kama lugha nyingine kubwa ulimwenguni, Kiswahili ni lugha inayoendelea kukua na kupata umaarufu mkubwa ulimwenguni. Idadi ya watumiaji Kiswahili inaendelea kuongezeka kila siku. Ikumbukwe pia kwamba, Kiswahili ni moja ya lugha za asili ya Kiafrika pamoja na Kihausa, Kiyoruba, Kioromo, Kiigbo, Kizulu, Kiamharic na Kiberber. Kufikia mwaka 2015 Kiswahili kilikuwa na zaidi ya wasemaji milioni 90 Barani Afrika na ndiyo lugha maarufu na yenye wasemaji wengi zaidi wa asili ya Kiafrika katika Bara la Afrika kuliko lugha hizo nyingine. Ni kwa sababu ya kuendelea kuimarika kwake ambapo tafiti mbalimbali zinastahiki kufanywa kuhusu Kiswahili ili katika kukua kwake iendelee kudumisha sarufi yake.

Kihore na wenzake (2008) wanaeleza sarufi kuwa sayansi ya muundo wa lugha pamoja na sheria na kanuni za matumizi yanayokubalika kwa watumiaji wake. Kukubalika au kukataliwa kwa tungo yoyote katika lugha hutegemea kanuni zake. Kwa mujibu wa Besha (1994), kutii kanuni za kisarufi za lugha fulani huitwa **usarufi** ilhali **utosarufi** ni ukiukaji wa kanuni za lugha. Utafiti wetu umejengwa katika misingi kwamba watu wanaojifunza lugha hutokea kuwa na utosarufi katika tungo zao. Huu utosarufi ndio tutakaorejelea kwa istilahi ya '**makosa**' katika utafiti huu.

Katika kazi hii, tulitathmini makosa yaliyofanywa katika MYW wa shule za upili. Aidha**,** kwa sababu wanafunzi hutumia vitabu mbalimbali katika mafunzo yao shuleni, tulichambua makosa yaliyotokea katika baadhi ya vitabu vya kiada vinavyotumiwa na wanafunzi katika mafunzo yao shuleni. Tuliufanya uamuzi huu kwa ajili ya kujaribu kudadisi vyanzo vya aina mbalimbali za makosa kama yanavyotokea katika kazi za wanafunzi wa shule za upili. Tulipata msukumo wa kufanya utafiti wetu katika utendaji wa wanafunzi kwenye mitihani ya Kiswahili ya kidato cha nne katika kiwango cha kitaifa. Umilisi wa wanafunzi katika stadi zote za Kiswahili kufikia kiwango cha mtihani wa mwisho wa kidato cha nne hupimwa kupitia stadi ya kuandika. Madhali majibu yao yote huwasilishwa kwa njia ya maandishi, linakuwa jambo la lazima kwa wanafunzi kumakinika katika stadi ya kuandika.

Kiswahili ni somo la lazima linalotahiniwa katika shule zote nchini Kenya. Kwa wanafunzi wengi, Kiswahili ni lugha ya pili ikizingatiwa kwamba lugha yao ya kwanza ni ya mama. Hali ni tofauti katika shule zilizo katika sehemu nyingi za pwani ambapo Kiswahili ni lugha ya kwanza ya wanafunzi hawa. Katika harakati za kujifunza Kiswahili, wanafunzi wengi hufanya makosa kwa kukiuka kanuni za lugha

hii. Huku kukiuka kanuni za lugha huathiri uelewa wao wa lugha hii. Kwa kufanya hivi wanadhihirisha upungufu wao katika umilisi wao wa Kiswahili. Upungufu wao huonekana katika utendaji wao kuhusiana na jinsi wanavyoandika. Matokeo yao katika uandishi wa insha na sarufi yanakuwa duni.

Kulingana na takwimu kutoka katika Baraza la Kitaifa la Mitihani nchini Kenya (KNEC), matokeo ya wanafunzi katika somo la Kiswahili yanazidi kushuka. Kwa mfano, baina ya 2015 na 2017, alama ya wastani ya kitaifa katika Kiswahili ilikuwa 95.75, 77.97 na 69.43 juu ya alama 200. Baina ya miaka hiyo, alama ya wastani ya matokeo ya shule za upili katika Kiswahili kwenye Kaunti ndogo ya Likuyani ilikuwa 5.105 (2015), 4.815 (2016) na 3.932 (2017) juu ya alama 12. (Taz. Jedwali 1.1)

**Jedwali 1.1: Matokeo ya Kiswahili ya KCSE ya kaunti ndogo ya Likuyani**

| **Mwaka**<br>**Shule** | **2015** | **2016** | **2017** |
|---|---|---|---|
| Friend's Mbururu | 7.660 | 5.457 | 4.822 |
| St Michael's Kilimani | 5.306 | 5.721 | 3.672 |
| St Joseph's Kogo | 6.150 | 5.614 | 3.634 |
| St Peter's Machine | 5.442 | 6.421 | 4.024 |
| St Augustin's Soysambu | 6.329 | 5.205 | 3.901 |
| Friend's Kongoni | 3.896 | 4.418 | 3.915 |
| Friend's Binyenya | 4.767 | 4.227 | 4.107 |
| St Joseph's Lumino | 4.109 | 3.632 | 3.122 |
| St John's Mutoni | 3.431 | 3.410 | 3.552 |
| Alama ya wastani ya Kaunti Ndogo | 5.105 | 4.815 | 3.932 |

*Asili: Afisi ya Elimu Kaunti Ndogo ya Likuyani*

Takwimu hizi zinadhihirisha mporomoko wa utendaji wa watahiniwa katika Kiswahili katika kipindi hicho.

Wakati wa kutahini kazi za wanafunzi katika mitihani ya kitaifa, makosa wanayofanya huchunguzwa. Karatasi ya Kwanza hutahini Insha ilhali Lugha hutahiniwa katika Karatasi ya Pili. Mathalani, katika mtihani wa Lugha, athari ya

makosa ya kitahajia na kisarufi katika utendaji wa wanafunzi ni ya moja kwa moja kwa sababu mbali na kukosa kuwasilisha ujumbe vizuri, alama za mwanafunzi husika hupunguzwa kulingana na idadi ya makosa. Makosa yanapokuwa mengi, alama anazopoteza mwanafunzi zinaongezeka. Hatimaye, makosa yanaathiri utendaji wa wanafunzi katika somo hili na kufanya matokeo ya Kiswahili kudorora. Huku kudorora kwa utendaji wa wanafunzi ni tatizo linalostahili kushughuliwa na watafiti ili kuimarisha Kiswahili.

Makosa yanayotokea katika Kuzungumza na Kusoma hujidhihirisha katika Kuandika. Mazungumzo ya wanafunzi huathiriwa na lugha yao ya kwanza ambapo, kwa sababu ya tofauti za kifonolojia baina ya lugha yao ya kwanza na Kiswahili ambayo ni lugha ya pili, sauti ambazo ni ngeni kwao huwatatiza katika kuzitamka na hapo wanafanya makosa katika kuandika maneno. Aghalabu, makosa ya aina hii huwa ni ya kitahajia. Kadhalika, katika harakati za ujifunzaji lugha, wanafunzi husikiliza jinsi watumiaji wengine wa lugha wanavyozungumza lugha husika na wanaweza kuwaiga na endapo wanajamii hawa watakuwa na matumizi potofu ya lugha, haya matumizi potofu yataigwa na wanafunzi na yatajitokeza katika utendaji wao wanapoandika. Makosa ya aina hii huwa na asili yake miongoni mwa wanajamii.

Kwa sababu kusoma ni stadi nyingine ya kujifunza lugha, kuna vitabu ambavyo hutumiwa na wanafunzi wengi katika mafunzo yao. Kati ya vitabu hivi, kunavyo vya fasihi ambavyo huteuliwa kwa minajili ya mtihani wa Fasihi ya Kiswahili unaotahiniwa katika Karatasi ya Tatu. Aidha, kuna vitabu vingine vya mafunzo vinavyoidhinishwa ili kutumiwa na wanafunzi shuleni. Hivi huitwa vitabu vya kiada.

Uchapishaji wa vitabu vya shule ulifanywa kuwa huru mwaka wa 2003 ambapo serikali ya Kenya iliruhusu mashirika ya kibinafsi kuchapisha vitabu vya kiada. Kabla

ya mwaka huo, vitabu vya kiada vilikuwa vinachapishwa na Kampuni za Jomo Kenyatta na Kenya Literature Bureau. Kampuni hizi zilimilikiwa na Serikali ya Kenya. Katika mabadiliko haya, mashirika ya kibinafsi yalipewa uhuru wa kuchapisha vitabu vya kiada. Katika harakati zao za kuandaa vitabu vya kiada, kampuni hizi zina uhuru wa kuchagua waandishi wowote ili kuandika vitabu ambavyo baadaye zinavichapisha. Hata hivyo, ikiwa wachapishaji wa vitabu hivi wanataka vitabu vyao viidhinishwe kuwa vitabu vya kiada, ni lazima nakala zake ziwasilishwe kwa Wizara ya Elimu ya Kimsingi kupitia kwa Taasisi ya Ukuzaji Mitaala nchini Kenya (KICD) kwa ukaguzi. Vitabu vinavyoidhinishwa hutambulika kwa kuwekewa alama maalumu pamoja na maandishi '*Kimeidhinishwa na KICD'*. Sio vitabu vyote vinavyowasilishwa kwa ukaguzi huidhinishwa. Sababu za kutoidhinishwa kwa baadhi ya vitabu, kijumla, huwa kwamba vina upungufu wa namna fulani. Hata hivyo, ilmuradi nakala za vitabu hivi huwa zimesambaa, wanafunzi hawawezi kuzuiwa kutagusana navyo madukani na maktabani. Hata vitabu vinavyoidhinishwa na wizara ya elimu kutumiwa shuleni vinatokea kuwa na kasoro mbalimbali ambazo huathiri wanafunzi wanaovitumia katika mafunzo yao.

Baadhi ya makosa katika MYW hufanana na yale yaliyo katika vitabu vya mafunzo ambavyo wanatumia shuleni. Hii ni ishara kwamba lipo tatizo katika uandalizi wa vitabu vya kiada na hata maafisa wanaoidhinisha vitabu hivi wana utepetevu wa namna fulani katika utenda kazi wao. Hii ndiyo maana makosa yanapatikana katika vitabu vya kiada vilivyoidhinishwa sawasawa na yalivyo katika vitabu ambavyo havijaidhinishwa. Tulihakiki makosa katika VVK na ambavyo tunajua kwamba vinasomwa na wanafunzi wengi, tukilenga kutathmini kama vina makosa na ikiwa makosa haya yana uhusiano na yale yanayofanywa na wanafunzi katika maandishi yao.

Makosa yanayofanywa katika matumizi ya lugha yanaweza kugawanywa katika makundi mbalimbali. Katika muktadha wa utafiti wetu, tulitenga makosa katika makundi mawili ya tahajia na sarufi. Makosa ya kila kundi yalijidhihirisha kwa njia zinazotofautiana kama itakavyoonekana katika utafiti wetu. Kwa hivyo, utafiti wetu ulichunguza, kwa kutumia istilahi aliyobuni Besha, **utosarufi**, katika maandishi ya wanafunzi wa shule za upili na baadhi ya vitabu vya mafunzo na kuchunguza asili za makosa haya.

## 1.2 Suala la Utafiti

Makosa ya kitahajia na kisarufi hutokea katika harakati za kujifunza lugha ya pili. Makosa yenyewe hudhihirika kupitia maandishi na matamshi ya wanaojifunza lugha husika na yanaweza kudhihirika kupitia namna mbalimbali kama vile udondoshaji, uchopekaji, ubadilishaji wa herufi, neno au maneno. Mathalani, mwanafunzi wa lugha ya pili anapokumbana na muundo mpya ambao hauko katika lugha yake ya kwanza huenda akabuni namna mbalimbali za kuukabili kama vile kuudondosha, kuuchopeka au kuubadili muundo wenyewe. Katika kufanya hivi, muundo mpya unaotokea unaweza kukosa kukubalika katika lugha ya pili na kwa hivyo kuwa makosa katika lugha hiyo. Kadhalika, njia nyingine ya kudhihirika kwa makosa hayo ni kubadilisha mpangilio wa maneno katika sentensi na kutokea kwa mpangilio usiokubaliana na lugha ya pili.

Maandishi yanaposheheni makosa ya hijai na sarufi, huvuruga mawasiliano kwa vile ujumbe unaweza kukosa kumfikia mlengwa jinsi ilivyotarajiwa. Athari ya makosa hayo ni kutatizwa kwa mawasiliano. Msomaji hutambua kwamba mwandishi ana udhaifu katika lugha anayoandikia na kwamba maandishi hayo yana thamani duni. Kwa upande wa mwanafunzi wa shule, athari ya makosa hayo ni kupata matokeo duni

katika mtihani wake madhali hataweza kuwasilisha ujumbe wake na kueleweka. Ili kurekebisha maandishi yenye dosari, sharti kutambua makosa yaliyomo kwa kuzingatia aina zake, kuchunguza asili zake na hatimaye kupendekeza njia za kukabiliana nayo.

Kufanya hivi ni kumsaidia mwanafunzi anayejifunza lugha kuyarekebisha makosa yake katika lugha hiyo na kupata matokeo bora katika mtihani wake.

## 1.3 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu ulinuia kutimiza malengo yafuatayo:

i. Kufafanua makosa ya kitahajia yanayojitokeza katika maandishi ya wanafunzi wa shule za upili na vitabu vya kiada vinavyotumiwa na wanafunzi darasani.

ii. Kuchambua makosa ya kisarufi yanayojitokeza katika maandishi ya wanafunzi wa shule za upili na vitabu vya kiada vinavyotumiwa na wanafunzi darasani.

**iii.** Kutathmini chimbuko la makosa ya kitahajia na kisarufi katika maandishi ya wanafunzi na vitabu vya kiada.

## 1.4 Nadharia Tete

Ili kutimiza malengo ya utafiti huu, tuliongozwa na nadharia tete zifuatazo:

i. Makosa ya kitahajia katika maandishi ya wanafunzi wa shule za upili na baadhi ya vitabu vya kiada vinavyotumiwa na wanafunzi darasani hujidhihirisha kwa namna mbalimbali.

ii. Makosa ya kisarufi yanadhihirika kwa namna tofautitofauti katika maandishi ya wanafunzi wa shule za upili na baadhi ya vitabu vya kiada wanavyotumia darasani.

iii. Makosa ya kitahajia na kisarufi katika maandishi ya wanafunzi na vitabu vya kiada yana visababishi anuwai.

### 1.5 Sababu za Uteuzi wa Mada

Uteuzi wa mada hii ulichochewa na sababu kwamba makosa yanayofanywa na wanafunzi yana athari hasi katika utendaji wao kwenye mitihani yao. Lugha ya kwanza ya mwanafunzi pamoja na lugha nyingine anazokumbana nazo mwanafunzi huathiri ujifunzaji wake wa lugha ngeni. Ni muhimu kuchunguza makosa ili kutambua asili yake ndipo njia za kuyakabili zipendekezwe. Mchakato huu utajenga msingi unaotegemewa katika kukabiliana na makosa yanayofanywa katika maandishi ya wanafunzi. Aidha, waandaaji wa vitabu vya kiada watafaidi utafiti huu kwani makosa yanayotokea katika kazi zao yatawekwa wazi na kwa njia hii watatambua haja ya kuzingatia umakinifu wanapoandaa vitabu vyao.

Vilevile, matokeo ya utafiti huu yatakuwa na manufaa kwa Wizara ya Elimu kwa kuitambulishia kwamba baadhi ya kazi zinazotumiwa shuleni katika mafunzo ya wanafunzi zina makosa ambayo yanawaathiri wanafunzi licha ya kwamba baadhi ya kazi huwa zimeidhinishwa na wizara yenyewe. Kwa hivyo, kuna haja ya kuwa makini wakati wa kuzikagua kazi zinazowasilishwa kwao kabla ya kuidhinishwa ili kutumiwa shuleni. Uchunguzi wa mara kwa mara nyanjani wa vitabu vinavyotumiwa katika mafunzo shuleni ni muhimu ili kuhakikisha ya kwamba vitabu ambavyo havijaidhinishwa haviuzwi madukani wala kutumiwa katika shule. Kwa njia hii, wanafunzi wataepushwa na kazi zenye makosa.

Isitoshe, kufunguliwa kwa soko huru katika eneo la Afrika Mashariki mnamo Juni 2010, kuliashiria kuwa maingiliano miongoni mwa wananchi wa nchi husika yangeongezeka. Pana uwezekano wa ushirikiano huu kuhusisha uwanja wa elimu ambapo panahitajika mtaala wa pamoja wa kufundishia Kiswahili ambayo ndiyo lugha ya mawasiliano mapana katika eneo hili. Kuwepo kwa vitabu ambavyo havina makosa ni muhimu katika kufanikisha mchakato huu na kuwaepusha wanafunzi

kufanya makosa kwa kuyaiga makosa haya kutoka katika vitabu vya kiada shuleni. Matokeo ya utafiti yatafaidi harakati za kuandaa mtaala wa kufundishia Kiswahili katika shule kwa vile maandalizi mazuri ya mtaala huzingatia mahitaji ya wanafunzi.

Umaarufu na umuhimu wa Kiswahili unaendelea kuimarika kila uchao na sharti kuwepo na machapisho ya Kiswahili yasiyo na makosa ili wanaojifunza lugha hiyo wazingatie usanifu wake. Mathalani, Wizara ya Elimu nchini Afrika Kusini kupitia waziri wake Angie Motshekga, mnamo Septemba 18, 2018 ilitangaza kwamba kuanzia mwaka wa 2020 Kiswahili kitaanza kufundishwa katika shule za Afrika Kusini kama lugha mojawapo kwa lengo la kustawisha umoja na mshikamano wa kijamii. Tangazo hili limeanza kutekelezwa Januari 2020 katika shule zote nchini humo. Aidha, nchini Rwanda, Kiswahili kimepewa umuhimu wa kufunzwa katika shule zote na kuchukua nafasi ya Kifaransa. Kiswahili kinaendelea kupata umaarufu katika maeneo mengi Barani Afrika hasa maeneo ya Mashariki, Kati na Kusini. Kwa hivyo, ni muhimu kuhakikisha ya kwamba Kiswahili kimetumiwa kwa kuzingatia kanuni zake kama zilivyo lugha nyingine ulimwenguni.

Makosa yanaashiria kile ambacho mwanafunzi anahitaji kufunzwa tena. Utafiti huu utawafaa wanafunzi wanapofanya marudio kwa ajili ya mitihani yao. Mchakato wa kujifunza hutegemea maamuzi na uhusika wa wanafunzi wenyewe pamoja na tajriba yao maishani. Kwa hivyo, ni muhimu kuwa na ufahamu huu katika harakati za kuelewa namna ujifunzaji wa lugha ya pili unavyotokea.

Waaidha, umaarufu wa Kiswahili umefikia kiwango cha kutumiwa kwake kama lugha ya kimtandao hivi kwamba mbali na kutumiwa kama lugha mojawapo katika simutamba, mnamo Mei 2018 ilijumuishwa kama moja kati ya lugha zinazotumiwa

katika mtandao wa 'Twitter'. Ikumbukwe kwamba hivi sasa matandao wa 'Facebook' umejumuisha Kiswahili miongoni mwa lugha zake.

Uteuzi wa mada hii umenuia kutoa mchango wa kitaaluma hasa kwa upande wa walimu, wakuza mitaala na waandishi wa vitabu vya mafunzo. Kupitia kwa matokeo ya utafiti wetu, washika dau hawa watatambua mapengo yaliyopo katika uandalizi wa matini ya kufunzia wanafunzi na kuchukua hatua za kuziba mapengo hayo ili kazi zinazotumiwa na walimu kuwafunzia wanafunzi ziondolewe makosa ya kisarufi na kitahajia kwa sababu ya athari zake hasi kwa wanafunzi. Ni sababu hizi zilizotufanya kuteua mada hii katika utafiti wetu.

**1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti**

Eneo la utafiti lilikuwa Kaunti Ndogo ya Likuyani, katika Kaunti ya Kakamega. Kabla ya kuanza kutekelezwa kwa Katiba ya Kenya ya 2010, eneo hili lilikuwa katika Mkoa wa Magharibi. Hili ni eneo linalokaliwa na jamiimseto za Wakenya. Utafiti huu ulihusisha wanafunzi wa kidato cha pili katika shule za upili za kutwa. Sababu ya kuteua shule za kutwa katika kufanya utafiti huu ni kwamba hizo ndizo zilikuwa na wanafunzi ambao ni wakazi wa kaunti ndogo hii na kwa hivyo ziliwakilisha hali halisi ya jamiimseto. Tulipendelea jamiimseto kwa sababu tulitaka kuhusisha wanafunzi kutoka jamii mbalimbali zilizo nchini ili kuwa na uwanja mpana wa kutambua aina mbalimbali za makosa yanayohusishwa na jamii fulani. Usampuli wetu uliteua shule tisa (9) kati ya shule 34 za kutwa zilizo katika Kaunti Ndogo ya Likuyani. Idadi hii ilikuwa zaidi ya asilimia 25 ya shule za upili katika kaunti hii ndogo. Uteuzi wa kidato cha pili ulitokana na sababu zifuatazo: Kwanza, kufikia mwisho wa kidato cha pili wanafunzi hutarajiwa kuwa wamemakinika katika stadi za kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika. Kadhalika, wanafunzi wa kiwango hiki huhitajika kuwa wamefunzwa dhana zote za kisarufi katika lugha. Kidato hiki ni cha mpito kabla

ya kujiunga na vidato vya juu ambapo dhana zinashughulikiwa katika upana na kina wala sio upya tena. Matarajio ya mtaala ni kwamba wanafunzi wa kidato hiki watakuwa wamepata umilisi wa kutosha katika stadi za lugha. Sababu nyingine ni kwamba udhaifu unapotambuliwa katika kidato cha pili, hatua za kurekebisha makosa zinaweza kuchukuliwa kwa sababu ya kuwa na muda wa kutosha. Hii ni tofauti na wanafunzi wa kidato cha kwanza ambao huwa katika mada tangulizi na kwa hivyo hawajafunzwa dhana zote za lugha. Kwa hivyo umilisi wao katika lugha haujafikia kiwango cha juu. Aidha, tafiti zilizofanywa awali na akina Rapando (2005) na Ontieri (2010) zilishughulikia kazi za wanafunzi wa kidato cha tatu. Tuliona haja ya kuchunguza hali ilivyo katika kidato cha pili.

Ili kuchunguza makosa katika vitabu vya kiada, tuliteua vitabu vitatu; kimoja cha kidato cha kwanza na viwili vya kidato cha pili. Kitabu cha kidato cha kwanza kilikuwa *Uhondo wa Kiswahili, Kitabu cha Wanafunzi,* kilichochapishwa na Moran Publishers ambacho kilikuwa kimeidhinishwa na Wizara ya Elimu kwa ajili ya kutumiwa shuleni ilhali vile vya kidato cha pili vilikuwa *Kiswahili Fasaha Kidato cha 2, Toleo la 2015,* kilichochapishwa na Oxford University Press, na *Kiswahili Kitukuzwe Kidato cha 2, Kitabu cha Wanafunzi, Toleo la Sita 2018,* kilichochapishwa na Kenya Literature Bureau Publishers and Printers. Uteuzi wa kitabu kimoja cha kidato cha kwanza ulitokana na sababu kwamba ilmuradi wanafunzi tuliokuwa tunafanyia utafiti walikuwa wamemaliza kidato cha kwanza, walikuwa wametagusana na kitabu hiki na kwa hivyo kikaathiri mafunzo yao. Tuliteua vitabu viwili vya kidato cha pili kwa sababu utafiti wetu ulihusu wanafunzi wa kidato cha pili. Kimoja kati ya vitabu vya kidato cha pili tulivyochunguza hakikuwa na idhini ya kutumiwa kutoka kwa Wizara ya Elimu. Licha ya kukosa idhini ya Wizara ya Elimu kulikuwa na uwezekano wa kitabu hiki kutumiwa shuleni katika mafunzo ya wanafunzi kwa

sababu ya kinauzwa madukani. Hakuna hatua inayochukuliwa na serikali kuhakikisha ya kwamba kitabu chochote kisichokuwa na idhini ya Wizara kimeondolewa madukani ili kisiwafikie wanafunzi. Kwa maoni yetu uteuzi huu wa maandishi ya kiada tuliuona ukiwa wakilishi tosha kwa ajili ya utafiti wetu.

Mada ya uchanganuzi wa makosa katika lugha ni pana. Kwa mujibu wa Elis (1997), makosa katika lugha yanatokea katika makundi makuu mawili. Kundi la kwanza ni la makosa yanayotokea bila kutarajia na ambayo, kulingana na Elis, mwanafunzi wa lugha anaweza kuyasahihisha akipata fursa nyingine ya kuhariri maongezi au maandishi yake. Ingawa mwanafunzi wa lugha anaweza kufanya makosa ya aina hii, haifai makosa ya aina hii kutokea katika machapisho rasmi kama VVK kwa sababu ni mfano mbaya kwa wanafunzi madhali wataiga mtindo wa kutojali. Aidha, kwa sababu maandishi haya ni rasmi, baadhi ya wanafunzi wanaweza kuiga makosa haya. Kundi la pili linahusu makosa yanayoashiria hali ya kutojua na haya hudhihirisha kuwa mtumiaji lugha hana umilisi wa kutosha katika lugha. Katika utafiti wetu tulizingatia aina ya pili ya makosa katika maandishi ya wanafunzi kwa sababu lengo la utafiti huu lilikuwa kutathmini umilisi wa mwanafunzi katika Kiswahili. Hata hivyo, katika VVK, tulichunguza aina zote mbili za makosa kwa sababu kazi rasmi zinastahiki kuepukana na aina yoyote ya makosa.

Uchanganuzi wa makosa huzingatia vigezo mbalimbali kama vile ulinganishaji wa miundo ya lugha mbili, uwasilishaji wa dhana potofu, udhaifu au ukosefu wa kukumbuka dhana fulani na kukosa ufahamu wa dhana katika lugha. Kadhalika, makosa katika lugha yanaweza kudhihirika katika kategoria mbalimbali kama vile udondoshaji wa elementi muhimu, uchopezi wa elementi isiyofaa yaani isiyo sahihi, ubadilishaji wa elementi na upangaji wa elementi. Miongoni mwa mambo hayo,

utafiti wetu ulijikita katika uteuzi wa matini za lugha na kutambua makosa yaliyo katika matini hizo. Tuliyapanga baadaye katika kategoria zake kuu za tahajia na sarufi na kuthibitisha namna yalivyodhihirika kisha tukafafanua vyanzo vya makosa yenyewe. Hatimaye tulitathmini kiwango cha makosa katika VVK kwa kulinganisha idadi ya makosa na jumla ya kurasa katika kitabu chenyewe. Utafiti wetu ulifuata dhana ya nadharia hii inayodai kwamba makosa katika ujifunzaji lugha ya pili hayatokei kiholela bali hufuata mfumo maalum na kadhalika kwamba makosa katika lugha ya pili yanaweza kusababishwa na athari kutoka lugha ya kwanza ya mwanafunzi**.**

Kunazo nadharia mbalimbali kuhusu uchanganuzi wa makosa katika lugha. Miongoni mwa nadharia hizi ni Uchanganuzi Linganuzi na Mwingiliano Lugha zilizoasisiwa na Lado (1957), Uchanganuzi Makosa ya Corder (1967) na ile ya Lugha Mpito iliyobuniwa na Selinker (1972). Kwa ajili ya utafiti wetu tuliteua Nadharia ya Uchanganuzi Makosa ya Corder kwa sababu tulizingatia hatua za kuchanganua makosa zilizopendekezwa na nadharia hii yaani uteuzi wa matini ya kimaandishi, utambuzi wa makosa katika maandishi, kuratibu kwa makosa katika kategoria, kueleza vyanzo vya makosa na kutathmini viwango vya, na kina cha kila aina ya makosa. Hata hivyo, tulirejelea mhimili mmoja wa Nadharia ya Uchanganuzi Linganuzi inayodai kwamba lugha ya kwanza ya mtu humwathiri anayejifunza lugha ya pili kwa kudhihirisha makosa yanayohusiana na lugha yake ya kwanza. Tulitambua kwamba baadhi ya makosa yaliyotokea katika maandishi ya wanafunzi yalitokana na athari za lugha zao za kwanza.

## 1.7 Hitimisho

Katika sura hii tumejadili masuala mbalimbali yanayojenga misingi ya utafiti wetu kuhusu mada ya uchanganuzi wa makosa katika maandishi ya wanafunzi na machapisho ya kiada. Aidha tumetambua malengo ya utafiti na nadharia tete zilizoongoza utafiti huu. Vilevile tumeeleza sababu za kuteua mada hii kwa ajili ya utafiti huu na hatimaye kuwekea mipaka utafiti kwa kuzingatia vipengele mbalimbali. Katika Sura ya Pili tumerejelea baadhi ya maandishi tuliyopitia kuhusu mada ya Uchanganuzi wa Makosa. Aidha, tumeeleza misingi ya kinadharia iliyotuongoza katika kufanya utafiti hata kuweza kuchambua data tuliyokusanya.

# SURA YA PILI

# KIUNZI CHA NADHARIA NA MAPITIO YA MAANDISHI

## 2.0 Utangulizi

Katika sura hii, tulichunguza baadhi ya maandishi ya wataalamu na maoni yao kuhusiana na mada hii ya uchanganuzi wa makosa kwa kuzingatia malengo yetu ya utafiti. Tulifanya hivi kwa kubaini kwamba maandishi haya yangetuelekeza katika kuelewa aina mbalimbali za makosa katika lugha na namna yanajidhihirisha katika maandishi na matamshi ya wajifunzaji lugha. Vilevile tulipitia haya maandishi ili yatusaidie katika kubuni kiunzi cha nadharia iliyotuongoza katika utafiti wetu. Tulielewa kwamba kunao wataalamu wengine ambao wamefanyia utafiti mada ya uchanganuzi wa makosa katika lugha na kwa hivyo tukarejelea maandishi ya baadhi yao.

## 2.1 Maandishi Kuhusu Aina za Makosa

Katika sehemu hii tunarejelea baadhi ya maandishi yanayohusu tafiti zilizofanywa kuhusu aina mbili kuu za makosa tuliyozingatia katika utafiti wetu yaani makosa ya kitahajia na kisarufi.

### 2.1.1 Maandishi kuhusu makosa ya tahajia

Kuna maandishi mbalimbali kuhusu makosa ya kitahajia katika maandishi ya wanafunzi. Kuhusu upataji wa lugha ya kwanza, Lieberman (1970) alipendekeza kuwa baadhi ya sifa za kifonolojia huwepo katika lugha kwa sababu ya usikikaji wake. Kuwepo kwa sifa nyingine za kifonolojia hutokana na kutamkika kwake kwa urahisi. Kwa hivyo, sifa zilizo ngumu kutamkwa au kusikika kifonolojia, hudondoshwa au kupuuzwa na mwanafunzi huku zile ambazo ni rahisi zikidumishwa. Katika utafiti wetu tuligundua kwamba baadhi ya makosa ya kitahajia yalikuwa na asili yake katika matamshi mabaya ya maneno ya Kiswahili kutokana na kutokuwepo

kwa baadhi ya sauti za Kiswahili katika lugha ya kwanza ya wanafunzi. Corder (1973) anatambua fonolojia na mofolojia kuwa vitengo vya lugha vinavyoathiriwa na makosa ya wanafunzi katika maandishi. Tahajia hurejelea vipengele vya kifonolojia yaani sauti katika lugha na mofolojia ambayo huhusiana na maumbo ya maneno. Corder anaongezea kwamba makosa haya hutokana na mwingilio wa lugha ya kwanza ya wanafunzi. Kwa kuzingatia maoni haya, utafiti wetu ulichunguza makosa ya kitahajia kwa kuzingatia sifa za kifonolojia za sauti zilizohusika katika uandishi wa maneno yenye makosa kimaendelezo.

Cook (1999) wa anagawanya makosa ya kitahajia katika vitengo vinne (4) vya kuchopeka, kudondosha, kubadilisha na kuvuruga mpangilio wa herufi katika maneno. Utafiti huu pia ulitumia mgawanyo huo kwa sababu tulichambua makosa ya kitahajia katika vitengo hivi. Hata hivyo, katika mgao huu wa Cook, makosa yanayohusu kutenganisha neno na kuunganisha maneno hayakushughulikiwa na kwa hivyo katika utafiti wetu tuliyaongeza kama kitengo kingine cha aina za makosa ya kitahajia. Katika uchunguzi wa Smith na Swan (2001) kuhusu makosa ya kitahajia miongoni mwa wanafunzi wenye asili ya Kiarabu katika kusoma Kiingereza kama lugha ya pili, walifikia uamuzi kwamba wanafunzi wenye asili ya Kiarabu walifanya makosa mengi ya kitahajia kuliko wanafunzi wasio wa Kiarabu katika maandishi yao ya Kiingereza. Sababu kuu ilikuwa ni kuwepo kwa tofauti kubwa za kifonolojia kati ya Kiarabu na Kiingereza. Smith na Swan walitumia insha ili kupata data kuhusu makosa yaliyolengwa. Utafiti huu ulitusaidia kwa vile tulitumia insha kama kifaa kimojawapo cha utafiti wetu ili kuzalisha data kuhusu makosa ya kitahajia kama watafiti hawa walivyofanya.

Figueredo na Varnhagen (2004) walitumia insha mbili ili kupata data ya makosa ya kitahajia miongoni mwa wanafunzi wenye asili ya Canada ambapo walionyesha

kwamba kutambua makosa ni hatua muhimu katika kusahihisha makosa ya kitahajia. Utafiti huu uliwashirikisha wanafunzi katika kusoma insha walizopewa kwa ajili ya kutambua makosa ya kitahajia katika insha zenyewe. Utafiti huu uliyagawa makosa ya kitahajia katika vitengo vitatu vya kifonolojia, kimofolojia na kiotografia. Matokeo ya utafiti wa Figueredo na Varnhagen yalionyesha kuwepo kwa makosa mengi ya kifonolojia kuliko yale ya kimofolojia na kiotografia. Utafiti huu ulitusaidia kubuni Zoezi la Viasho kama kifaa cha kutambua makosa ya kitahajia yaliyotokana na matamshi. Vivyo hivyo, Zoezi la Jozi za Mlinganuo Finyu lilitumiwa kwa ajili ya kutambua makosa zaidi ya kitahajia yanayotokana na matamshi yasiyo sahihi kwa sababu usahihi wa matumizi ya maneno hayo ulitegemea utamkaji sahihi wa jozi za maneno yaliyotolewa kwa wanafunzi.

Tafiti nyingine kuhusu makosa ya kitahajia miongoni mwa MYW zimedhihirisha kwamba makosa ya kudondosha na kubadilisha herufi katika maneno ndiyo mengi zaidi ya aina nyingine za makosa. Al-Jabri (2006) alithibitisha jambo hili katika uchunguzi wake miongoni mwa wanafunzi wa daraja la tano nchini Oman. Uamuzi huu ulichangia utafiti wetu kwa ajili ya kuthibitisha kwamba wanafunzi wengi hufanya makosa ya kitahajia kwa kudondosha na kubadilisha herufi katika maneno. Ontieri (2010) alithibitisha hali hii katika uchanganuzi wake kuhusu makosa katika insha za wanafunzi wa shule za upili wilayani Nakuru. Mbali na kuainisha makosa katika vitengo hivyo vinne, Ontieri aliainisha makosa katika vitengo vya uunganishaji na utenganishaji wa maneno ambavyo tumevijumuisha katika utafiti wetu. Ontieri alitumia hojaji na zoezi la kuandika insha.

Watafiti wengine waliothibitisha kuwepo kwa makosa mengi ya udondoshaji na ubadilishaji wa herufi ni Al-zuoud na Kabian (2013) waliochunguza insha za wanafunzi wa chuo kikuu Jordan na Alhaisoni na wenzake (2015) waliofanya

uchunguzi miongoni mwa wanafunzi wa chuo kikuu nchini Saudi Arabia. Kijumla, tafiti hizi zilitusaidia ili kupata vigezo vya kutumia katika kuchanganua makosa ya kitahajia katika MYW na VVK.

Tofauti za kifonolojia kati ya lugha ya kwanza ya wanafunzi na lugha ya pili zimetajwa kuwa chanzo cha makosa ya kitahajia katika maandishi ya lugha ya pili miongoni mwa wanafunzi. Dixon (2010) aligundua kwamba athari za lugha ya kwanza zilidhihirika katika MYW wa lugha ya Kiingereza katika utafiti uliofanywa nchini Singapore. Opijah (2014) aligundua kwamba makosa mengi ya kitahajia yaliyofanywa na wanafunzi wenye asili ya Kinyore katika Kiswahili yalitokana na athari za Kinyore. Alitumia mjarabu wa kutafsiri, insha na mjadala wa darasani kama vifaa vya utafiti. Alhaisoni (2015) anadai kuwa makosa ya kitahajia yanatokana na udhaifu ulio katika lugha ya pili ya mwanafunzi na mwingiliano wa lugha ya kwanza. Dixon, Alhaison na Opijah walitumia insha kama kifaa cha utafiti. Tafiti hizi zinadhihirisha kwamba makosa ya kitahajia yanasababishwa na tofauti za kifonolojia baina ya lugha mbili zinazohusika yaani lugha ya kwanza ya mwanafunzi na lugha anayojifunza mwanafunzi. Maelezo haya yalikuwa muhimu kwetu kwa sababu wanafunzi tuliochunguza walitoka katika jamii mbalimbali nchini. Baadhi ya jamii hizo hazikuwa za Kibantu; lugha ambazo ni tofauti na Kiswahili ambayo ni lugha ya Kibantu. Tulijumuisha wanafunzi kutoka jamii za Luo, Teso na Kalenjin ambazo ni za Kinailoti.

Katika nyingi ya tafiti tulizorejelea hapo juu, watafiti walijikita katika kuchunguza maandishi ya wanafunzi huku wakitumia insha kama kifaa cha kupata data kuhusu makosa. Ontieri (2010) aliongezea hojaji katika uchunguzi wake miongoni mwa wanafunzi wa shule za wilaya ya Nakuru naye Opijah (2014) alitumia mjadala na mjarabu wa kutafsiri katika utafiti miongoni mwa wanafunzi wa shule za msingi

miongoni mwa Wanyore. Aidha, tafiti hizi zote zililenga makosa katika maandishi na matamshi ya wanafunzi pekee. Mbali na kutumia insha kupata data kama walivyofanya watafiti wengi, tulijumuisha zoezi la Viasho na Utungaji wa sentensi kwa kutumia Jozi za Mlinganuo Finyu ili kuweka wazi makosa ya kitahajia yaliyotokana na matamshi. Hali kadhalika, hakuna mtafiti aliyechunguza makosa katika VVK kama njia mojawapo ya kutathmini asili za makosa katika MYW wanaosoma Kiswahili kama lugha ya pili. Ujumuishaji wa makosa katika VVK umedhamiria kuziba mwanya ambao umeachwa na watafiti hawa katika kutambua vyanzo vya makosa yanayofanywa na wanafunzi.

### 2.1.2 Maandishi kuhusu makosa ya kisarufi

Tafiti nyingi kuhusu uchanganuzi makosa katika lugha zinalenga makosa ya kisarufi. Pengine sababu kubwa ni kwamba sarufi husheheni vipengele vingi zaidi ya tahajia. Katika sehemu hii tumeangazia baadhi ya maandishi yaliyopo kuhusu makosa ya kisarufi ambapo tumejumuisha kipengele cha msamiati kwa sababu msamiati huathari sarufi.

Simotwo (1993) alitafiti kuhusu uchanganuzi wa makosa ya maana na kimsamiati kama yalivyofanywa na wazungumzaji asilia wa Kinandi katika Kiingereza. Alikusanya data kwa wanafunzi wa shule za msingi kupitia kuandika insha, kutafsiri mitihani, kusimulia hadithi na kuzungumza. Aligundua kwamba uhamishaji wa maana ya msamiati kutoka katika lugha ya Kinandi hadi Kiingereza ndiyo sababu kuu ya makosa ya maana ya msamiati miongoni mwa wanafunzi wanaojifunza lugha ya pili. Katika utafiti wetu tulitumia insha ili kupata data kuhusu makosa ya kisarufi na kimsamiati kama Simotwo alivyofanya. Utafiti wetu ulihusu wanafunzi kutoka katika jamiimseto na miongoni mwao kulikuwa na wenye asili ya Kinandi ambayo ni lahaja ya Kikalenjin. Utafiti mwingine kuhusu makosa ya kisarufi miongoni mwa wanafunzi

kutoka katika jamii ya Kipsigis ulifanywa na Chepkwony (2012). Tafiti hizi zilitufaa katika kuchambua baadhi ya makosa yaliyo na asili yake katika lugha ya kwanza kama yalivyotokea katika maandishi ya wanafunzi wenye asili ya Kalenjin kwa kuelewa baadhi ya miundo ya tungo katika lahaja za Kikalenjin.

Njeng'ere (1996) alishughulikia uchanganuzi wa makosa ya Kikundi Tenzi katika Kiingereza miongoni mwa wanafunzi wa Kikikuyu katika kidato cha nne. Alitumia mitihani, zoezi la kutafsiri na insha kama vifaa vya utafiti. Aligundua kwamba makosa mengi ya Kikundi Tenzi katika MYW yanatokana na lugha ya kwanza ya wanafunzi yaani Kikikuyu. Miongoni mwa watafitiwa wetu kulikuwa na wanafunzi wenye asili ya Kikikuyu na utafiti wa Njeng'ere ulitusaidia kutambua baadhi ya vipengele vya sarufi ya Kikikuyu. Makosa ya kisarufi katika Kiswahili yaliyotokana na athari za lugha ya Kikikuyu yalitambulika kwa urahisi.

Kulingana na Richards na wenzake (2002), makosa katika lugha yanaweza kugawanywa katika makundi mawili makuu yaani yale yanayotokana na mwingiliano wa lugha ya kwanza kwa lugha ya pili na yale ya mwingiliano wa ndani kwa ndani wa lugha ya kwanza yenyewe. Makosa katika kundi la kwanza yanadhihirisha kwamba lugha ya kwanza ya mwanafunzi inasababisha makosa yanayotokea katika ujifunzaji wa lugha ya pili ambapo mwanafunzi wa lugha anatumia kanuni za lugha yake ya kwanza katika lugha ya pili. Hii ni sawasawa na kuhamisha kanuni za lugha anayoijua na kuziweka katika lugha anayojifunza.

Makosa katika kundi la pili yanatokana na mwanafunzi wa lugha ya pili kutekeleza vibaya kanuni za lugha anayojifunza. Makosa ya kundi la pili yanaweza kujidhihirisha kwa njia zifuatazo: kwanza, ujumlishaji wa kanuni za kisarufi, pili ni usahilishaji ambapo mwanafunzi hubuni mitindo rahisi iliyo katika lugha anayojifunza, tatu

uhamishaji wa kanuni kutokana na mambo anayosikia kutoka kwa wasemaji wa lugha hiyo, nne kukwepa kutekeleza kanuni anazoona kuwa ni ngumu kwake na tano ni uzalishaji uliokithiri mipaka ambao unajidhihirisha kwa kujirudiarudia katika matumizi yake ya lugha. Hali hizi zote zinaweza kujidhihirisha kwa namna mbalimbali katika uchanganuzi wa makosa. Hizi njia tofauti za kujidhihirisha kwa makosa zilitufaa katika uchanganuzi wetu kwa sababu ya kujaribu kuelezea asili za makosa katika maandishi. Baadhi ya makosa yalitokana na kujumlisha, kusahilisha na kuhamisha kanuni za kisarufi. Aidha, kulikuwa na visa kadhaa vya kujirudia katika tungo za wanafunzi katika utafiti wetu na hii ilikuwa ishara ya kutatiza sarufi ya tungo husika.

Msanjila (2005) aligawanya makosa katika MYW kwenye insha za wanafunzi wa shule za upili nchini Tanzania katika makundi sita: matumizi ya herufi kubwa, uakifishaji, tahajia, utata, mparaganyo wa maneno na sarufi. Alihitimisha kwamba makosa yaliyotokea katika MYW yalidhihirisha kwamba kulikuwa na mbinu mbovu za kufunzia wanafunzi shuleni. Utafiti wa Msanjila ulitufaa kwa namna mbili. Kwanza, tulitumia vipengele viwili vya kuchambua makosa ya kisarufi yaani utata na mparaganyo wa maneno katika tungo. Pili, kutokana na kuonyesha kwamba makosa yanasababishwa na mbinu mbovu za kufunzia wanafunzi, tuliteua baadhi ya VVK ili kutathmini makosa yaliyomo kwa kuwa vitabu ni vielelezo vya kufunzia wanafunzi. Tulionyesha kwamba mbinu za kufunzia haziwezi kukamilika bila kuhusisha VVK ambavyo ni vifaa muhimu vya kufunzia shuleni.

Ontieri (2010) alitumia vipengele vya upatanishi wa kisarufi, nomino, vitenzi, vivumishi, vielezi, viambishi, herufi, silabi, maneno, methali, misemo na utohozi kuchanganua makosa kwenye insha za wanafunzi wa shule za upili wilayani Nakuru. Aligundua kwamba makosa mengi ya kisarufi yalihusu ukosefu wa upatanishi

yakiwakilisha zaidi ya 50% ya makosa yote ya kisarufi. Aidha, makosa ya kudondosha neno katika sentensi yalifuatia kwa kuchukua nafasi ya pili kwa 8.1%. Katika orodha hiyo, idadi ndogo sana ya makosa iliyowakilishwa na 1.1%, ilihusu matumizi potofu ya viunganishi. Katika utafiti wetu tulizingatia vingi kati ya vipengele vya Ontieri katika utafiti wetu. Katika MYW, idadi kubwa ya makosa ilihusiana na ukosefu wa upatanisho (Ontieri alitumia istilahi ya 'upatanishi') Hata hivyo, tofauti na Ontieri aliyechambua makosa ya upatanisho katika ujumla wake, utafiti wetu ulizingatia makosa ya upatanisho kwa kuzingatia aina za maneno. Kwa mfano, makosa ya upatanisho yalichambuliwa katika misingi ya vitenzi, vivumishi na virejeshi.

Uchunguzi mwingine kuhusu makosa ya kisarufi ulifanywa na Kisakwah (2014), kwa kuzingatia muundo wa sentensi za Kiswahili sanifu na Kisuba katika Kisiwa cha Mfangano. Katika uchunguzi huu, alifikia uamuzi kwamba kati ya makosa yaliyojitokeza katika vipashio vya lugha, asilimia 50 ilihusishwa na athari za lugha ya kwanza ya wanafunzi yaani Kisuba. Uchunguzi huu unatilia mkazo dhana kwamba lugha ya kwanza ya wanafunzi ina mchango mkubwa katika idadi ya makosa yanayotokea katika lugha yao ya pili. Kwa mujibu wa uchunguzi wa Kisakwah, asilimia 50 ya makosa hutokana na vianzo vingine ambapo kwa mujibu wa utafiti wetu, vitabu vya kiada ambavyo tulichunguza, vinachangia kuwepo kwa makosa katika maandishi ya wanafunzi. Tunaweza kudai kwamba ingawa lugha ya kwanza inachangia makosa katika lugha ya pili, sio makosa yote yanasababishwa na lugha ya kwanza. Kuna visababishi vingine na miongoni mwao ni vitabu vinavyosomwa na wanafunzi shuleni.

Utafiti wa Opijah (2014) ulihusu uchanganuzi wa makosa ya kiisimu katika matumizi ya Kiswahili miongoni mwa Wanyore. Utafiti wa Opijah ulizingatia kundi la wanafunzi wa darasa la saba wanaozungumza Kiswahili kama lugha ya pili na ambao Kinyore ni lugha yao ya kwanza. Alijikita katika kutafuta na kutathmini chemchemi ya matatizo yanayotokea katika matamshi ya wanafunzi, namna yanavyotokea, kuyafafanua, kuthibitisha uzito wake na hatimaye kuyasahihisha. Aliyarejelea kijumla kama makosa ya kimawasiliano. Opijah aligundua kwamba makosa ya wanafunzi yalitokana na Lugha ya Kwanza (Kinyore) na pia Kiswahili ambayo ni Lugha ya Pili. Athari hii ilijidhihirisha katika vipengele vya sarufi, msamiati, matumizi ya lugha na hijai. Kwa ajili ya utafiti wa baadaye kuhusu mada hii, Opijah anapendekeza kwamba utafiti ufanywe kwa kiwango cha kitaifa madhali utafiti wake ulizingatia sehemu ndogo ya jamii moja. Ilmuradi katika utafiti wetu tulihusisha jamiimseto, (tulirejelea wanafunzi kutoka katika jamii tano (5) za Luhya, Kikuyu, Kalenjin, Teso na Luo), tunaweza kudai kwamba tumeshirikisha idadi kubwa ya jamii katika utafiti wetu na kwa njia hii tumejaribu kutekeleza baadhi ya mapendekezo ya Opijah.

Lukamika (2015) alifanya uchunguzi kuhusu matumizi ya ngeli katika Chuo Kikuu cha Maseno miongoni mwa wanafunzi wa Kiswahili wa Shahada ya Kwanza. Alijikita katika kipengele cha ngeli kwa sababu ngeli ndio msingi wa sarufi ya Kiswahili. Matokeo ya uchunguzi wake yalionyesha kwamba umaizi wa wanafunzi ulikuwa duni hususan katika ngeli za PA-KU-MU na LI-YA. Utambuzi huu ulitusaidia katika kuchambua makosa ambayo yalihusiana na upatanisho. Miongoni mwa ngeli zilizowatatiza wanafunzi kupatanisha katika utafiti wetu ni ya LI-YA sawasawa na Lukamika alivyodhihirisha.

Kwa jumla jinsi ilivyodhihirika katika tafiti kuhusu makosa ya kitahajia, kadiri ya ufahamu wetu, hapana mtafiti ambaye amechunguza makosa katika VVK kama tulivyofanya. Hii ndiyo tofauti kubwa kati ya utafiti wetu na tafiti nyingine zilizowahi kufanyika katika uwanja wa uchanganuzi wa makosa. Aidha, mpaka sasa takriban kila mtafiti ametumia insha kama kifaa cha kuzalisha data kwa ajili ya uchanganuzi wa makosa. Hii inaashiria umuhimu wa insha kama kifaa cha utafiti kuhusu uchanganuzi wa makosa katika lugha. Kwa kuelewa ukweli huu, utafiti wetu ulitumia kifaa hiki. Hata hivyo, kwa ajili ya kupanua uwanja ili makosa ya wanafunzi yadhihirike zaidi na kutambuliwa kwa udhaifu wao katika lugha, tulitumia mazoezi ya Viasho na Jozi za Mlinganuo Finyu ambayo yalitekeleza wajibu mkubwa katika kutambua makosa ya kitahajia na kimsamiati. Kwa kuzingatia hali ya watafitiwa, mbali na Ontieri na Lukamika, tafiti nyingine zote zililenga wanafunzi waliotoka katika jamii moja. Upekee wa utafiti wetu ulikuwa katika uamuzi wa kurejelea makosa katika vitabu vya kiada ambapo tuliteua vitabu vitatu vya kiada kwa ajili ya kutimiza lengo hili.

## 2.2 Tahakiki kuhusu Asili ya Makosa na Jinsi ya Kuyakabili

Katika sehemu hii tunadahili maandishi kuhusu asili ya aina mbalimbali za makosa yanayofanywa na wanafunzi katika maandishi yao na njia za kukabiliana na makosa hayo.

Richards (1974) aligundua kwamba makosa katika lugha ya pili hutokana na mwingiliano wa ndani kwa ndani wa lugha kama vile ujumlishaji mwingi, upuuzaji wa vighairi lugha, utekelezaji nusu wa kanuni, na makosa ya kisemantiki. Richards na Gloria (1974), waliorodhesha mambo saba ambayo yanaweza kuingilia na kuathiri mifumo ya mwanafunzi wa lugha ya pili. Mambo haya ni: uhamishaji lugha, mwingilianolugha wa ndani kwa ndani, hali ya kiisimujamii, mtindo, umri, mfuatano wa mifumo unaokaribiana na tabaka la ugumu wa kimataifa. Katika utafiti wetu

tuligundua kwamba baadhi ya makosa katika maandishi ya wanafunzi yalitokana na uhamishaji wa kanuni za lugha ya kwanza na kuzilazimisha katika Kiswahili. Pia tuligundua kwamba baadhi ya makosa yalisababishwa na hali ya kiisimujamii katika jamiimseto ambapo matumizi potofu ya lugha katika jamii yalichangia kuwepo kwa makosa katika maandishi ya wanafunzi pamoja na kuathiriana katika jamiimseto.

Taylor (1975) anapendekeza kuwa watu wanaoanza kujifunza lugha ngeni hutegemea lugha ya kwanza kubuni nadharia tete kuhusu sarufi ya lugha ngeni ilhali wale waliostawi zaidi huweza kufanya ujumlishi kuhusu lugha ngeni. Kwa mujibu huu, ujumlishaji ni sababu nyingineyo ya kufanya makosa katika lugha ya pili; hii ikiwa ni mojawapo ya sababu zilizo ndani ya lugha anayojifunza mtu.

Kulingana na Brown (1993), athari za kimatamshi miongoni mwa wanafunzi wanaojifunza lugha ya pili hutokana na sababu kwamba wanafunzi hao hawajui mfumo wa kanuni za lugha hiyo. Athari hizi ndizo zinazojumuisha kile kinachorejelewa na wataalamu wa lugha kama makosa katika lugha. Wanaisimu wengi wanaelekea kukubaliana kwamba lugha ya kwanza ya mjifunzaji wa lugha ya pili ina athari kubwa kwa lugha ya pili kutokana na tofauti za kifonolojia baina ya lugha hizo. Richards na wenzake (2002) wanakubaliana na Brown katika jambo hili ila wanaongezea kwamba makosa mengine yanatokana na lugha anayojifunza. Msanjila (2005) anapodai kwamba wanafunzi huandika namna wanavyotamka, anaashiria kwamba makosa katika lugha yanasababishwa na matamshi ya lugha ya kwanza ya msemaji.

Mapendekezo mbalimbali yametolewa na watafiti kuwa suluhisho kwa makosa yanayotokea katika ujifunzaji lugha**.** Ontieri (2010) anapendekeza kwamba mwanafunzi anaweza kukabiliana na makosa ya hijai kwa kuyaorodhesha maneno

yanayomkanganya anapoandika insha. Ontieri anapendekeza kwamba mwanafunzi afikirie muundo wa neno analotaka kuandika kama mbinu mojawapo ya kukabiliana na makosa ya kitahajia. Ili kuepuka kufanya makosa ya kisarufi, anapendekeza mikakati mbalimbali itumiwe na mwanafunzi kama vile kufanya mazoezi mengi katika lugha. Aghalabu, watumia lugha huandika jinsi wanavyotamka yaani, matamshi huathiri maandishi na kwa hivyo ikiwa watadumisha matamshi bora basi hawatakuwa na makosa katika maandishi yao.

Kulingana na Khansir (2012), kuna makosa mengi yanayofanywa na wajifunzaji wa lugha ya pili yasiyohusiana na lugha ya kwanza. Hii ni kwa sababu wanafunzi tofauti waliomiliki lugha moja ya kwanza, walipatikana kufanya makosa yasiyofanana. Katika utafiti wa Khansir ulionyesha kwamba wanafunzi walifanya makosa mengi sana ya hijai, kisha yale ya kisarufi na hatimaye makosa ya kimsamiati yalikuwa machache zaidi. Jambo linalolengwa hapa ni kwamba makosa yanayofanyika katika lugha ya pili hutegemea vipashio vinavyoathirika na makosa yenyewe ambapo baadhi ya vipashio huwa na makosa mengi zaidi ya vingine.

Kitsao (2015) anaafikiana na ukweli huu anaposema kuwa msingi bora wa lugha ya Kiswahili ni mwanafunzi kujua silabi za Kiswahili kwa kuzingatia stadi za lugha kama kusikiliza na kuzungumza. Anapendekeza kwamba walimu wazingatie stadi hizi katika ufundishaji pamoja na zile za kusoma na kuandika. Kwa mujibu wa Kitsao basi, makosa katika lugha yanaweza kukabiliwa kwa kushirikisha stadi zote za kufundisha lugha. Anaelekea kushabikia muelekeo mseto katika mchakato wa kufundisha ambapo stadi zote za lugha hushirikishwa katika mafunzo.

Ni bora pia kukumbuka kwamba wanafunzi katika shule wanastahili kustawisha matamshi bora kwa sababu ndicho kidato cha chini katika ngazi ya sarufi kabla ya

kufikia mofolojia na sintaksia ambavyo ni vidato vya juu (Obuchi & Mukhwana, 2010). Hoja hii inadhihirisha kuwa madhali wanafunzi hutumia mikakati tofauti kujifunza lugha katika viwango tofauti, ufunzaji wa lugha unastahiksi kutilia maanani stadi lugha yaani, kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika, ambavyo ni sharti vifunzwe kwa utaratibu wa kuanzia vile vya kimsingi yaani kusikiliza na kuongea kabla ya kufikia kusoma na kuandika ambavyo ni vya juu. Kwa njia hii wanafunzi watakabiliana na makosa yanayoweza kutokea katika kujifunza lugha ya pili.

Mpaka sasa, kadiri ya uelewa wetu, hapajakuwa na maandishi kuhusu sababu za VVK kuwa na makosa ya lugha. Hata hivyo, kwa sababu uandishi wa vitabu ni shughuli inayohusisha wataalamu, tunaweza kuhusisha tatizo hili na wataalamu hawa ambao hujumuisha waandishi, wahariri, wapiga chapa na wakuu wa elimu ambao ndio wanaoidhinisha VVK. Kwa sababu hii basi, suluhisho kwa makosa katika VVK ipo mikononi mwa wataalamu tuliowataja hapo juu.

## 2.3 Misingi ya Kinadharia

Ili kushughulikia suala la utafiti huu, tulitumia Nadharia ya Uchanganuzi Makosa ambayo ilifasiliwa na Corder (1967). Nadharia hii ni muhimu katika utafiti wetu kutokana na mihimili yake mikuu ambayo inachukuana vizuri na data inayochambuliwa katika tasnifu hii.

### 2.3.1 Nadharia ya Uchanganuzi Makosa

Utafiti huu ulifanywa chini ya misingi ya Nadharia ya Uchanganuzi Makosa ambayo ilifasiliwa na Corder (1967). Nadharia hii ilistawi kutoka Nadharia ya Uchanganuzi Linganuzi iliyobuniwa katika miaka 1950 na mwanzomwanzo wa 1960. Nadharia hizi ni matawi mawili ya Isimu Tekelezi ambayo kijumla hujishughulisha na kutumia mambo tunayojua kuhusu lugha fulani, jinsi lugha hiyo inavyotumiwa na namna

inavyofaa kutumiwa kwa ajili ya kuafikia malengo maalumu au kusuluhisha matatizo yaliyo katika ulimwengu halisi. Katika miaka ya 1960 na ya mapema 1970, wanaisimu walishikilia kwamba makosa katika lugha hayakutokea kiholela bali yalifuata mfumo maalumu na kwa sababu hiyo ikadhaniwa kwamba ujifunzaji wa lugha ulizingatia utaratibu fulani.

Richards (1974) ni miongoni mwa wanaisimu walioshabikia maoni kwamba ujifunzajilugha huzingatia utaratibu maalumu. Anaorodhesha aina tano za makosa kwa kuzingatia jinsi yanavyodhihirishwa na wajifunzajilugha. Aina hizi ni ujumlishaji mwingi wa kanuni za lugha anayojifunza, kutofahamu kanuni zinazohusiana na vighairilugha na utekelezaji nusu wa kanuni kutokana na ukosefu wa ujuzi kamili wa miundo ya lugha husika. Aina ya nne ya makosa ni kuendeleza dhana potofu kuhusu lugha. Aina ya mwisho ni udhaifu wa kukumbuka aliyojifunza. Baadhi ya mambo yaliyoorodheshwa hapa yalidhihirika katika MYW na VVK.

Richards, makosa haya yanaweza kutengwa katika makundi makuu mawili yaani makosa ya kiutendaji na ya kiumilisi. Makosa ya kiutendaji hutokea kwa nadra na kiholela bila kufuata utaratibu maalum na yanatokana na uchofu na usahaulifu. Makosa ya kiumilisi hutokea kwa kufuata mfumo maalum na yanawakilisha hatua ya mpito katika kubwia sarufi ya lugha au ishara ya mjifunzaji wa lugha kufikia mwisho wa ujuzi wake katika lugha anayojifunza.

Katika kipindi hiki, shughuli ya uchanganuzi wa makosa ilifafanuliwa kuwa ni kuchunguza tofauti ya matumizi ya lugha kati ya watu wanaojifunza lugha na jinsi wasemaji asilia wanavyoitumia. Tofauti ya matumizi ya lugha ilichukuliwa kuwa ndiyo makosa katika lugha. Kijumla nadharia za uchanganuzi makosa zinaratibu malengo manne ya kuchunguza makosa katika lugha ambazo ni: kutambua makosa,

kuyaeleza, kuyachambua na baadaye kuyatathmini. Tulizingatia mapendekezo haya katika kubuni malengo ya utafiti wetu.

### 2.3.2 Mihimili ya Nadharia ya Uchanganuzi Makosa

Wanaisimu kama vile Corder, Richards na Khansir wanakubaliana kwamba makosa katika ujifunzaji wa lugha ya pili hutokea kwa kufuata mfumo maalum na kwa hivyo, mfumo huo unaweza kuchunguzwa. Matokeo ya uchunguzi huo yanaweza kuwasaidia wanaisimu katika kubuni mbinu za kukabiliana na makosa hayo. Nadharia ya uchanganuzi wa makosa huanzia kujishughulisha na kutambua makosa yanayotokea katika ujifunzaji wa lugha ya pili na kuyajadili kwa kina. Katika kufanya hivyo, watafiti hupata takwimu zinazoonyesha makosa halisi yanayofanywa na mjifunzaji lugha na kumsaidia mwanaisimu kuelewa utaratibu wa kisaikolojia wa ujifunzaji wa lugha ya pili. Mathalani, mwalimu anaweza kusahihisha kazi zilizoandikwa na wanafunzi kama vile insha na kuorodhesha makosa ambayo yanafanana kisha akayarekebisha.

Nadharia ya Uchanganuzi Makosa huainisha makosa yanayotokea ndani ya lugha anayojifunza mwanafunzi kulingana na jinsi yanavyojidhihirisha. Nadharia hii huzingatia hatua tano katika mchakato wa kuchanganua makosa. Hizi ndizo hatua zilizoongoza utafiti wetu.

Katika hatua ya kwanza kuna uteuzi wa matini katika lugha inayolengwa. Kunazo aina tatu za uteuzi. Aina ya kwanza inahusu uteuzi wa matini yenye mifano mingi ya matumizi ya lugha ambayo humwezesha mtafiti kupata idadi kubwa ya makosa na inayowakilisha jamii kubwa inayotafitiwa. Uteuzi wa jamii kubwa humwezesha mtafiti kupata data ya kutosha ikiwa na uwakilishi wa ain azote za makosa. Udhaifu

wa uteuzi wa aina hii ni kwamba aghalabu wingi wa habari zilizokusanywa kuhusu lugha huleta bughudha kwa mtafiti kwa kushindwa kuzichuja habari alizopata.

Aina ya pili inahusu uteuzi halisi ambapo mtafiti huchagua idadi halisi na namna moja ya kupata habari kuhusu lugha. Kwa mfano, anaweza kutumia insha kama kifaa cha kukusanyia data kuhusu lugha inayofanyiwa utafiti. Manufaa ya uteuzi halisi ni kwamba humwezesha mtafiti kupata data kwa urahisi. Kwa sababu ya data kuwa halisi, shughuli ya uchanganuzi huwa rahisi. Hata hivyo, kuna uwezekano wa kukosa kupata idadi ya kutosha ya makosa yanayolengwa na utafiti kwa sababu kutumia aina moja ya kifaa cha kukusanyia data. Aina ya tatu ni uteuzi tukizi ambapo mtafiti huteua kisa kimoja na kukitumia katika kupata habari kuhusu matumizi ya lugha. Tulizingatia mtindo mahuluti katika utafiti wetu kwa kutumia idadi halisi pamoja na uteuzi tukizi. Idadi halisi ilitufaa katika kupata habari kuhusu matumizi ya lugha miongoni mwa wanafunzi ambapo tulitumia mazoezi matatu ya Viasho, Jozi za Mlinganuo Finyu na Insha. Uteuzi tukizi ulitumiwa katika kuteua vitabu vitatu vya kiada na kuchunguza makosa yaliyokuwa ndani yake.

Hatua ya pili inahusu utambuzi. Katika hatua hii mtafiti huweka wazi mambo ya kuzingatiwa katika utafiti. Kwanza, mtafiti hutambua lugha ambayo itatumiwa kama kigezo cha kuamua ni wapi alipokosea mtumiaji wa lugha. Haiwezekani kuamua kwamba kuna makosa katika lugha pasipo kuwa kigezo cha kupimia ukubalifu yaani lugha sanifu. Aidha ni lazima kutambua dhana ya makosa kwa kutofautisha baina ya makosa yanayoashiria kutojua kwa upande wa mtumiaji husika na tukio linaloashiria kuteleza katika matumizi ya lugha. Katika utafiti huu, lugha lengwa ya kupimia umaizi wa watumiaji tuliolenga ni Kiswahili Sanifu. Kwa mujibu wa utafiti huu, dhana ya 'makosa' inarejelea matumizi yoyote yanayokiuka kanuni za sarufi ya

Kiswahili Sanifu. Hatukutofautisha baina ya makosa ya kutojua na matumizi ya lugha yanayodhihirisha upungufu wa kutimiza lengo linalotarajiwa kwa sababu matukio yote mawili yanatatiza mawasiliano.

Katika hatua ya utambuzi, mtafiti anastahiki kufasiri habari anazopata kuhusu matumizi ya lugha ili kuonyesha aina za makosa katika taarifa hizo. Ili kufanikiwa katika shughuli hii ni sharti aelewe kwamba kuna makosa yanayodhihirika moja kwa moja mengine ambayo yanatambuliwa kwa kuchunguza undani wa matumizi ya lugha husika. Kulingana na uchunguzi wetu, makosa yaliyoonyekana kwa mtazamo wa nje ni yale ya kitahajia ilhali mengi ya makosa ya kisarufi yalitambuliwa kwa kuchunguza mambo ya ndani ya lugha kama sintaksia na semantiki. Katika kutambua makosa tulizingatia kigezo cha kupotoka kwa tungo.

Hatua ya tatu katika uchanganuzi wa makosa ni kuyaeleza makosa. Mtafiti huzingatia hulinganisha matumizi ya lugha ambayo yana upungufu na usahihi uliopo ama ulioandikwa katika vitabu. Aidha, katika hatua hii makosa huratibiwa katika kategoria mbalimbali. Mgao huu wa kitegoria huyaweka wazi makosa yenyewe. Miongoni mwa kategoria hizi ni kudondosha, kuchopeka, kufasiri vibaya na kuvuruga mpangilio unaofaa kuzingatiwa. Tulizingatia kategoria hizi katika kueleza makosa tuliyotambua katika MYW na VVK. Kategoria hizi zilitusaidia katika kubuni kategoria nyingine ndogo kama vile kutenganisha neno na kuunganisha maneno na kuzitumia katika kuchambua makosa katika utafiti wetu.

Hatua ya nne ni uchambuzi wa makosa. Katika hatua hii makosa yanafafanuliwa ili kueleza chanzo chake kwa kuzingatia lugha ya kwanza ya wanafunzi ili kuonyesha vipengele vya lugha ya kwanza vinavyoingilia ujifunzaji wa lugha ya pili. Mambo mengine yanayochambuliwa ni mbinu za kujifunzia lugha zinazofanana katika lugha

ya kwanza na ya pili na makosa yanayotoka kwingineko mbali na lugha ya kwanza na pili. Dhana kuu katika hatua hii ni kuonyesha kwamba makosa yana asili mbalimbali wala sio katika lugha mbili zinazohusika pekee. Mawazo haya yalituongoza katika kuchambua vyanzo mbalimbali vya makosa katika MYW na VVK.

Hatua ya tano inahusu tathmini ya makosa ambapo mtafiti anakadiria idadi ya kila aina ya makosa ili kuonyesha viwango vya kila aina ya makosa. Hii inamsaidia mtafiti kujua aina ya makosa yanayotokea kwa upana na yale ambayo yanatokea katika vipashio vidogo vya lugha. Hatua hii ni dhihirisho kwamba aina mbalimbali za makosa hutofautiana katika viwango vyake ambapo baadhi ya makosa hutokea mara nyingi zaidi ya mengine. Tathmini humsaidia mtafiti kufanya uamuzi kuhusu makosa yanayofaa kukabiliwa ili kumuimarisha mjifunzaji. Aidha, hatua hii hutambua ukweli kwamba haiwezekani kukabili makosa yote yanayotokea katika lugha. Hatua hii ilikuwa muhimu katika utafiti wetu kwani ilitusaidia kukadiria idadi ya makosa kwa kulinganisha VVK ambavyo tulichunguza. Tathmini ilitufaa ili kuripoti kwa walimu baadhi ya mambo yaliyowatatiza wanafunzi ili yazingatiwe na walimu wanapowafunza wanafunzi. Tulitambua viwango vya makosa katika kila kitabu kwa kuviwakilisha kwa njia ya asilimia kulingana na idadi ya kurasa zilizo katika kila kitabu. Kwa sababu hii, ilikuwa rahisi kutambua kitabu kilichosheheni makosa zaidi ya vingine. Taarifa hizi ni muhimu kwa wahusika katika idara ya elimu ili wafahamu kwamba wingi wa makosa katika VVK ni kumbusho kwamba nakala za vitabu hivyo hazifai kutumiwa shuleni kabla ya kufanyiwa marekebisho.

## 2.4 Hitimisho

Kwa jumla katika sura hii tulijadili vyanzo vya makosa yanayofanywa na wanafunzi wanaojifunza lugha ya pili ambavyo vilitokea kuwa ndani na nje ya lugha anayojifunza mwanafunzi na kurejelea mapendekezo ya baadhi ya waandishi kuhusu jinsi ya kukabiliana na makosa hayo. Asili ya makosa yenyewe ni athari za lugha ya kwanza, mwingiliano wa ndani kwa ndani wa lugha ya pili na kutojua kanuni za lugha ya pili kupitia matamshi mabaya. Aidha, tumeonyesha namna mbalimbali za kukabiliana na makosa katika lugha. Kijumla, mazoezi ya kutosha katika stadi zote za lugha yatafaa katika kukabiliana na makosa katika MYW. Tumerejelea maandishi mbalimbali kuhusu mada yetu ambayo yametuwezesha kutambua msingi wa kinadharia ambao utafiti wetu uliegemea. Tumeonyesha jinsi nadharia yetu ilivyotufaa katika kutekeleza utafiti wetu.

Katika Sura ya Tatu tumefafanua mbinu tulizotumia katika utafiti wetu ambapo tumeonyesha vifaa tulivyotumia katika kukusanya data yetu, kuisafisha na kisha kuichambua ili kutimiza malengo ya utafiti wetu.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.0 Utangulizi

Katika sura hii, tumeeleza mbinu tulizotumia katika utafiti wetu kwa kufafanua jinsi tulivyofanya uteuzi wa eneo na kundi la utafiti na kuonyesha idadi halisi ya wasailiwa waliohusishwa katika utafiti huu. Vifaa vitatu tulivyotumia katika kukusanya data kutoka kwa wanafunzi na sababu za kutumia kila kifaa ni mambo mengine yaliyoelezwa katika sura hii. Pia tumetambulisha VVK vitatu tulivyoteua ili kupata data ya makosa kisha kueleza njia zilizotumiwa kukusanya, kuchambua na kuwasilisha data kwa mujibu wa malengo yetu ya utafiti.

## 3.1 Muundo wa Utafiti

Utafiti huu ulifanywa kwa kukusanya data kutoka kwa wanafunzi wa shule za upili na VVK. Kwa umahsusi, utafiti huu ulifanywa kwa ziara ya nyanjani kwa ajili ya kukusanya data kuhusu makosa katika maandishi ya wanafunzi. Kwa ajili ya kukusanya data kuhusu makosa katika VVK, mtafiti alizuru maktaba shuleni ili kupata nakala za vitabu vinavyotumiwa na wanafunzi katika mafunzo shuleni.

## 3.2 Eneo la Utafiti

Utafiti shuleni ulifanywa miongoni mwa wanafunzi wa kidato cha pili katika shule za upili za kutwa katika Kaunti Ndogo ya Likuyani katika Kaunti ya Kakamega. Eneo hili liko katika uliokuwa Mkoa wa Magharibi kabla ya kuanzishwa kwa serikali za ugatuzi. Eneo hili linakaliwa na jamiimseto ingawa jamii ya Kiluhya ndiyo ina idadi kubwa ya watu. Wakati wa kufanywa kwa utafiti huu, kulikuwa na kata tano (5) katika eneo la utafiti. Kata hizi ni Likuyani, Sango, Kongoni, Sinoko na Nzoia. Miongoni mwa kata hizi, nne (4) zilikuwa na kati ya shule tano (5) na sita (6) za upili.

Kata moja (1) ilikuwa na shule tatu (3). Tulitumia usampuli nasibu wa kimaksudi katika kufanya uteuzi. Usampuli wa kimaksudi ulitumika katika kuteua shule kutoka kila kata. Tuliteua shule mbilimbili kutoka kila kata yenye shule tano au sita, na shule moja kutoka katika kata iliyokuwa na shule tatu. Lengo la kufanya uteuzi wa aina hii lilikuwa ni kushirikisha wanafunzi kutoka maeneo yote ya kijiografia ya kaunti hii ndogo na kupata data yenye uwakilishi tosha wa wanafunzi kutoka jamii tofautitofauti. Shule tulizoteua ni: St. Michael's Kilimani na St. Joseph's Lumino (Likuyani), St. Joseph's Kogo (Sango), Friends Secondary School, Kongoni na St. Augustine's Soysambu (Kongoni), Friends Secondary School, Mbururu na Friends Secondary School, Binyenya (Nzoia) na St. Peter's Machine na St. John's Mutoni (Sinoko). Uteuzi huu uliwakilisha zaidi ya 23% ya shule 39 za upili katika eneo la utafiti. Aidha, hakukuwa na rasilmali ya kutosha ya kutuwezesha kuteua shule zaidi.

Mtindo huu wa usampuli maksudi pia ulitumiwa katika kuteua jamii tano (5). Wanafunzi walioteuliwa walitoka katika jamii za Luhya, Kikuyu, Luo, Teso na Kalenjin. Katika kila shule tuliteua wanafunzi 12 kwa kutumia uteuzi wa kimaksudi. Kwa kuzingatia idadi ya wakazi wa jamii mbalimbali za eneo hili, katika kila shule tuliteua idadi ifuatayo ya wanafunzi: Luhya sita (6), Kikuyu wawili (2), Kalenjin wawili (2), Teso mmoja (1) na Luo mmoja (1). Tulichagua jamii hizi kwa sababu ndizo zilikuwa na idadi kubwa zaidi ya watu katika eneo hili la utafiti lenye jamiimseto. Katika kila shule wanafunzi walitengwa katika makundi haya matano kwa mujibu wa jamii zao kabla ya kuhusishwa katika kupiga kura. Usampuli nasibu ulitumika katika kuteua wanafunzi watafitiwa kutoka kundi la wanafunzi wa jamii moja katika kila shule ambapo walipiga kura kwa kuchagua kadi zilizokuwa na maandishi ya NDIO au LA. Ni wale waliochagua kadi za NDIO walioteuliwa kwa ajili ya utafiti huu. Kijumla, jamii ziliwakilishwa ifuatavyo: Luhya 54, Kikuyu 18,

Kalenjin 18, Luo 9 na Teso 9. Kwa jumla tuliwashirikisha wanafunzi 108 ambao walifanya mazoezi matatu ya kuandika.

Kwa ajili ya kukusanya data kuhusu makosa katika VVK, tuliteua kimaksudi vitabu vitatu vya mafunzo ya Kiswahili katika shule za upili vya kidato cha kwanza na cha pili. Kila kimoja kati ya vitabu hivi kilikuwa na waandishi na kampuni ya uchapishaji tofauti. Kati ya vitabu tulivyoteua, kimoja kilikuwa cha wanafunzi wa kidato cha kwanza na kilikuwa kimeidhinishwa na Wizara ya Elimu. Tulikiteua kimaksudi kitabu hiki kwa sababu wanafunzi wa kidato cha pili walikuwa wametagusana nacho katika mafunzo yao walipokuwa katika kidato cha kwanza. Kitabu tulichoteua ni *Uhondo wa Kiswahili, Kitabu cha Wanafunzi 1* cha Moran Publishers. Kutoka kidato cha pili, tuliteua vitabu viwili vya mafunzo yaani *Kiswahili Kitukuzwe, Kitabu cha Wanafunzi Kidato cha 2 Toleo la Sita* cha Kenya Literature Bureau na *Kiswahili Fasaha Kidato cha 2 Toleo Jipya* cha Oxford University Press. Tuliteua vitabu viwili vya kidato cha pili kwa sababu ni wanafunzi wa kidato hiki waliolengwa na utafiti huu.

### 3.3 Vifaa vya Utafiti

Kwa ajili ya kukusanya data kuhusu makosa katika maandishi ya wanafunzi, tulitumia mazoezi ya aina tatu. Mazoezi haya yalikuwa ya Viasho, Jozi za Mlinganuo Finyu na Insha. Tulizuru kila shule kibinafsi ili kuwasilisha mazoezi haya kwa watafitiwa kwa usaidizi wa mwalimu mmoja kutoka kila shule husika. Tulitumia penseli na karatasi kama vifaa vya kurekodi data.

#### 3.3.1 Zoezi la viasho

Katika zoezi la viasho, (Taz. Kiambatisho E) mtafitiwa alihitajika kujaza mapengo katika kifungu alichopewa akitumia maneno maalum. Kifungu hiki kilimwelekeza

mtafitiwa kuhusu neno lililostahili kujaza kila pengo na haikuwa vigumu kujua neno mwafaka kutokana na mdokezo uliokuwa katika baadhi ya maneno yaliyotumiwa katika kifungu chenyewe. Kati ya maneno kumi (10) yaliyostahili kujaza mapengo, kila moja kati ya maneno manane (8) lilikuwa sehemu ya jozi za vitate. Tahajia sahihi ya maneno mwafaka ndiyo iliyokuwa na umuhimu kwetu kwa sababu tulikuwa tunapima uwezo wa mwanafunzi katika kuandika tahajia sahihi ya maneno yanayotokea katika jozi za vitate. Kama inavyoeleweka vitate ni jozi za maneno yanayokaribiana kwa matamshi kwa sababu ya kutofautiana kwa sauti moja au mbili zinazotokea katika mazingira yale yale ya maneno husika ila yana maana ambayo ni tofauti kabisa.

Aghalabu, mwanafunzi anayeshindwa kutamka vitate, hutatizika katika kuyaandika maneno hayo na kwa hivyo atafanya makosa ya kitahajia anapoyaandika. Namna ilivyo ni kwamba maneno yote ya Kiswahili hutamkwa jinsi yanavyoandikwa. Lengo la zoezi hili lilikuwa ni kutambua makosa ya kifonolojia. Haya ni makosa yanayotokana na matamshi ya mwanafunzi. Makosa katika utamkaji yalidhihirika kwa njia ya kuyaandika maneno yenyewe na hii ilisaidia kutambua makosa ya kitahajia.

### 3.3.2 Zoezi la jozi za mlinganuo finyu

Katika zoezi la jozi mlinganuo finyu (Taz. Kiambatisho F), mtafitiwa alihitajika kutunga sentensi akitumia kila moja ya jozi kumi (10) za maneno ili kuonyesha tofauti ya maana ya kila neno katika jozi husika. Maneno haya yalihusisha jozi za mlinganuo finyu. Lengo la zoezi hili lilikuwa ni kutambua aina nyingine za makosa kama yale yanayohusiana na upatanisho wa kisarufi, udondoshaji wa maneno,

kujirudia na mnyambuliko mbali na yale ya kimatamshi. Aidha, utambuzi wa makosa ya kitahajia ulirahisishwa kupitia kwa zoezi hili.

Sababu ya kutumia zoezi hili ilikuwa kwamba utungaji wa sentensi ni shughuli changamano kuliko kuandika neno moja moja na kwa hivyo uwezekano wa kutokea makosa zaidi, na ya aina nyingine, ulikuwa mkubwa. Tofauti nyingine baina ya zoezi hili na lile la kwanza ni kwamba katika zoezi hili, maneno ya jozi za mlinganuo finyu yalikuwa yameandikwa na kwa hivyo tahajia ya maneno haya haikufaa kumtatiza mtafitiwa.

### 3.3.3 Zoezi la insha

Zoezi la insha (Taz. Kiambatisho G) lilikuwa la kuandika insha yenye urefu wa maneno baina ya 120 na 150 kuhusu mada: **'Mambo yanayozingatiwa wakati wa kuwapa watoto majina katika kabila langu'**. Uteuzi wa mada hii ulikusudia kutambulisha jamii anayotoka kila mtafitiwa ili kuyatambua makosa yanayotokana na matamshi ya lugha ya kwanza ya mtafitiwa. Aidha, katika insha yake alihitajika kutoa mifano ya majina katika kabila lake kwa ajili ya kuweka wazi kabila analorejelea. Kulingana na jinsi mada ilivyobuniwa, ni mwanafunzi asilia wa jamii husika pekee ambaye angeweza kuiandikia mada hii na kwa hivyo mwanafunzi aliyekuwa na nia ya kuhadaa kuhusu kabila angetambulika. Idadi ya maneno 120 ilitoa fursa kwa mtafitiwa kujieleza kwa urefu zaidi kuliko ilivyokuwa katika viwango vya neno na sentensi. Kwa kujieleza hivi, fursa ya kutokea makosa ilipatikana na kwa hivyo kurahisisha utambuzi wa makosa jinsi yanavyodhihirika. Uchangamano hujitokeza namna mwanafunzi anavyovuka kutoka kwa sentensi moja hadi nyingine pamoja na aya moja hadi nyingine. Aya ni kipashio changamano zaidi kuliko neno na sentensi moja ikiwa katika hali ya mtengo. Insha humpa mtafitiwa uhuru wa kujieleza na matatizo yake katika matumizi ya lugha yanadhihirika kwa urahisi zaidi. Hivyo basi,

insha ilikuwa kifaa muhimu cha kukusanyia data ya kutumiwa katika uchanganuzi wa makosa. Kifaa hiki kilitufaa pakubwa katika kutambua aina mbalimbali za makosa katika vitengo vya tahajia na sarufi.

Mtafiti alizuru kila shule binafsi ili kuwasilisha mazoezi haya kwa kila mtafitiwa aliyeteuliwa kwa usaidizi wa mwalimu mmoja katika kila shule. Tulizingatia utaratibu wa usampuli ulioelezwa chini ya 3.2. Tulizuru shule tatu kila siku. Ilituchukua siku tatu kuzuru shule zote na kukamilisha utafiti wa nyanjani. Mazoezi yote matatu yaliwasilishwa wakati mmoja kwa kila mwanafunzi aliyeteuliwa na kupewa muda wa saa moja na nusu kufanya mazoezi yote matatu.

**3.4 Ukusanyaji wa Data**

Baada ya wanafunzi wote kumaliza kufanya mazoezi haya, nakala za mazoezi yote zilikusanywa na mazoezi yote matatu yakasahihishwa kwa kupigia mistari tungo zenye makosa. Baadaye tulizinukuu tungo hizi na kuziorodhesha chini ya makundi mawili yaani Makosa ya Kitahajia na Makosa ya Kisarufi. Makosa ya Kitahajia na Kisarufi katika vitabu vya kiada yalitambuliwa kwa kusoma nakala za vitabu husika na kupiga msitari kwa penseli chini ya kila tungo iliyokuwa na kosa katika kila kitabu.

Kwa sababu tulikuwa tunashughulikia eneo la jamiimseto, ilibidi kuwahoji baadhi ya wasemaji wa kwanza wa lugha za Walenjin Nandi na Kipsigis), Wakikuyu, Waluo na Wateso ili kutambua makosa ya kimaandishi katika kazi za wanafunzi yaliyotokana na athari za lugha ya kwanza ya wanafunzi. Tuliwaomba kutafsiri baadhi ya vifungu katika maandishi ya wanafunzi kutoka kwa Kiswahili hadi lugha zao za kwanza. Mtafiti alinakili tafsiri akitumia lugha hizo huku akisaidiwa na hawa wasemaji wa kwanza wa lugha hizi. Kwa sababu mtafiti ni msemaji asilia wa Kibukusu, aliweza

kutambua makosa yaliyotokana na lugha ya kwanza miongoni mwa wanafunzi kutoka jamii za Waluhya bila kuhitaji usaidizi wa wasemaji asilia wa jamii za Kiluhya.

**3.5 Uwasilishaji wa Data**

Data kutoka katika kila kitabu cha kiada ilipangwa katika orodha iliyofuata utaratibu wa kurasa ambapo makosa yaliyotokea mwanzoni yaliratibiwa kwanza na yale yaliyotokea baadaye yakaorodheshwa nyuma. Kwa hivyo, tofauti na ilivyokuwa katika MYW, makosa katika VVK hayakutengwa katika vitengo vya Tahajia na Sarufi. Data yote iliorodheshwa katika viambatisho vinne vilivyotambulishwa kwa kupewa herufi za alfabeti zifuatazo: **A, B, C** na **D**. Makosa yaliyopatikana katika MYW yalipangwa katika Kiambatisho **A** tukianza na yale ya Kitahajia kisha yale ya Kisarufi. Viambatisho **B, C** na **D** vilijumuisha makosa yaliyopatikana katika VVK kwa utaratibu huu: **B** - *Uhondo wa Kiswahili*, **C** - *Kiswahili Kitukuzwe* na **D** - *Kiswahili Fasaha*. Baada ya kunakili kila tungo iliyokuwa na kosa kutoka kila kitabu cha kiada katika sehemu ya kwanza ya kila jozi, tuliandika kifupisho ‘uk.’ yaani kifupi cha ‘ukurasa’, kisha tukafuatisha namba ya tarakimu zilizoonyesha ukurasa wenye tungo hiyo na hatimaye kifupisho cha anuani ya kitabu cha kiada ambamo kosa lilipatikana kama ifuatavyo:

1. *Uhondo wa Kiswahili* tulitumia UWK
2. *Kiswahili Kitukuzwe* tulitumia KK
3. *Kiswahili Fasaha* tulitumia KF

Katika orodha ya makosa katika kila kiambatisho, kila aina ya kosa ilipewa namba kuanzia 1 ambapo kila namba ilikuwa na jozi ya tungo. Tungo ya kwanza katika kila jozi ndiyo ilikuwa na kosa au makosa na ilipewa herufi ‘**a**’ ilhali tungo ya pili inayoonyesha masahihisho kwa kosa au makosa, ilipewa herufi **‘b’**. Licha ya kufanya hivi, kulikuwa na mifano michache ya tungo ambazo hazikuwa kamilifu. Katika tungo za aina hii, tulitoa maelezo ndani ya mabano mwishoni mwa sehemu ya jozi

yenye herufi '**a**' kuonyesha kwamba tungo haikuwa imekamilika. Makosa yaliyokuwa katika kila tungo yalibainishwa kwa kukoleza neno au maneno yaliyokuwa na kosa au makosa. Katika mifano mingine ya tungo, kulikuwa na zaidi ya aina moja ya kosa. Katika tungo za aina hii, tulikoleza maneno yote yaliyokuwa na makosa katika tungo inayohusika na kuyawasilisha kupitia viambatisho vilivyo mwishoni mwa tasnifu hii.

Kadhalika, katika tungo ambazo makosa yake yalikuwa ni kudondoshwa kwa neno au maneno, maadamu hakukuwa na neno lenye makosa katika tungo yenye herufi 'a' ili likolezwe, tulitumia alama ya achwa (yaani ^) mahali katika tungo ambapo neno lililodondoshwa lilistahili kuandikwa. Katika tungo za aina hii tulikoleza neno katika tungo 'b' ambalo lilidondoshwa na lilistahili kuchopekwa katika tungo 'a'. Kwa kuzingatia takwimu kuhusu idadi ya makosa, majedwali, michoro ya grafu na duara ilitumiwa katika kuwasilisha baadhi ya data.

**3.6 Uchambuzi wa Data**

Data ilichambuliwa katika makundi makuu mawili ya Tahajia na Sarufi kila moja katika sura tofauti. Tulianza kwa makosa ya kitahajia kwa kufuata utaratibu wa Makosa ya Kudondosha, Kuchopeka, Kubadilisha Herufi Katika Maneno, Kutenganisha Neno na hatimaye Kuunganisha Maneno. Katika kila kundi dogo, tulianza kwa kuchambua makosa yaliyokuwa katika maandishi ya wanafunzi kisha makosa katika vitabu vya kiada yakafuatia. Uchambuzi wa Makosa ya Kisarufi ulifuata utaratibu wa Makosa ya Kudondosha Maneno, Kuchopeka Maneno, Upatanisho, Minyambuliko na hatimaye Uambishaji. Wakati wa kuchambua tuliirejelea kwa kuiorodhesha tukionyesha namba yake katika kiambatisho husika kwa kuzingatia malengo mawili ya kwanza ya utafiti huku tukiongozwa na Nadharia ya Uchanganuzi wa Makosa.

### 3.7 Hitimisho

Katika sura hii, tulifafanua muundo wa utafiti wetu kwa kueleza mahali ambapo data yetu ilipatikana, vifaa tulivyotumia katika kukusanya data na mbinu tulizotumia ili kupata data yenyewe. Tulionyesha kwamba utafiti wetu ulihusu kwenda nyanjani kwa ajili ya kukusanya data iliyohusu maandishi ya wanafunzi na vilevile kwenda maktabani kusoma vitabu vya kiada ambavyo vilikuwa asili nyingine ya data ya utafiti wetu. Vifaa vyetu vya utafiti vilikuwa ni mazoezi matatu yaliyowasilishwa kwa wanafunzi. Tumeeleza jinsi tulivyopanga data yenyewe ili kurahisisha urejelewaji wakati wa kuichambua kulingana na malengo ya utafiti wetu. Katika Sura ya Nne, tumeanza kwa kuchambua makosa ya kitahajia kama yalivyojitokeza katika MYW na katika VVK.

# SURA YA NNE

## UHAKIKI WA MAKOSA YA KITAHAJIA

### 4.0 Utangulizi

Katika sura hii tumefafanua aina mbalimbali za makosa ya kitahajia jinsi yalivyotokea katika MYW na VVK kwa mujibu wa lengo la kwanza la utafiti huu. Kulingana na *Kamusi ya Kiswahili Sanifu Toleo la Nne,* tahajia ni uwakilishaji wa sauti kwa herufi katika maandishi kufuatana na mwendelezo wa maneno uliokubalika. Nayo *Kamusi ya Karne ya 21 Toleo Jipya* inaeleza tahajia kuwa utaratibu wa kutumia herufi kuandika maneno, utaratibu wa kuendeleza maneno; maendelezo, hijai. Katika sura hii tumehakiki makosa yanayohusiana na kutumia herufi katika kuwakilisha sauti katika maneno kwa kuzingatia Kiswahili sanifu. Makosa ya aina hii yamegawanywa katika vitengo vitano ambavyo ni: kudondosha, kuchopeka na kubadilisha herufi ambazo zinasadifu kuwa ni sauti kwa mujibu wa fonolojia ya Kiswahili, kutenganisha neno na kuunganisha maneno. Vitengo viwili vya mwisho vinarejelea maumbo ya maneno ya Kiswahili sanifu yaani mofolojia. Katika baadhi ya mifano ya makosa, herufi zilizodondoshwa ni silabi.

Katika uchambuzi wa makosa katika kila kundi tumeanza kwa makosa yaliyotokea katika maandishi ya wanafunzi yanayoashiriwa kwa ufupi kama MYW kisha yakafuata makosa kutoka vitabu vya kiada kwa ujumla bila kutenga makosa kutoka kila kitabu tulichorejelea. Makosa katika kila kitabu yametambulishwa kwa kutumia vifupisho tulivyotaja awali katika sehemu ya 3.5 tukifuata utaratibu wa UWK, KK na KF mradi makosa tunayochambua yawe katika kitabu husika. Ikiwa aina ya makosa tunayochambua katika kitengo fulani haikupatikana katika kitabu fulani, hakikurejelewa. Kulikuwa na kisa kimoja ambapo kwa sababu ya kuwa na mfano

mmoja wa kosa hatukulitenganisha na kulichambua chini ya makosa katika VVK bali tulirejelea kosa hili kijumla (Rej. 31. a KF uk. 171).

### 4.1 Kudondosha Herufi

Kudondosha herufi kunarejelea hali ambapo herufi moja au zaidi inaachwa wakati wa kuandika neno. Katika ya maneno mengi, makosa ya kudondosha herufi yalidhihirika kwa kuachwa herufi moja na katika visa vichache herufi mbili zilidondoshwa katika baadhi ya maneno. Mifano yote ya makosa ya kuachwa kwa herufi mojamoja kwa kila neno ilitokea kuwa sawasawa na sauti moja yaani kila herufi iliyodondoshwa katika neno, ilikuwa sauti.

Kulikuwa na udondoshaji wa konsonanti na silabi na baadhi silabi zilikuwa ni irabu. Kulikuwa na makosa mengi ya kudondosha konsonanti kuliko silabi ambapo makosa ya kudondosha konsonanti yalitokea mara 39 dhidi ya yale ya irabu yaliyotokea mara 6. Kijumla haya ni makosa ambayo yanaweza kuhusishwa na matamshi ya wanafunzi ilmuradi maandishi huathiriwa na matamshi. Kwa hivyo tunaweza kuyahusisha makosa haya na fonolojia kwa sababu sauti na silabi ni vipashio vya kimatamshi.

#### 4.1.1 Kudondosha konsonanti: maandishi ya wanafunzi

Makosa ya udondoshaji yalidhihirika kupitia kwa konsonanti h, n, y, w na d. Visa vingi vya kudondosha konsonanti vilihusu h**.**

2. a) Hii ni **dhairi shairi** kwamba mtoto yule ana baraka nyingi sana.
3. a) Wanafunzi walikuwa na **aya** kuzungumza.
4. a) Asipokudhamini **awezi** kuniamini mimi.
5. a) Pia mtoto **upewa** jina la … baba.
13. a) Mgeni alikuja jana **jiani**.
14. a) Nilihisi **jaa** wakati wa shule.
18. a) Mtoto **aliezaliwa** wakati wa matanga huitwa Masika.
19. a) Njia nyingine ni kama mtoto **akiekwa** halafu akataye.
35. a) Kina mama **umpa** mtoto aliyezaliwa jina.
36. a) Kizazi chake **akipendez**i.
37. a) Asipokudhamini **aendi** tena.
42. a) Yeyote kati ya **dugu** zangu aliyekaidi …

Mifano hii inadhihirisha kwamba herufi ‘**h**’ ambayo kama sauti /h/ ni kikwamizo ghuna cha kooni pamoja na nazali ya ufizi /**n**/ zimedondoshwa mara nyingi zaidi zikiwa mwanzoni mwa neno kuliko inapokuwa katikati ya neno. Udondoshaji wa herufi ‘**h’** katika 2a umetokea katika kielezi ilhali katika mfano namba 3a **‘h’** imedondoshwa kutoka nomino ‘**haya**’ kwa maana ya fedheha. Katika 4a, 5a, 35a, 36a na 37a, ‘**h**’ imedondoshwa katika vitenzi vilivyokanushwa. Hii inaonyesha kwamba wanafunzi waliofanya makosa haya wana udhaifu wa kuandika vitenzi vinapokanushwa katika nafsi ya pili umoja na nafsi ya tatu katika umoja na wingi kwa sababu herufi ‘**h**’ ni kiungo muhimu wakati wa kukanusha vitenzi katika nafsi hizi. Kwa hivyo wanafunzi walifanya makosa ya kudondosha konsonanti ‘**h**’ katika maandishi ya vitenzi kuliko katika aina nyingine za maneno.

Makosa ya kudondosha herufi ‘**h’** yana asili yake katika matamshi ya wanafunzi wenye asili ya Wakalenjin hasa, Wanandi na Wakipsigis ambao walishirikishwa katika utafiti wetu. Ugunduzi huu unatokana na kuwahoji wasemaji wa kwanza wa lahaja hizi pamoja na tajriba ya mtafiti ambaye amekuwa akiwafunza wanafunzi katika shule zilizo katika maeneo yanayokaliwa na Wakalenjin kwa zaidi ya miongo miwili. Sababu ya wanafunzi wenye asili ya Kalenjin kudondosha konsonanti /h/ katika maandishi yao ni kwamba, kwa mujibu wa fonolojia ya Kinandi na Kipsigis, ambazo ni miongoni mwa lahaja za Kalenjin, konsonanti /h/ haiko katika sauti za Kikalenjin. Katika jedwali lifuatalo kuna konsonanti 13 za Kipsigis na Nandi na mifano ya maneno ya Kipsigis yanayotumia kila konsonanti inayolengwa kisha tafsiri ya Kiswahili Sanifu ya hayo maneno imefuatia.

**Jedwali 4.1: Konsonanti za Nandi na Kipsigis**

| | Sauti | Mfano wa maneno | Tafsiri ya Kiswahili Sanifu |
|---|---|---|---|
| 1. | /p/ | *pakakten* | acha |
| 2. | /t/ | *Telel* | simama |
| 3. | /ch/ | *chakchin* | harakisha |
| | | *chagun* | njoo haraka |
| 4. | /k/ | *konorwon* | nihifadhie |
| 5. | /m/ | *matinye* | sina kitu fulani |
| | | *matinyon* | usije |
| 6. | /n/ | *nee* | nyinyi |
| | | *naru* | acha nilale |
| 7. | /ny/ | *Nyone* | yuaja |
| | | *nyoon* | njoo |
| 8. | /ng'/ | *ng'alal* | ongea |
| | | *ng'alalwon* | ongea nami |
| 9. | /s/ | *samse* | anaomba kitu |
| 10. | /r/ | *rarwech* | haitatutosha |
| 11. | /l/ | *laale* | anakohoa |
| 12. | /y/ | *yaywon* | nisaidie |
| 13. | /w/ | *waach* | piga kamsa |

Asili: Kattam R. J, (2014) *Master of Arts Thesis: Nandi Consonants*

Habari hizi tulizipata baada ya kuwahoji baadhi ya wasemaji asilia wa Nandi na Kipsigis ambao walithibitisha kauli hii. Aidha, walisema kwamba hakuna neno lolote linaloanza kwa herufi '**h'** katika Kikalenjin. Hata katika majina ya maeneo zinakoishi jamii hizi, hakuna mahali popote ambapo jina lake huanza kwa herufi '**h'**. Kwa sababu ya kutokuwepo kwa sauti hii katika Kikalenjin, wanafunzi hawawezi kuwa nayo katika matamshi yao. Wanafunzi kutoka jamii hii wanapokutana na sauti hii ama wataidondosha katika matamshi na vivyo hivyo kuiacha katika maandishi au wanaweza kuipachika popote bila mpango maalum kwa sababu ya kutokuwa na uhakika. Kwa hakika, haiwezekani mtu kutumia kitu ambacho hana na aghalabu anapokutana na kitu kipya asichojua matumizi yake, kuna uwezekano wa kukitumia bila kujali. Matokeo yake ni kwamba kitu hicho kinaweza kutumiwa vibaya. Hii ndiyo sababu wanafunzi wenye asili ya Kalenjin huipachika herufi '**h'** mahali

pasipofaa katika maneno kwa sababu uelewa wao wa Kiswahili ni kwamba herufi hii iko miongoni mwa sauti za Kiswahili sanifu.

Tungo 13a, 14a na 42a ni mifano ya udondoshaji wa nazali ya ufizi **‘n’**. Kwa kuchunguza mifano hii, inadhihirika kwamba herufi **‘n’** zinazofuatwa na herufi **‘j’**, **‘d’** na **‘g’** katika maneno zimedondoshwa katika maandishi. Sio herufi **‘n’** zote zinadondoshwa bali ni zile ambazo zinafuatwa na vipasuo ghuna. Kwa mfano, katika 13a, kuna herufi **‘n’** tatu ambazo zimedumishwa katika kuandika maneno ‘mge**n**i’, ‘ja**n**a’ na ‘jia**n**i’ (njiani) na hizi ni herufi ambazo zimetokea katika mazingira yaliyo baina ya irabu.

Katika 14a, **‘n’** kwenye neno ‘**n**ilihisi’ ilidumishwa kwa vile inafuatwa na irabu yaani ‘i’. Ingawa **‘n’** katika neno ‘za**n**gu’ katika 42a inafuatwa na kipasuo ghuna **/g/**, hili neno lilikuwa katika zoezi la viasho na lilikuwa limechapishwa tayari katika zoezi lenyewe na kwa hivyo watafitiwa hawakuhitajika kuliandika. Tungo hizi zilitokana na MYW kutoka jamii ya Kikuyu. Makosa haya yanatokana na utekelezaji mbaya wa kanuni ya Kiswahili sanifu ambapo utangulizi wa nazali katika vizuiwakwamizwa hutegemea maneno binafsi na kwa hivyo hautokei kila mara.

Kutokana na kuchanganya kanuni hii na ile ya Kikuyu ambapo vizuiwa vyote vyenye mghuno (vipasuo na vizuiwakwamizwa) hutangulizwa kwa nazali katika lugha ya Kikuyu na kwamba katika Kiswahili kuna wakati ambapo nazali hudondoshwa, wanafunzi walijumlisha kanuni hii kwa kudondosha nazali zilizotangulia kizuiwakwamizwa /**j**/, na vizuiwa /**d**/ na /**g**/. Walifanya hivi kwa kuhofia kwamba ikiwa wangeziandika wangekuwa wanakosea kwa sababu walitambua kwamba Kiswahili ni tofauti na lugha yao ya Kikuyu. Kwa hivyo, tunaweza kudai kwamba wanafunzi kutoka jamii ya Kikikuyu hudondosha nazali **/n/** ikitokea katika mazingira

ya konsonanti zenye sifa za vizuiwa ghuna kutokana na kujumlisha kanuni kwamba utangulizi wa nazali hutegemea maneno binafsi katika Kiswahili sanifu. Hali hii ya kudondosha inahusu nazali **n** na **m** zinapofuatwa na sauti ghuna mwambatano katika maneno. Kwa sababu hii, maneno kama **ndama, mbuzi, ngoma** na **njama** yatatamkwa kama **dama, buzi, goma** na **jama**. Hivyo ndivyo yatakavyoandikwa na hapo makosa ya kudondosha nazali kutokea katika MYW.

Makosa ya udondoshaji wa konsonanti katika maandishi ya wanafunzi yalihusu herufi **'w'** na **'y'** ambazo ni viyeyusho **/w/** na **/y/** jinsi inavyoonyeshwa katika 18a na 19a hapo juu. Katika 18a, kiyeyusho cha kaakaa gumu **/y/** kimedondoshwa katika kiambishi awali cha urejeshi **-ye-** katika umoja wa Ngeli ya A-WA kwenye kitenzi '**akiekwa**'. Katika 19a, kiyeyusho cha midomoni **/w**/, kimedondoshwa kwenye neno '**weka**'. Makosa haya yalitokea kwenye tungo za wanafunzi wa jamii za Kiluhya. Hali inayodhihirika hapa ni kwamba katika matamshi ya wanafunzi wa jamii za Kiluhya, viyeyusho hudondoshwa na kwa hivyo wakati wa kuandika maneno yenye viyeyusho herufi hizi hudondoshwa.

### 4.1.2 Kudondosha konsonanti: vitabu vya kiada

Mifano ifuatayo ilinukuliwa kutoka kwenye VVK na inadhihirisha jinsi konsonanti zilivyodondoshwa kutoka maneno yaliyokolezwa wino**.**

20. a) Nilikuwa ninaamini kwamba ni bora kila mtu **ajishuhulishe** na mambo yake… UWK uk. 104
23. a) Katika wingi vivumishi **ambavo** mzizi wake unaanza na konsonanti huambishwa kiambishi awali ***vi***- UWK uk.108

Katika 20a, kikwamizo ghuna cha kaakaa laini, **/gh/** (ambayo ni konsonanti mwambatano), kimepoteza moja katika jozi zake yaani **/g/** (hiki ni kipasuo ghuna cha kaakaa laini). Sehemu ya pili ya konsonanti mwambatano hiyo inayosalia baada ya kipasuo kudondoshwa, inakuwa kikwamizo ghuna cha kooni yaani **/h/**. Aidha, katika

23a, udondoshaji wa kiyeyusho cha kaakaa gumu /**y**/, umetokea katika kirejeshi '**amba-**' katika Ngeli ya KI-VI katika wingi. Tunaona kwamba kwa sababu ya mazoea ya kutamka maneno '**shughuli**' kama '**shuhuli**' na '**ambavyo'** kama '**ambavo**' kumekuwa na udondoshaji wa '**g**' na '**y'** katika maandishi yaliyo katika UWK. Si ajabu kwamba hata wanafunzi wamefuata matamshi ya lugha yao na kudondosha baadhi ya herufi katika maneno. Kwa mfano, katika 18a kiyeyusho /**y**/ kimedondoshwa na wanafunzi sawasawa na jinsi kilivyodondoshwa katika '**ambavyo**' katika kitabu cha kiada.

Kwa sababu kitabu cha kiada ni chapisho rasmi linalopitia hatua kadhaa kuanzia uandishi, upigaji chapa hadi uhariri, kosa hili haliwezi kuhusishwa na hali ya kutojali. Kuna uwezekano kwamba kosa hili linatokana na kuathirika kimatamshi kwa waandaaji wa kitabu hiki. Athari hizi zimedhihirika katika MYW kudondosha kiyeyusho kutoka katika viambishi vya urejeshi jinsi inavyoonekana katika 18a. Kutokea kwa makosa katika VVK vilevile kunaweza kuhusishwa na lafudhi. Katika matamshi ya baadhi ya watu sauti **/vy**/ hutamkwa bila /**y**/ ambapo hutamkwa /**v**/. Kwa mfano badala ya **'asemavyo'** watu hao watatamka **'asemavo'** na kuishia kuyaandika maneno jinsi walivyoyatamka. Huku ni kukiuka kanuni ya uyeyushaji ambapo irabu ya mbele juu /**i**/ huwa kiyeyusho cha kaakaa gumu /**y**/, inapotokea baina ya vikwamizwa vya mdomomeno, /**f**/ na /**v**/ na irabu zile nyingine (a, e, o na u) kama inavyodhihirika katika mifano ifuatayo:

1. vi + -etu = **vyetu** sio **vietu**
2. vi + -angu = **vyangu** sio **viangu**
3. vi + -ake = **vyake** sio **viake**
4. **afya** sio **afia**
5. **fyeka** sio **fieka**
6. f**yonza** sio **fionza**

Mifano hii yote inaonyesha kwamba tahajia sahihi ya maneno ambayo yanaanza kwa konsonanti za mdomomeno na yanapounganika na irabu ya mbele juu /**i**/ huhusisha uyeyushaji wa irabu hiyo /**i**/. Kuidumisha irabu hiyo katika kuandika ni kosa la kitahajia linalokiuka kanuni ya uyeyushaji. Kosa lililo katika 18a, lina asili yake katika kupuuza kanuni ya uyeyushaji na kudondosha kiyeyusho na linahusiana na athari za lafudhi ya jamii za pwani ya Kenya.

### 4.1.3 Kudondosha silabi: maandishi ya wanafunzi

Silabi ni kipashio cha kimatamshi kinachotokana na muungano wa sauti. Ipo miundo mbalimbali ya silabi kutokana na kuwepo kwa aina mbili kuu za sauti, yaani irabu na konsonanti. Katika miundo ya silabi za maneno ya Kiswahili sanifu, kuna miktadha ambapo irabu inaweza kuwa silabi. Katika tungo za wanafunzi, silabi zilizodondoshwa zilitokea kuwa irabu kama inavyoonekana kwenye mifano ifuatayo:

21.a) Pia katika **jami** ya Wakikuyu.
43.a) Jina ni Okware **yani** usiku.
44.a) Mwelimishe mwana huyu **manake** yeye ndiye kizazi **kijao**.

Tuliyahusisha makosa na jamiilugha maalum kutokana na mifano ya majina ambayo walitaja kutoka jamii zao ndani ya zoezi la insha. Tuliyahusisha makosa ya aina hii na Kiswahili kuingiliwa na lugha ya kwanza ya wanafunzi. Mengi ya makosa ya namna hii yalikuwa ni ya kitahajia.

Katika tungo hizi, irabu /**i**/ na /**a**/ zimedondoshwa katika maneno yaliyokolezwa. Katika mofolojia ya Kiswahili irabu hutekeleza wajibu wa kuonyesha mipaka baina ya silabi moja na nyingine hivi kwamba irabu mbili zikifuatana katika neno lolote, zinakuwa katika silabi tofauti. Kwa sababu ya kudondoshwa kwa irabu mojamoja kutoka kila neno, imesadifu kwamba ni silabi zilizodondoshwa katika maneno yanayohusika. Makosa haya yana asili yake katika matamshi. Katika matamshi ya

baadhi ya wanafunzi ni kawaida kukosa kutamka moja ya irabu zinazofanana zinapofuatana katika neno. Kwa sababu ya kutamka hivi, wakati wa kuandika vilevile wataandika wakidondosha irabu moja. Kosa la aina hii linaweza kuwa ishara ya wanafunzi kuathiriana wao kwa wao katika mazungumzo yao. Maingiliano baina ya wanafunzi hawa kutoka jamiimseto yaliwafanya kudondosha irabu /**i**/ na /**a**/ katika maandishi yao.

Hali kadhalika, makosa yaliyo katika 21a na 43a yanaweza kuhusishwa na athari kutoka lugha ya kwanza ya wanafunzi. Makosa haya yalitokea kwenye wanafunzi wa ya asili ya Kikuyu. Kikuyu kina irabu msingi saba zinazojumuisha ndefu na fupi. Hii ni tofauti na Kiswahili ambacho kina irabu msingi tano na zote ni fupi. Kwa kuidondosha irabu /**i**/ katika neno **'jamii'** katika 21a, tunaweza kusema kwamba wanafunzi hawa wameathiriwa na lugha yao ya asili yaani, Kikuyu wakidhani kwamba haya ni mazingira ya irabu fupi kwa msingi wa lugha ya Kikuyu.

Mfano 43a, unawahusu wanafunzi wa jamii ya Kiteso ambayo, kama ilivyo katika lugha nyingi za Kinailoti, ina irabu fupi. Kutokana na kuwahoji baadhi ya wasemaji asilia wa Kiteso tuligundua kwamba maneno mengi katika lugha ya Kiteso hayana irabu zinazofuatana na kwa hivyo matamshi yao hufuata mkondo huu. Kwa hivyo, huku kuandika '**yani**' badala ya '**yaani**' ni dhahiri kwamba ni athari ya Kiteso katika Kiswahili.

### 4.1.4 Kudondosha silabi: vitabu vya kiada

Makosa ya kudondosha silabi yalitokea katika vitabu vyote vitatu vya kiada (VVK). Udondoshaji huu uliathiri mawasiliano moja kwa moja kwa sababu maumbo yaliyotokea hayakuwa maneno ya Kiswahili. Katika mifano hii, UWK ndicho

kilichosheheni makosa mengi ya kudondosha silabi kuliko vitabu vingine viwili. Zifuatazo ni tungo zilizokuwa na makosa haya katika VVK**:**

10. a) Baadhi ya **watalamu** wanaielezea fasihi kama maandishi ambayo yanathaminiwa kama kazi ya sanaa … UWK uk.10
21. a) Tulipaswa kulilia purukushani zetu na **mapuza** yetu. UWK uk. 104
32. a) Kijiji kizima kilipigwa na **butwa** wakati Zawadi alipotimuliwa kutoka kwa kishamba alichohalifu mumewe. UWK uk. 166
36. a) **Akafuliza** moja kwa moja hadi mwembeni ambapo mimi na wanawake wenzangu tulikuwa tunasukana. UWK uk. 175
30. a) Majizi yaliyokamatwa yatapelekwa **mahakani** kesho. KK uk.255
33. a) Kitabu hiki kinazungumzia **juu ya** maisha ya **mwanake** mmoja kwa jina Siti Binti Saad, ambaye alizaliwa katika kijiji cha Fumba huko Zanzibar. KF uk. 191
52. a) Yaani kuwafunika macho au kubururwa **mahakami**. KF uk. 226

Udondoshaji wa silabi ulidhihirika kwa njia mbili. Njia ya kwanza ilikuwa ni kupitia kwa silabi yenye muundo wa irabu. Irabu **'a'** imedondoshwa katika nomino '**maanake**', '**wataalamu**' na '**butwaa'**. Hii ndiyo irabu iliyodondoshwa mara nyingi zaidi kuliko irabu nyingine. Katika 21a, irabu **'u'** imedondoshwa katika nomino '**mapuuza**'. Zinapotokea irabu mbili au zaidi katika maneno ya Kiswahili, kila irabu hutamkwa kivyake kwa sababu huwa katika silabi tofauti. Katika utafiti wetu, silabi zenye muundo wa irabu '**a**' na '**u**' ndizo zilizodondoshwa katika kitabu kimoja cha kiada. Ikumbukwe kwamba katika tungo za wanafunzi kulikuwa na visa vya kudondosha irabu /**a**/ katika maneno. Huku kudondoshwa kwa irabu kumefanana na kule kuliko katika maandishi ya kiada tuliyonukuu. Tunaweza kudai kwamba wanafunzi waliodondosha irabu katika maneno waliiga makosa kwenye vitabu.

Mifano hii inadhihirisha kwamba ingawa lugha ya kwanza ya wanafunzi ni sababu ya kudondosha silabi katika tahajia ya maneno, vitabu wanavyosoma vinaweza kuwaathiri wakafanya makosa. Kwa waandishi wa vitabu, haya ni makosa madogo na yanaweza kusahihishwa kwa urahisi lakini katika muktadha wa mtihani hakuna kosa

dogo kwa vile makosa yote yana athari sawa kwa mwanafunzi. Hakuna kigezo cha kupima makosa ili kutofautisha baina ya makosa ya kiutendaji na yale yanayoashiria hali ya kuteleza katika muktadha wa mtihani.

Muundo wa pili wa silabi zilizodondoshwa ni ule unaohusisha konsonanti. Kulikuwa na makosa ya kudondosha silabi katika baadhi ya maneno kama inavyofafanuliwa kwenye maelezo yafuatayo. Katika 36a, silabi **'-lu-'** inayostahiki kutokea baina ya silabi **'-fu-'** na **'-li-'** katika umbo '**mfulizo**' (linastahili kuwa '**mfululizo**'), imedondoshwa. Hali ni hiyo hiyo katika 28a kwenye umbo '**mahakani**' ambalo linastahili kuwa '**mahakamani**' ambapo silabi **'-ma-'** baina ya silabi **'-ka-'** na **'-ni-'** imedondoshwa. Katika 33a, kuna makosa mawili ambapo lile la kwanza limeshughulikiwa katika Sura ya Tano chini ya 5.4 kuhusu Kuchopeka Neno. Kuhusu kosa la pili katika tungo hiyo, silabi ya konsonanti moja /**m**/ imedondoshwa baina ya '**a**' na '**k**' ambapo neno lilistahili kuwa '**mwanamke**'.

Udondoshaji katika 52a unahusu kumegwa kwa herufi mojamoja kutoka kwenye silabi mbili jirani yaani herufi **'a'** kutoka katika silabi **'ma'** na herufi **'n'** kutoka kwenye silabi **'ni'** katika neno '**mahakamani**'. Ilmuradi, kwa kufanya kosa hilo idadi ya silabi imepungua katika neno linalohusika, tumelijumuisha kosa hili pamoja na yale ya kudondosha silabi. Kutokea kwa makosa ya aina hii katika maandishi ya kiada ni thibitisho kwamba kuna ukosefu wa uangalifu miongoni mwa waandaaji wa kitabu hiki. Wahariri na wapiga chapa wanafaa kuwajibikia makosa haya. Huku kutomakinika pia kunaweza kuhusishwa na kuwa na haraka wakati wa kuandaa vitabu hivi. Umakinifu hupungua pale palipo na haraka ya kufanya mambo.

Wanafunzi wanaosoma vitabu vya aina hii wanapoona makosa kama haya katika vitabu, hujenga tabia ya kukukosa kumakinika katika uandishi wao na inapotokea

katika muktadha wa mitihani, kinachoshuhudiwa ni kudorora kwa matokeo kwa sababu ya kuadhibiwa kwa makosa. Hii ni ithibati kwamba makosa ya kitahajia miongoni wanafunzi hayatokani na matamshi yao tu bali pia yanachangiwa na makosa kwenye VVK.

## 4.2 Kuchopeka Herufi

Uhakiki wetu katika sehemu hii unachunguza makosa yanayohusu kuweka herufi isiyostahili kuwa katika neno. Katika kitengo cha makosa ya kitahajia, hii ndiyo aina ya makosa iliyokuwa ndogo zaidi. Katika VVK, kosa hili lilitokea mara moja pekee katika kitabu kimoja tu na kwa sababu hiyo tumelichambua kosa hilo katika sehemu hii. Kwa mujibu wa uhakiki huu, herufi zilizochopekwa katika maneno ni konsonanti **‘h’, ‘n’, ‘w’**, na **‘y’**, na irabu **‘u**’, na **‘a’** jinsi inavyodhihirika katika tungo zifuatazo kutoka kwa MYW:

1. a) Nyumba **hile** unatoa moshi.
15. a) Sisi kama Wakikuyu majina **hupokenzwa**.
17. a) Mwalimu alimuonya **awache** kuandika **aya** fupi.
19. a) Njia nyingine ni kama vile mtoto akiekwa halafu **akataye**.
20. a) Ukali wake **ulimusaidia** alipokamatwa na polisi.

Maneno yote yaliyokolezwa yana makosa ya kuongezewa herufi. Katika 1a, herufi **/h/** imechopekwa katika kivumishi kionyeshi cha mbali sana katika ngeli ya I-ZI umoja yaani, ‘**ile**’. Makosa haya yalisababishwa na matamshi mabaya ya maneno na ni kinyume cha hali iliyokuwepo katika kudondoshwa herufi. Inavyoonekana hapa ni kwamba wale wale wanafunzi kutoka jamii zilizodondosha viyeyusho kwenye matamshi ndio waliovichopeka vilevile. Kutokana na uzoefu wa kufunza wanafunzi wa jamii za Kikalenjin kama vile Nandi, Keiyo na Kipsigis, tuligundua kwamba wanafunzi hawa huchanganyikiwa katika kutamka maneno yanayoanza kwa irabu na yanayoanza kwa herufi **h**. Wengi wao hupachika sauti /**h**/ katika maneno yanayoanzia irabu na kwa hivyo wakati wa kuandika maneno hayo wataipachika katika maneno

kama inavyoonekana katika 1a anapoandika ‘**hile**’ akimaanisha ‘**ile**’. Kwa upande mwingine, wanafunzi hawa watadondosha /**h**/ katika matamshi ya maneno yaliyo na sauti hii kama tulivyoona katika sehemu ya 4.1.1 chini ya Kudondosha Konsonanti Katika MYW. Tatizo hili hutokea katika maandishi ambapo herufi hii itadondoshwa inapofaa kuwekwa na kupachikwa pale ambapo haistahili kuwepo. Kwa hivyo, tungo kama hizi zinaweza kujitokeza katika maandishi yao:

Nyumba **hile aiko maali** pazuri.
badala ya:
Nyumba **ile haiko mahali** pazuri.

Haya ni makosa yanayotokana na athari za lahaja za Kikalenjin.

Kuchanganyikiwa kama huku katika jamii ya Wakikuyu hutokea wanapotamka nazali /**n**/ na /**m**/ ambapo zinadondoshwa kutoka pale zinapofaa kuwa na kuchopekwa pale ambapo hazifai kuwa. Tuliona mifano ya kudondoshwa kwa /**n**/ katika sehemu ya 4.1.1 kuhusu udondoshaji wa konsonanti. Aidha, katika 15a, tunaona /**n**/ imechopekwa katika ‘hupoke**n**zwa’ badala ya kuandika neno ‘**hupokezwa**’.

Wanafunzi wenye asili ya jamii za Kiluhya nao wanatatizika katika kutamka maneno yenye irabu zinazofuatana ambapo wanachopeka viyeyusho /**w**/ na **/y**/ baina ya irabu mbili katika matamshi yao na kuidondosha kutoka mahali inapostahili kuwa jinsi tulivyoona katika 4.1.1 kuhusu Kudondosha Konsonanti. Matamshi haya huathiri maandishi yao na wanaishia kufanya makosa ya kitahajia. Hii ndiyo sababu ya kuandika ‘**awache**’ badala ya ‘**aache**’ katika 17a na ‘**akataye**’ badala ya ‘**akatae**’ katika 19a. Katika jamii hii hii ya Luhya, matamshi yao ya **/m**/ inapofuatwa na konsonanti huongezwa irabu /**u**/. Hali hii imesababisha kosa lililo katika 20a ambapo wameandika ‘ulim**u**saidia’ badala ya ‘**ulimsaidia**’. Hivyo basi, tunaona namna matatizo ya matamshi yanayotokana na lugha ya kwanza ya wanafunzi yalivyosababisha makosa ya kitahajia ya kuchopeka herufi katika maneno. Hapa

tunaona namna lugha ya kwanza ya mwanafunzi inavyoathiri maandishi ya mwanafunzi anayejifunza lugha ya pili.

Huu ni mfano wa kosa moja lililotokea katika kitabu kimoja cha kiada linalohusu kuchopeka silabi katika neno:

31. a) Hata niliwacheka kimoyomoyo nilipokuwa nikiwaona wakizionyesha tabia zao nyofu kwa **waalimu**… KF uk.171

Nomino ‘**walimu**’ ilichopekwa irabu tande ya chini kati, /**a**/ katika 31a kwa kupuuza kanuni ya kimofofonemiki ya kudondosha irabu mbili zinazofanana zikitokea katika kiambishi awali na mzizi zikiunganishwa kuunda neno. Katika mfano huu, wakati wa kuambisha kiambishi awali cha wingi, **wa-** kwenye mzizi -**alimu** neno linalotokea ni **waalimu**. Kwa mujibu wa kanuni ya kimofofonemiki ya udondoshaji wa irabu zinapokutana, tahajia sahihi ya neno hilo inastahili kuwa **walimu.** Kosa hili linaashiria upungufu kwa waandishi wa kitabu kutekeleza kanuni hii ya kimofolojia. Kadhalika, kosa la aina hii linaweza kutokana na ujumlishaji wa tahajia ya neno hili na maneno mengine katika Kiswahili yaliyo na irabu zinazofuatana kama vile **taarifa, maarifa, maalum, taaluma, mtaala, mtaalam** na kadhalika. Hii ni kanuni inayohusu maneno ya mkopo katika Kiswahili sanifu na aghalabu mengi yanatokana na Kiarabu. Yamkini waandishi wa kitabu hiki wameathirika na mtindo huu ambao huhusu baadhi ya maneno. Ama pia tunaweza kudai kwamba kosa hili ni matokeo ya kutekeleza sheria bila kukumbuka vighairi vyake ambapo katika baadhi ya miktadha, sheria inayoeleweka haistahili kutumika kwa sababu katika kuitumia makosa hutokea.

### 4.3 Kubadilisha Herufi

Makosa ya kubadilisha herufi yalijitokeza kupitia kwa kuwekwa katika neno herufi tofauti na ile inayostahili kuwepo. Tuliyachambua makosa haya kwa kurejelea herufi kijumla katika MYW kisha katika VVK. Makosa haya yalijitokeza zaidi katika vitate.

Vitate vikitokea katika makundi huunda jozi za mlinganuo finyu. Tofauti za kimaandishi baina ya maneno katika kila jozi ni kwamba sauti moja ni ghuna ilhali nyingine ni sighuna. Kijumla basi, katika sehemu hii makosa yaliyotokea katika kuandika maneno yalihusiana na kushindwa kutofautisha sauti ghuna na sighuna.

### 4.3.1 Kubadilisha herufi: maandishi ya wanafunzi

Makosa yaliyodhihirika katika MYW kuhusiana na ubadilishaji wa vipasuo ni:

6. a) Mama **alipiga** ugali.
7. a) Mwalimu alizuru **mpuga** ya Tsavo.
38. a) Njaa **ilizuga** katika Lodwar.
39. a) Ugali nilioula **ulinishipisha**.
40. a) **Kulikuwebo** na karamu ya kukata na shoka.
41. a) Mtoto wa kike **hubewa** jina kama Akiteng'i.

Vipasuo ni sauti zinazotamkwa kwa kubana hewa kwenye ala za kutamkia kisha kuiachilia ghafla na kusababisha sauti ya mpasuko. Kwa sababu ya kuzuiliwa kwa hewa wakati wa kutamka vipasuo, neno 'vizuiwa' pia hutumiwa kama kisawe cha vipasuo. Sauti hizi ni: /p/, /b/, /t/, /d/, /k/ na /g/. Katika orodha hii vipasuo ghuna ni /b/, /d/ na /g/ ilhali /p/, /t/ na /k/ ni sighuna. Bado hapajakuwa na makubaliano kama sauti /j/ ni kipasuo. Massamba na wenzake (2004) wanaijumuisha katika vizuiwakwamizwa au vipasuokwamizwa na kwa sababu hiyo, hatujaihusisha miongoni mwa vipasuo katika kuhakiki makosa yanayohusu ubadilishaji wa konsonanti.

Isipokuwa katika 7a ambapo ubadilishaji wa kipasuo umetokea katika nomino '**mbuga**', mifano mingine yote inaonyesha kosa hili likitokea katika vitenzi. Katika 6a, na 38a, kipasuo ghuna cha kaakaa laini yaani, **/g/** kimetumiwa mahali palipostahili kuwekwa kipasuo sighuna cha kaakaa laini yaani, **/k**/. Ingawa '**alipiga**' ni neno la Kiswahili sanifu, lakini kitenzi '**piga'** (kinachomaanisha charaza) ambacho ndilo

shina la kitenzi hiki, kikihusishwa na nomino '**ugali**', sentensi hiyo inakosa kuwa na mantiki kwa sababu 'mama hawezi **kucharaza** ugali'.

Madhali mwanafunzi alinuia kutaja maana ya kitendo cha kuandaa chakula kiitwacho '**ugali**', basi neno sahihi lilikuwa '**pika**'. Katika muktadha huu, **/k/** na **/g/** ni fonimu tofauti. Kwa kubadilisha **/k/** na kuwa **/g/** maana iliyolengwa imepotea. Katika 38a, ubadilishaji wa **/k/** kuwa **/g/** umezalisha neno **'zuga'** ambalo lina maana ya **pumbaza**, **zubaisha** au **fanya kuwa mjinga**. Ijapokuwa njaa inaweza kupumbaza yaani, kumfanya mtu atende jambo lisilotarajiwa, lakini muktadha wa mwanafunzi ulikuwa na nia ya kuonyesha kutokea ghafla kwa kitu hasa bila kuwa tayari kukikabili yaani, **zuka**.

Kwa sababu njaa ni janga, hutokea ghafla na kuleta dhiki sio kupumbaza. Katika 7a, 39a, 40a na 41a ubadilishaji uliopo ni baina ya vipasuo vya midomoni **/b/** na **/p/** ambapo cha kwanza ni ghuna na cha pili ni sighuna. Kuandika **/p/** mahali pa **/b/** katika 7a, kulizalisha '**mpuga**' ambalo sio neno katika msamiati wa Kiswahili sanifu. Nomino ya pekee, '**Tsavo**' inarejelea mahali ambapo wanyama wa porini hutengwa kwa ajili ya kutazamwa na wageni na hii ndiyo inayoitwa '**mbuga**'. Kwa hivyo ubadilishaji wa **/b/** na **/p/** katika mfano huu umesababisha kutokea kwa umbo ambalo sio neno katika nomino za Kiswahili sanifu.

Vivyo hivyo, matokeo ya kuandika **/p/** badala ya **/b/** katika 39a, ni kuwepo kwa umbo lisilo katika msamiati wa Kiswahili. Neno sahihi lilistahili kuwa **'ulinishibisha'** ambayo ni kauli ya kutendesha ya kitenzi '**shiba**' kinachomaanisha tosheka na chakula wakati wa kukila. Kwa mujibu wa mwanafunzi, hapa neno asilia ni '**shipa**' ambalo sio kitenzi katika Kiswahili sanifu. Kiambishi tamati '**-po**' katika vitenzi hurejelea dhana mbalimbali kama wakati na masharti. Matumizi ya **/b/** badala ya **/p/**

katika 40a, yalisababisha umbo **‘kulikuwebo’** ambalo sio neno katika Kiswahili. Katika muktadha huu, alinuia kuleta dhana ya mahali. Kiambishi **‘-ku-’** kinaashiria mahali kijumla ilhali **‘-pa-’** ni mahali maalum. Kiambishi awali cha kwanza **‘ku-’** katika neno ‘**kulikuwebo**’ kinapoambatanishwa na mahali maalum ni kosa la kisarufi la kuchanganya ngeli za mahali. Katika kuteua kiambishi cha ngeli ya mahali ambacho hakifai yaani **‘-po’** badala ya **‘-ko’**, kosa la kisarufi linatokea, na kwa kubadilisha sauti /**p**/ kuwa /**b**/, kosa la kitahajia linatokea.

Katika 41a, neno lenye kosa la kitahajia linatokana na kitenzi chenye shina la silabi moja ‘**-pa’**. Kitenzi hiki kinaponyambuliwa katika kauli ya kutendewa kinakuwa ‘**pewa**’. Mwanafunzi anapobadilisha **/p/** kuwa **/b/**, kitenzi hiki kinakuwa ‘**bewa**’ ambalo ni neno la Kiswahili sanifu linaloingia katika kundi la nomino wala sio vitenzi. Kama nomino, maana yake ni ndaki au sehemu ndogo katika chuo kikuu ambayo ni maana iliyotofautiana kabisa na ile inayolengwa na tungo ya mwanafunzi. Makosa ya kubadilisha sauti **/p/** na **/b/** yalisababisha kutokea kwa maumbo ambayo hayatambuliki kama maneno ya Kiswahili sanifu na yalitokea katika vitenzi na nomino ingawa kulikuwa na makosa mengi zaidi katika vitenzi kuliko nomino.

Makosa haya yanasababishwa na athari za matamshi ya lugha ya kwanza. Tungo hizi zilitokana na MYW wenye asili ya Kiteso. Katika lugha ya Kiteso, kuna sauti nyingi ambazo ni sighuna. Hii ni tofauti na Kiswahili ambacho kina sauti ghuna nyingi (17) kuliko sighuna (8). Makosa yaliyodhihirika katika maandishi yao yanaonyesha kwamba wanaelewa tofauti iliyopo baina ya lugha yao na Kiswahili kuhusiana na sifa za ughuna na usoghuna katika konsonanti na kwa hivyo wanapoandika wanachanganya sauti ghuna na sighuna kwa sababu ya kushindwa kutofautisha miktadha inayofaa ghuna na ile ambayo haistahili. Hii ndiyo maana kulitokea hali hii

ya kutumia sauti ghuna mahali panapofaa sighuna nayo sighuna ikachopekwa mahali pa sauti ghuna. Tunaweza kusema kwamba wanafunzi hawa wanababahatisha katika kuteua baina ya ghuna na sighuna na ndiyo maana makosa haya hayana mfumo maalum.

Katika utafiti huu tulitambua kwamba vikwamizwa vilikuwa miongoni mwa sauti nyingine zilizobadilishwa. Vikwamizwa pia huitwa vikwaruzo. Miongoni mwa konsonanti za Kiswahili, vikwamizwa ndivyo vilivyo vingi zaidi ya aina nyingine za konsonanti. Baadhi ya vikwamizwa vya Kiswahili ni: **/f/**, **/v/**, **/th/**, **/dh/, /s/** na **/z/**. Katika orodha hii, **/v/**, **/dh/**, na **/z/** ni ghuna ilhali **/f/**, **/th/** na **/s/** ni sighuna.

Tulizingatia sauti hizi katika uchambuzi wetu kwa sababu makosa ya kubadilisha konsonanti yalihusu aina hizi za vikwamizwa. Hivyo basi, makosa katika vikwamizwa, kama yalivyokuwa katika vipasuo, yalitokana na udhaifu katika kutofautisha baina ya sauti ghuna na sighuna. Makosa yaliyotokea hapa yalihusu kubadilisha kikwamizwa ghuna cha menoni **/dh/** kuwa kikwamizwa sighuna cha menoni **/th/**. Udhaifu katika kutofautisha **/s/** na **/z/, /th/** na **/dh/, /f/ na /v/** na **/ch/** na **/j/** ulidhihirika katika MYW kwenye tungo zifuatazo:

8. a) **Asiyekuchua hakuthamini**.
9. a) Siku ya vijana kwenda **chondoni** wanapewa majina kama vile Maina.
10. a) Moshi **ulivuka** baada ya moto kuzuka.
11. a) **Waliwafua** samaki wadogo wadogo.
12. a) Mwanafunzi **amefunja** kalamu.
22. a) **Tulidhuru inchi** ya Kenya.
45. a) Huweza kufunzwa na kuelezewa **jinzi** wanavyoweza kumtunza mwana.

Methali ya Kiswahili ambayo husema '**Asiyekujua hakudhamini**' ndiyo inayodokezwa katika 8a. Maana yake ni kwamba mtu ambaye hajakufahamu hawezi akakusimamia kwa njia ya kukuwekea fedha unapokuwa na kesi ili uachiliwe na

mahakama. Ingawa tungo inayotokea katika kubadilisha **/dh/** kuwa **/th**/, ina maana kimantiki (yaani kwamba mtu ambaye hana habari kukuhusu hawezi kukustahi au kukuheshimu), ni wazi kwamba hii sio maana iliyokusudiwa na mwanafunzi. Kwa kukosa kutofautisha kwamba **/th/** ni sighuna na **/dh/** ni ghuna, MYW yametokea kuwa na kosa la kitahajia. Mbali na kukosa kutofautisha sauti hizi za menoni, kulikuwa na kosa lililoonyesha kwamba baadhi ya wanafunzi wanashindwa kutofautisha vikwamizwa ghuna /**dh**/ na /**z**/ vinavyotofautishwa na mahali pa kutamkia; ya kwanza ni ya meno na ya pili ni ya ufizi. Katika 22a, kwa kukosa kutofautisha vikwamizwa /**dh**/ na /**z**/ kitenzi katika tungo hii kimeleta maana ambayo haikulengwa na mtungaji. Kwa yakini, lengo lilikuwa kuonyesha kuwa walitembelea nchi ya Kenya na neno sahihi ni '**zuru**'.

Katika tungo 8a, mwanafunzi ametumia kizuiwakwamizwa sighuna /**ch**/ katika umbo '**asiyekuchua**' badala ya /**j**/ ambayo ni ghuna na kwa njia hii akapotosha maana iliyodhamiriwa. Kitenzi '**chua**' kinamaanisha 'sugua sehemu ya mwili kwa dawa ili kupunguza uvimbe'. Kitenzi kilicho na maana ya kuwa na habari ni '**jua**'. Kwa kupachika herufi hizi katika tungo hiyo kuna maana inayodokezwa ila ni kwamba, kwa vile hii ni methali, jinsi tulivyotaja hapo juu, ni lazima iandikwe kwa mujibu wa Wahenga. Kosa la kutotofautisha **/dh/** na /**th**/ katika 8a, limejitokeza katika 15a KF (kama inavyodhihirika katika sehemu 4.3.2 kuhusu Kubadilisha Konsonanti) ambapo /**th**/ imetumiwa mahali pa /**dh**/ na limenukuliwa kutoka kitabu cha kiada. Bila shaka, kosa kutoka MYW katika 8a ni athari kutoka kwa VVK.

Mfano mwingine wa kosa la kubadilisha konsonanti ni ule wa **/j/** katika umbo '**chondoni**' ambalo lilifaa kuwa neno '**jandon**i' katika 9a. Ijapokuwa '**chondo**' ni nomino ya Kiswahili sanifu ikiwa na maana tatu yaani, kikapu maalum cha kusafiria,

mnyama wa baharini, na ngoma inayopigwa kuwaita watu kwenda mkutanoni, ni dhahiri kwamba mwanafunzi hakuwa na maana hizi katika tungo yake.

Nia yake ilikuwa nahau isemayo '**kutia jandoni'** inayomaanisha vijana wa kiume kupashwa tohara kama hatua inayoadhimisha kuingia katika utu uzima. Asili ya kosa la kutumia '**chondoni**' badala ya **'jandoni'** ni mazoea yanayotokana na kurejelea neno '**jandoni**' kama '**kiondoni**'. Wengi wa wakazi wa eneo letu la utafiti husema '**watoto wameenda kiondoni'** wakiwa na maana ya '**watoto kwenda jandoni'.**

Kutokana na habari alizo nazo mtafiti, akiwa ni mzaliwa na mkazi wa eneo la utafiti, neno '**jandoni**' lilivurugwa na kuwa '**kiondo**' ambalo ni jina linalotumiwa na jamii ya Wakikuyu, ambao ni miongoni mwa jamii zinazoishi katika eneo la utafiti, kumaanisha kikapu na lilionekana kuwa na ukuruba na neno '**jando**'. '**Chondo**' sasa ni matokeo ya kuvurugwa kwa '**kiondo**' na limejitokeza katika MYW. Matumizi ya lugha miongoni mwa wanajamii yanadhihirika yakiwa na athari katika MYW. Wanafunzi wameiga makosa kutokana na matumizi maarufu yenye makosa katika jamii wanayoishi. Hii ni hali changamano mno kwa sababu kwanza neno linatoka katika jamii moja kisha linavurugwa na wanajamii ambao wanaliingiza katika lugha nyingine na kubadilisha matamshi yake na kulipa maana nyingine iliyo tofauti sana.

Katika 10a, badala ya kutumia /**f**/ katika neno la pili (alifuka), alitumia /**v**/ ambayo imepotosha maana ya tungo yenyewe. Kuna kitenzi '**vuka**' katika Kiswahili na miongoni mwa maana zake mbalimbali, hakuna inayolenga '**moshi kutoka mahali**'. Hivi ndivyo hali ilivyo katika 11a, ambapo /**f**/ imetumiwa mahali panapofaa /**v**/. Inatokea kwa sadfa kuwa kitenzi '**fua**' kinaweza kuhusishwa na samaki ambapo maana yake ni 'toa magamba katika samaki'. Hata hivyo, kwa kuelewa kwamba mwanafunzi alilenga tendo la kuwatoa samaki kutoka majini kwa kutumia vifaa

mbalimbali vya uvuvi, basi ni dhahiri kwamba mwanafunzi huyu anatatizwa na kutofautisha vikwamizwa vya menoni kwa kuzingatia ughuna.

Udhaifu huo umeonekana pia kupitia 12a, anapoandika ‘**funja**’ badala ya ‘**vunja**’; neno linalomaanisha ‘tenganisha kitu katika vipande kwa kukipinda’. Tofauti na ilivyo katika tungo mbili za kwanza yaani 10a na 11a, katika tungo hii, umbo linalotokea yaani, ‘**funja**’ sio neno katika Kiswahili sanifu. Makosa haya yanatokana na kuingiliwa kwa Kiswahili na lugha za kwanza za wanafunzi. Kubadilisha sauti ghuna na kuweka sighuna ni athari ya moja kwa moja kutoka katika Kibukusu (ambayo ni lugha ya kwanza ya mtafiti) ambacho sauti zake nyingi ni sighuna. Katika Kibukusu sauti ghuna hutokea katika mazingira yaliyo na nazali mwanzoni vinginevyo, sauti huwa ni sighuna. Hii ndiyo maana /**v**/ katika ‘**vunja**’ itakuwa /**f**/ lakini **/j**/ haitabadilika kuwa /**ch**/ katika neno ‘**vunja**’ katika matamshi ya Wabukusu kwani /**j**/ katika neno hilo imetanguliwa na nazali ya ufizi /**n**/.

Neno ‘**inchi**’ katika 22a limechopekwa irabu ‘**i**’ mwanzoni na maana yake ni aina ya kipimo cha urefu ilhali neno ‘**nchi**’ ndiyo inayodhamiriwa hapa kwa sababu Kenya ni eneo la kijiografia. Katika 45a nomino ‘**jinsi**’ imeandikwa kama ‘**jinzi**’ kwa kubadilisha kikwamizwa sighuna /**s**/ kuwa kikwamizwa ghuna /**z**/. Hili ni kosa lingine linalotokana na kutotofautisha sauti ghuna na sighuna.

Katika sehemu hii tunaona jinsi makosa tofauti tofauti ya kubadilisha herufi yalivyotokea katika MYW; mengi yakiwa na asili yake katika matamshi mabaya. Matamshi haya yalitokana na lugha ya kwanza ya wanafunzi. Baadhi ya makosa yalitokana na matumizi ya lugha katika jamii kwa sababu ya kuchotwa na wanafunzi kutoka kwenye jamii wanayoishi. Kuna makosa mengine katika MYW yanayofanana na yale yaliyotokea katika VVK kama tunavyochambua katika sehemu ifuatayo

(4.3.2). Kwa sababu hii tunaweza kudai kuwa baadhi ya makosa ya wanafunzi ni athari ya moja kwa moja kutoka kwa VVK.

### 4.3.2 Kubadilisha herufi: vitabu vya kiada

Kulikuwa na makosa ya kubadilisha herufi katika vitabu vyote tulivyochunguza. Mifano ifuatayo inaonyesha maneno yaliyobadilishwa herufi katika VVK:

6. a) Kupitia kwa ufahamu, mwanafunzi anafundishwa **jinzi** ya kupanua msamiati wake na hata nyenzo za kujieleza kwa ufasaha. UWK uk.19
15. a) Mataifa yaliyoendelea yamekuwa yakipigania **kuthibiti** nafasi zao kiuchumi na kisiasa. KF uk. 102

Ubadilishaji wa vikwamizwa vya ufizi /**z/** na /**s**/ katika 6a, ni kosa la kubadilisha sauti sighuna na ghuna. Kutumika kwa ‘**jinzi**’ badala ya ‘**jinsi**’ ni kosa la kushangaza kutokea katika kitabu cha mafunzo ya wanafunzi shuleni. Kosa hili linaweza kuhusishwa na utepetevu katika uandishi na uhariri wa kitabu hiki. Si ajabu kwamba kubadilisha /**s**/ kuwa /**z**/ katika neno ‘**jinsi**’. Hili ni kosa lililotokea katika MYW na ni dhahiri kwamba limetokana na athari za VVK.

Katika 15a, kupachikwa kwa kikwamizwa /**th**/ katika neno ‘**thibiti**’ kumeunda neno ambalo lina maana iliyo tofauti sana na ile inayonuiwa na mwandishi. Maana ya ‘**thibiti**’ ni ‘tafuta habari kuhusu jambo fulani.’ Katika tungo iliyopo, matumizi ya neno hili hayawezi kuwa sahihi kwa sababu mataifa ya ulimwengu hayawezi kupigania kutafuta habari fulani kuhusu nafasi zao kiuchumi na kisiasa. Ujumbe unaolengwa hapa ni kusimamia, kutawala au kuweka chini ya mamlaka yao nafasi za kiuchumi na kisiasa. Hii ndiyo maana ya neno ‘**dhibiti**’ ambalo limebadilishwa na kuwa ‘**thibiti**’ kwa sababu ya kukosa kutofautisha /**th**/ na /**dh**/ na kwa njia hii kutokea kwa maana ambayo haina mantiki. Kosa linalohusu kubadilisha sauti za menoni katika 15a linaweza kuwa na chanzo chake kwa waandishi. Huenda hata waandishi

wanatatizika katika matamshi yao ya sauti za menoni au hawana habari kuhusu tofauti ya maana baina ya vitate '**thibiti**' na '**dhibiti**'. Ikiwa wanatatizika katika matamshi yao, kuna uwezekano wa waandishi kama hawa kuwaambukiza wanafunzi udhaifu huu hasa ikichukuliwa kwamba kampuni nyingi za uchapishaji hutumia walimu kama waandishi katika kuandaa VVK. Hatuwezi kupuuza uwezekano kwamba hata miongoni mwa walimu kuna, wasio na habari kuhusu tofauti iliyopo baina ya '**thibiti**' na '**dhibiti**'. Kadhalika, huenda kosa hili likawa linatokana na wapiga chapa ambao wanakabiliwa na tatizo la kutotofautisha /**th**/ na /**dh**/ hivi kwamba wakati wa kupiga chapa wanafanya makosa. Aidha, wahariri wa vitabu hivi wanafaa kubebeshwa lawama kwa sababu miongoni mwa majukumu yao ni kusafisha miswada ya mwisho kabla ya kuiwasilishwa kwa uchapishaji na kwa sababu wahariri wanastahiki kuwa na ujuzi katika lugha, ni wao waliostahiki kutambua makosa haya na kuyarekebisha. Vinginevyo, inaweza kudaiwa kwamba VVK havihaririwi kwa uangalifu.

Makosa mengine ya kubadilisha herufi yaliathiri irabu na yalihusu maneno ambayo tahajia yake ilikuwa na kasoro kwa sababu ya kuweka irabu isiyofaa katika mazingira yaliyostahili irabu nyingine tofauti. Makosa yote yaliyoorodheshwa katika sehemu hii yalitokea katika VVK. Ifuatayo ndiyo orodha ya makosa yenyewe:

28. a) …maana ya **tahijia** ya msamiati wa lugha hiyo husawazisha matumizi ya lugha. UWK uk. 130
10. a) Katika kidato cha kwanza tulieleza maana ya maktaba kuwa mahali ambapo pana vitabu, majarida, nakala mbalimbali na **magezeti** ya kusoma. KK uk. 37
2. a) **vivumushi.** KF uk. 7
29. a) Walilima mashamba ya wazazi wao, kuenda mtoni na hata **katafuta** kuni kwa pamoja. KF uk. 164
47. a) Kama mwandalizi wa shughuli za **uchuguzi** wa viongozi wa Baraza la Wanafunzi shuleni mwenu, andika ratiba itakayofuatwa katika sherehe ya **kuapiza** viongozi wapya wa Baraza la Wanafunzi. KF uk. 213

Maumbo yaliyosheheni makosa katika tungo hizi ni haya: ‘**tahijia**’, ‘**magezeti**’, ‘**vivumushi**’, ‘**katafuta**’ na ‘**uchuguzi**’. Kila moja kati ya maumbo haya lina kosa moja la kubadilisha irabu. Katika kila neno, irabu zilizobadilishwa ni /**i**/ badala ya /**a**/, /**e**/ badala ya /**a**/, /**u**/ badala ya /**i**/, /**a**/ badala ya /**u**/, na /**u**/ badala ya /**a**/. Kwa utaratibu huu, maneno haya yanastahiki kuandikwa ifuatavyo: ‘**tahajia**’, ‘**magazeti**’, **‘vivumishi’**, ‘**kutafuta**’ na ‘**uchaguzi**’. Neno ‘**kuapiza**’ katika 47a, lina kosa ambalo limeshughulikiwa katika 5.6.2 chini ya Mnyambuliko Usioafikiana na Muktadha.

Kwa muhtasari makosa ya kubadilisha herufi katika VVK ni matokeo ya wahusika kuwa na utepetevu katika kazi yao. Wahusika hawa wanaweza kuwa waandishi wenyewe au wapiga chapa na waratibu wa rasimu za vitabu vyenyewe. Makosa yote yanayohusu kubadilisha irabu yangesahihishwa kama rasimu za mwisho za vitabu zingehaririwa kwa uangalifu.

**4.4 Kutenganisha neno: maandishi ya wanafunzi**

Katika sehemu hii tumechunguza makosa yaliyotokana na kugawanya neno moja na kuwa vipande viwili katika kuandika. Makosa ya kutenganisha neno yalitokea katika vitenzi pekee kama inavyodhihirishwa katika tungo zifuatazo:

23. a) **Tulipo fika** nyumbani tulivua nguo.
24. a) **Tulipo zuru** mbuga ya Maasai Mara, **tuli waona** wanyama.
25. a) Tusifurahi **kuwa dhuru** wenzetu.
26. a) Maji **yali jaa** hadi pomoni.
27. a) Ni jukumu la aila ya mama mtoto kumpa jina lakini hayo yatakuwa **yame kiuka** desturi ya jamii.

Katika tungo hizi (23a hadi 27a), makosa ya kutenganisha neno yamedhihirisha udhaifu wa wanafunzi wa kutotambua kwamba viambishi vinavyowakilisha mtendaji, wakati na urejeshi ni lazima viambatanishwe katika mzizi wa kitenzi na kutamkwa na kuandikwa kama neno moja. Tukitazama 2a, na 24a, **‘tu-li-**’ na ‘**-po-**’ ni viambishi vinavyowakilisha watendaji katika nafsi ya kwanza wingi, wakati uliopita na kirejeshi

‘**o**’. Viambishi hivi vinastahiki kuwa sehemu ya neno kwa kuambishwa katika vitenzi vyao yaani ‘**fika**’ na ‘**zuru**’. Katika 25a, kiambishi ‘**ku-**’ kinachosimamia kitendo na ‘**-wa-**’ kinachosimamia wingi wa nafsi ya tatu vimetenganishwa kutoka kwenye mzizi huru ‘**dhuru**’. Katika ‘**tuli waona**’ (sehemu ya pili ya 24a), kiambishi cha nafsi ya mtendaji na kile cha wakati uliopita vimetenganishwa kutoka katika sehemu nyingine za neno. Aidha, katika 26a, kiambishi kiwakilishi cha ngeli ya YA - YA na kile cha wakati uliopita ‘**li**’, vimetenganishwa kutoka kitenzi ‘**jaa**’. Kwenye 27a, kiambishi kiwakilishi cha wingi katika ngeli ya LI - YA na kile cha hali timilifu ‘**me**’, vimetenganishwa kutoka kwenye kitenzi ‘**kiuka**’.

Kiswahili ni lugha iliyo na uambishaji mwingi kwa sababu dhana mbalimbali kama mtendaji, wakati au hali na mtendewa zinaweza kuwakilishwa ndani ya kitenzi ambacho kinaonyesha kauli na mambo haya yote yakaandikwa kuwa neno moja. Baadhi ya wanafunzi wanaoshindwa kutambua viwakilishi vya dhana hizi hugawa maneno ya aina hii na kuyaandika kama zaidi ya neno moja bila kutambua kwamba ni neno moja. Kama tunavyoona makosa ya kutenganisha neno yalitokea katika vitenzi pekee kwa sababu vitenzi huwa na uambishwaji mwingi katika Kiswahili. Aidha, makosa haya yalitokea katika MYW pekee wala hayakuweko kwenye VVK. Hii inathibitisha ya kwamba wanafunzi waliofanya makosa haya wana udhaifu wa kuelewa dhana za viambishi na mofimu.

Makosa ya kutenganisha neno ni ishara ya udhaifu wa wanafunzi katika kuelewa kanuni ya uambishaji kwenye vitenzi halisi vya Kiswahili sanifu. Wanafunzi wana upungufu katika kuelewa kikamilifu dhima za viambishi awali. Bila shaka huku ni kuathiriwa na kanuni ya vitenzi vishirikishi ambavyo mizizi yake huwa imejificha ndani ya viambishi kama tunavyoonyesha katika tungo zifuatazo:

1. Mgeni **ana** kitabu.
2. Shati **lililo** kubwa linaoshwa.
3. Kitabu **kilicho** bora kiliteuliwa.

Kwenye tungo 1, 2 na 3, vitenzi vishirikishi vimeandikwa katika mkolezo. Katika kuendeleza vitenzi hivi haifai kuviunganisha na maneno yanayovifuatia katika tungo kwa sababu maneno hayo ama ni vivumishi au nomino wala sio vitenzi. Katika 23a na 24a makosa ya uendelezaji yameathirika moja kwa moja na kanuni inayohusu vitenzi vishirikishi. Vitenzi vyote katika tungo hizo ni halisi na kwa hivyo katika kuviendeleza, haifai kuvitenganisha viambishi na mashina ya vitenzi vyake. Kadhalika, upungufu huu unaweza kuhusishwa na kuathiriwa na Lugha ya Kiingereza ambayo haina utajiri wa uambishwaji jinsi Kiswahili kilivyo. Kwa sababu Kiingereza ni lugha nyingine ya lazima wanayosoma wanafunzi katika shule za upili, kuna uwezekano kwamba wanafunzi wamehamisha kanuni za Kiingereza na kuziingiza katika Kiswahili na kusababisha makosa ya kutenganisha neno katika MYW katika uendelezaji wake.

### 4.5 Kuunganisha Maneno

Sehemu hii inachunguza makosa ya kuchukua maneno mawili na kuyaendeleza kama neno moja. Hali hii inatokana na kushindwa kutambua aina tofauti za maneno katika lugha. Neno ni kipashio chenye maana na kwa hivyo maneno mawili au zaidi yakiunganishwa katika maandishi huzua mtafaruku katika maana na hivyo kutatiza mawasiliano.

#### 4.5.1 Kuunganisha maneno: maandishi ya wanafunzi

Ifuatayo ni mifano ya makosa ya kuunganisha aina mbili za maneno katika MYW:

28. a) Mtoto **watatu** huitwa upande wa mama.
29. a) **Inauwezo** kwamba mama mjamzito anaweza akitembea barabarani.

30. a) Katika mila na desturi ya jamii za Kiafrika, kila mtu **anajina** lake.
31. a) Nyanya zao walioaga dunia au **waliohai**.
32. a) Mama **anahoma** ya mafua.
33. a) Hii ni **kwasababu** nilizaliwa wakati wa kulima.
34. a) Jina lile linatumika kwa mtoto **wakiume** na Nasimiyu kwa mtoto **wakike**.

Katika 28a, kihusishi '**wa**' kimeunganishwa na nomino '**tatu**' na kuunda neno ambalo, ingawa ni la Kiswahili sanifu yaani, '**watatu**', katika muktadha wa tungo hii, linasababisha kosa la kisarufi. Mtoto akiwa mmoja, namna inavyoashiriwa katika tungo hii, hatuwezi kutumia '**watatu**' kama kivumishi cha idadi. Umbo linalotokea kwa kuunganisha kihusishi '**kwa**' na nomino '**sababu**' katika 33a, sio neno la Kiswahili sanifu. Katika 34a kuna kosa la kuunganisha kihusishi na vielezi vinavyorejelea jinsia ambapo kihusishi '**wa**' kimeunganishwa na vielezi vinavyoeleza jinsia ya '**kiume**' na '**kike**' na kuunda maaumbo '**wakike**' na '**wakiume**' ambayo sio maneno ya Kiswahili sanifu.

Kuna kuunganishwa kwa kitenzi kisaidizi '**na**' na maneno mengine. Kwa mujibu wa Wesana-Chomi E, (2003), '**na**'ni kitenzi maalum. Chomi anadai kuwa '**na**' hiki ni kitenzi ambacho hakichukui kiambishi cha wakati ila huchukua viambishi vingine kama vya ngeli na vya wakati. Katika 29a, 30a, na 32a hicho kitenzi '**na**' kinachoonyesha hali isiyodhihirisha wakati maalum, kimeunganishwa na nomino '**uwezo**','**jina**' na '**homa**'.

Yamkini wanafunzi walifanya makosa haya kwa kufikiria kwamba, kwa sababu viambishi awali '**i**' (katika '**ina**') na '**a**' (katika '**ana**') katika kila tungo vinawakilisha ngeli ya kiima, basi '**na**' ni kiwakilishi cha wakati uliopo. Hata hivyo, haileweki ni kwa namna gani waliamua kuunganisha na nomino kwa sababu ni vitenzi pekee vinavyochukua viambishi vya kiima na wakati wala sio nomino. Katika 31a, kuna

mfano wa kuunganisha kitenzi kishirikishi ‘**-wa**’ (ambacho kinajidhihirisha kwa maumbo mbalimbali kama vile ‘**ni**’, ‘**li’**, ‘**si**’ na ‘**yu**’) na kivumishi (kitenzi ‘**-wa**’ kinajidhihirisha kama ‘**li**’ katika umbo lililokolezwa katika ‘**waliohai**’), ambapo kimeunganishwa na kivumishi cha sifa ‘**hai**’. Uwezekano upo kwamba mwanafunzi anaona ‘**walio**’ kama viambishi na hatambui kuwa kuna kitenzi kilichobadilisha umbo ndani ya neno hili. Hili ni kosa ambalo linatokana na mwanafunzi kujumlisha kanuni za uambishaji katika Kiswahili ambapo katika muktadha maalum, ‘**walio**’ ni viambishi. Huku ni kujumlisha kanuni. Katika kiwango cha kidato cha pili, mwanafunzi anatarajiwa awe na ufahamu wa kutofautisha maneno haya. Makosa ya utenganishaji wa aina hii hayawezi kuhusishwa na matamshi mabaya kama yalivyo makosa mengineyo ya kitahajia bali ni ukosefu wa umilisi wa kutosha wa dhana nzima kuhusu maumbo ya maneno.

### 4.5.2 Kuunganisha maneno: vitabu vya kiada

Katika VVK tuligundua visa vitatu vya kuunganisha maneno na vyote vilipatikana katika kitabu kimoja. Zifuatazo ni tungo zilizokuwa na uunganishaji katika KF:

25.a) Haki za binadamu **zakulinda** maisha zina mipaka gani? KF uk. 147

32. a) Mawazo yote yanayotolewa yaegemee **nani** lazima yaingiliane na kifungu hicho. KF uk. 171

44. a) Wapaze sauti dereva akikiuka **sheriaau** polisi wanapokosa kuwashtaki wenye hatia. KF uk. 206

Katika tungo hizi, ‘**zakulinda**’, ‘**nani**’ na ‘**sheriau**’ ni maumbo yanayotokana na kuunganisha maneno mawilimawili ambayo ni tofauti. Katika 25a, kihusishi cha –a unganifu, ‘**za**’ katika wingi wa ngeli ya I - ZI, kimeunganishwa na kitendo ‘**kulinda**’. Matokeo yake ni umbo ambalo si neno la Kiswahili. Katika 32a, kiunganishi ‘**na**’ kimeambishwa kwenye kitenzi kishirikishi ‘**ni**’ na kuunda umbo ambalo limesadifu kuwa neno la Kiswahili. Licha ya kuwa neno la Kiswahili, linaposomeka katika tungo

hiyo namna lilivyo, tungo hiyo haileti maana kwa sababu ya kukosa kukamilika kisarufi. Tunaona kihusishi kikiunganishwa na kitenzi, kiunganishi na kitenzi na nomino na kiunganishi katika mifano hiyo mitatu. Haya ni makosa yaliyo wazi sana na yanaweza kutambuliwa na wanafunzi. Kwa kuwa makosa haya yalitokea katika MYW tunaweza kusema kuwa yanaashiria kwamba uhariri wa kazi za kiada una dosari. Upo uwezekano kwamba wakaguzi hupitia vitabu kijuujuu na kukosa kutambua makosa yanayodhihirika kwa urahisi kama kuunganisha maneno ilhali makosa yanayomhitaji mtu kusoma kwa makini yanakosa kuonekana kwao madhali hawana dhati ya kufanya kazi yao.

### 4.6 Hitimisho

Katika sura hii tumechambua aina mbalimbali za makosa ya kitahajia katika MYW na VVK kwa mujibu wa lengo la kwanza la utafiti. Kwa kuongozwa na mihimili mikuu ya Nadharia ya Uchanganuzi Makosa, tumeyachambua makosa ya kitahajia kwa kuzingatia namna mbalimbali za kujidhihirisha kwake. Tumefafanua asili mbalimbali za makosa haya. Baadhi ya makosa yalitokana na athari za lugha za kwanza za wanafunzi wa jamiimseto. Zile sauti ambazo hazikuwepo katika lugha ya kwanza ya wanafunzi ziliwatatiza wanafunzi katika kuyaandika maneno yaliyozihusisha na hivyo matokeo yake yakawa ni makosa ya kitahajia. Kadhalika, tumedhihirisha kwamba baadhi ya makosa katika MYW yalifanana na yale yaliyokuwa katika VVK. Jambo hili linaashiria kwamba wanafunzi waliiga makosa mengine kutoka katika vitabu wanavyosoma. Nayo makosa ya kitahajia katika vitabu vya kiada (ambayo ni machapisho rasmi), yanaashiria ukosefu wa umakinifu miongoni mwa waandishi, wapiga chapa na wahariri. Mradi wanafunzi hufanya makosa wanapojifunza, haifai wao kukumbana na makosa katika machapisho rasmi kwa sababu wanaweza kuchanganyikiwa au kuiga hali ya kutojali wanapoandika na hapo kuruhusu makosa

kufanyika. Jambo hili litakuwa na athari hasi kwa matokeo ya wanafunzi katika Kiswahili.

Katika Sura ya Tano tumechambua aina mbalimbali za makosa ya kisarufi jinsi tulivyogundua katika uchunguzi wetu kwa kuzingatia lengo letu la pili la utafiti. Tuligundua kwamba kitengo hiki kilikuwa na aina nyingi za makosa kuliko kitengo cha tahajia. Aidha, makosa yenyewe yalikuwa ni ya aina mbalimbali. Labda kuwepo kwa wingi wa makosa katika kitengo cha sarufi kunatokana na sababu kwamba sarufi ni uwanja mpana katika lugha na hujumuisha mambo mengi. Kama tulivyofanya katika sura hii, tumejaribu kuchambua mambo mbalimbali yanayosababisha kuwepo kwa makosa ya kisarufi katika MYW na VVK.

# SURA YA TANO

# UHAKIKI WA MAKOSA YA KISARUFI

## 5.0 Utangulizi

Katika sura hii tumechambua aina mbalimbali za makosa yanayohusu sarufi na ambayo yalidhihirika katika MYW na VVK tulivyochunguza kwa mujibu wa lengo letu la pili la utafiti. Kihore na wenzake (2008) wakiwanukuu Pei na Gaynor (1969), wanaeleza sarufi kuwa sayansi ya muundo wa lugha pamoja na sheria na kanuni za matumizi yake ambayo hukubalika kwa watumiaji wake. Maelezo haya ni ya kijumla kwa sababu yanajumuisha vipengele vyote vya lugha yaani, fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki. Katika *Kamusi ya Kiswahili Sanifu Toleo la 3*, sarufi inaelezwa kuwa kanuni za lugha zinazotumika ili kupata ufasaha katika lugha. Katika muktadha wa utafiti wetu tumechukulia makosa ya kisarufi kuwa ni yale yanayohusiana na sintaksia, semantiki na baadhi ya vipengele vya kimofolojia. Makosa haya yalichambuliwa chini ya vitengo vifuatavyo: Kudondosha Maneno, Kuchopeka Maneno, Makosa katika Upatanisho wa Kisarufi, Minyambuliko Isiyokubalika, na Makosa katika Uambishaji.

## 5.1 Kudondosha Maneno: Maandishi ya Wanafunzi

Katika sehemu hii, tumechunguza makosa yaliyotokea katika tungo kutokana na mwandishi kuacha neno moja au zaidi katika tungo. Maneno yaliyoachwa katika tungo husika yaliathiri usahihi wa kisarufi wa tungo hiyo. Aina za maneno yaliyodondoshwa ni Vihusishi, Vitenzi na Nomino. Tungo zifuatazo kwenye MYW zina mifano ya makosa ya kudondosha aina mbalimbali za maneno:

2. a) Mwaka huu **haujakuwa** ^ njaa.
4. a) Ninaandika ^ kalamu nyekundu.
6. a) Pia watoto hupewa majina kulingana ^ kazi.
7. a) Katika kabila langu kuna mambo ambayo ^ yazingatiwe kabla ya kuwapa watoto majina.

8. a) Wanyama walioko ^ eneo hilo kwa mfano ndovu …
9. a) Hakikisha ^ insha yako ina aya.
52. a) Watoto hawa wanaishi ^ njaa sana.
58. a) ^ Kabila langu kila mtu humpa mtoto jina.

Katika 2a, (kosa la kisarufi linalotokea katika neno **haujakuwa** limejadiliwa baadaye) kitenzi kishirikishi kikamilifu '**haujakuwa**' kimefuatwa na nomino '**njaa**' ambayo inafaa kutanguliwa na kihusishi kwa sababu mwaka hauwezi kuwa '**njaa**'. Kwa hivyo, ili tungo hii itimize usahihi wa kisarufi, inabidi vihusishi '**na**' au '**wenye**' vitumiwe mara tu baada ya kitenzi kishirikishi '**haujawa**'. Kwa hiyo, usahihi wake utakuwa '…haujawa **na** njaa.' au '… haujawa **wenye** njaa.' Kosa la aina hii limefanywa katika 52a ambapo kitenzi kishirikishi '**wanaishi**' kimekosa kuhusishwa. Tendo la **'kulingana**' linavyodhihirika katika 6a, linastahili kuandamana na kihusishi '**na**'. Kudondoshwa kwa '**na**' kumeifanya tungo hii kuwa na upungufu wa kisarufi. Katika 4a, kihusishi kinachoashiria utumizi '**kwa**', kimeachwa. Ujumbe unaolengwa katika tungo hiyo ni kalamu kutumiwa kufanya tendo la kuandika wala sio kalamu yenyewe kuandikwa namna inavyodokezwa katika tungo hiyo. Ni sharti katika muktadha huu tendo la kuandika lihusishwe na kalamu. Matumizi ya kitenzi '**yazingatiwe**' katika 7a, yanadokeza masharti ya namna fulani. Kwa hivyo, inabidi kuwe na kihusishi cha masharti kabla ya kitenzi '**yazingatiwe**'. Kihusishi hicho ni '**sharti**'. Vinginevyo, ili tungo hiyo iwe sahihi bila kihusishi hicho basi kitenzi hicho kinafaa kuwa '**yanazingatiwa'** ambapo tungo ingekuwa:

> Katika kabila langu mambo ambayo **yanazingatiwa** kabla ya kuwapa watoto majina…'

Kihusishi cha mahali '**katika'** chenye maana ya '**ndani ya'**, kimedondoshwa katika 8a na 58a. Katika tungo ya kwanza, kitenzi kielekezi '**wanaishi**' hakiwezi kuteua nomino '**eneo'** katika uelekezi wake. Ni sharti kuwe na kihusishi cha mahali baina ya

kitenzi '**wanaishi**' na nomino '**eneo**'. Kwenye 58a, kihusishi '**katika**' kilipaswa kuwa mwanzoni mwa sentensi ili kuleta dhana ya '**ndani ya**' kuhusu nomino '**kabila**'.

Tungo hizi zote zilitokana na wanafunzi wenye asili ya Kibukusu. Hii ni lugha ya kwanza ya mtafiti na kwa hivyo anaielewa vizuri. Karibu tungo hizi zote zinatokana na tafsiri ya moja kwa moja kutoka Kibukusu, moja ya lahaja kubwa za Kiluhya. Baadhi ya tungo hizo zikitafsiriwa kwa Kibukusu zitakuwa:

2a*) Kumwika kuno sekwabhele enjala tawe.*
*6a) Lundi bhabhana bhabhatyukha khulondekhana kimilimo.*
*7a) Mu kholo yange khuli ne kamakhuwa ko khulonda ne bhatyukhe bhabhana kamasina.*
*17a) Chisang'i chili ebhweneyi enga chinjofu.*
*52a) Bhabhana bhano bhamenya enjala.*
*58a) Ekholo yange bhuli omundu awa omwana lisina*.

Hii ni tafsiri ya kimaongezi ya baadhi ya tungo hizo na tunaona jinsi makosa yalivyotokea kwa sababu ya kufanya tafsiri sisisi kutoka lugha ya asili ya wanafunzi. Hata hivyo ni muhimu kukumbuka kwamba pamoja na kufanywa kwa tafsiri sisisi hadi Kibukusu, tungo hizi katika Kibukusu zina makosa ya kisarufi yanayohusu kudondoshwa kwa maneno. Aghalabu, tungo hizi zinakubalika katika matamshi lakini katika uandishi haziruhusiwi kama tungo sanifu za Kibukusu. Tunaweza kufikia uamuzi kwamba lugha ya maongezi imesababisha kuwepo kwa makosa ya kisarufi katika MYW.

**5.2 Kudondosha Maneno: Vitabu vya kiada**

Katika VVK kulikuwa na matukio mengi ya kudondosha maneno katika tungo. Vitabu vyote vitatu vilikuwa na visa vya kudondosha maneno kama inavyoonyeshwa hapa:

17. a) Njia nyingine ya kufufulia na kuendeleza uchumi wa nchi ni kuteremsha viwango vya riba inayolipwa ʌ mashirika ya ukopeshaji nchini. UWK uk. 102

31. a) Sifa nyingine ya sentensi ya Kiswahili ni ^ Kirai-nomino kiima huathiri Virai-vitenzi na Virai-vivumishi kwenye sentensi. UWK uk. 140
9. a) Ni mahali ambapo mtu anaweza kufanya utafiti zaidi kwa ^ vinavyohifadhiwa humo**.** KK uk.37
17. a) Tunashuku kwamba ^ maneno aliyotueleza amepiga chuku. KK uk. 71
20. a) hali kadhalika kutazama vitabu vilivyo katika maktaba bila kwenda huko… KK uk. 105
27. a) kuanza insha kwa utangulizi wenye kuvutia… KK uk. 233
12. a) Waliokuwa ^ pembe za chaki walijua ukweli ulipokuwa. KF uk. 85
13. a) ^ Katiba ya mwaka elfu mbili na kumi, Kiswahili kilipanda hadhi kwani kiliidhinishwa kuwa ni lugha rasmi na ya kitaifa nchini. KF uk. 95
39. a) Katika shairi UKIMWI, kwa mfano, dhamira ya msanii ni kuonya ^ UKIMWI huua na kila juhudi sasa zinafanywa katika vita dhidi ya yake. KF uk. 204
43. a) Kunayo haja ya kuwajibika ili kuchangia ^ kupunguza ajali za barabarani. KF uk.206
50. a) Kunao pia waliong'ang'ana na magunia ya mahindi. Mimi nilikuwa wa kuyanyanyua na kuyapandisha juu ya chanja ya basi njiani maana utingo walibakia ^ kituo cha mabasi. KF uk. 225

Katika 31a UWK na 39a KF kuna makosa ya kudondosha vitenzi. Kitenzi ni neno linalobeba ujumbe katika tungo yenye uamilifu wa sentensi. Tungo yoyote ni sharti iwe na kitenzi ndipo iafiki sifa za sentensi. Aidha, kuwepo kwa kitenzi si ithibati kwamba tungo husika imekamilika kimaana. Mathalani, panapokuwa na kitenzi kikuu yaani kile kitenzi kinachobeba maana kuu katika sentensi, ni lazima pawe na kitenzi kisaidizi kinachofanya kazi ya kusaidia kitenzi kikuu ili kukamilisha sentensi.

Hebu tutathmini mifano miwili hii ya tungo ambazo, japo zina vitenzi vikuu, hazitimizi sifa ya sentensi kwa sababu ya kukosekana kwa vitenzi visaidizi:

1. Jangwa **kuenea** kwa kasi
2. Wanariadha **wakishiriki** mashindano

Licha ya kuwepo kwa vitenzi, tungo hizi sio sentensi. Kila moja inafaa itanguliwe na kitenzi kingine; hiki ni kitenzi kisaidizi na ndicho kinachohitajika ili kukamilisha kila

tungo. Ili kukamilisha tungo hizi ni sharti kuweka vitenzi visaidizi kwa kila tungo kupitia kwa maneno yaliyokolezwa wino kama ilivyo hapa:

1. Jangwa **lizuiwe** kuenea kwa kasi.
2. Wanariadha **watakuwa** wakishiriki mashindano.

Makosa ya kudondosha vitenzi yalidhihirika zaidi katika vitenzi visaidizi. Hii ina maana kwamba vingi kati ya vitenzi vilivyodondoshwa ni visaidizi.

Usahihi wa kisarufi katika 31a UWK na 39a KF unakosekana kwa sababu ya kudondoshwa kwa kitenzi '**kuwa**'. Katika 31a, kitenzi kishirikishi kipungufu '**ni**' kinastahiki kufuatwa na kitenzi kishirikishi kikamilifu '**kuwa**' au '**kwamba**' ili kauli hii ikamilike. Katika 39a KF kukosekana kwa kitenzi '**kuwa**' kunafanya maana inayodhihirika iwe kwamba UKIMWI ndio unaoonywa ilhali mwandishi alinuia kuonyesha kuwa watu ndio wanaoonywa. Tendo la kusoma halidhihirishi ni nini kinachoathiriwa nalo kwa mujibu wa 9a KK. Kwa hivyo sentensi inakosa kutambua shamirisho kipozi. Shamirisho kipozi ndiyo inayopokea athari za moja kwa moja za tendo katika sentensi. Katika mfano huu, vinavyofaa kusomwa vimerejelewa tu kama '**vinavyohifadhiwa humo**' bila kutajwa waziwazi. Ilitarajiwa kwamba nomino kama '**vitabu**' ingewekwa baada ya neno '**kusoma**' ili tungo iwe na ukamilifu kimaana. Kwa kufanya hivyo tungo hii itasomeka:

> Ni mahali ambapo mtu anaweza kufanya utafiti zaidi kwa kusoma **vitabu** vinavyohifadhiwa humo.

Mpangilio wa maneno katika 17a KF umevurugwa kwa sababu nahau '**amepiga chuku**' ndiyo inayofaa kuja kabla ya '**maneno aliyotueleza'**. Huu ndio mpangilio sahihi wa maneno katika tungo hii:

> Tunashuku kwamba amepiga chuku **katika** maneno aliyotueleza.

Mbali na kurekebisha mpangilio wa maneno katika tungo hii, tumeongezea kihusishi '**katika**'.

Ikumbukwe kwamba, kwa sababu 20a KK na 27a KK sio sentensi zilizokamilika, tumeziandika bila kuzingatia kanuni za uakifishaji wa sentensi kuhusu kuanza kwa herufi kubwa na kuweka nukta mwisho wake. Tumetumia alama za dukuduku baada ya kila tungo kuonyesha kwamba tungo hiyo haijakamilika. Katika tungo zote mbili nomino za kitenzijina zimetumiwa kama kiima na kwa hivyo kukamilika kwa kila moja kulitarajiwa kuwekewa vitenzi vinavyoonyesha matokeo ya kila kitendo. Katika 20a, tunahitaji kuambiwa matokeo ya kutazama vitabu vilivyo maktabani ni nini. Kuna udondoshaji wa kihusishi katika 12a KF. Kihusishi hicho ni ‘**katika**’ na kinastahili kiwekwe baina ya kitenzi kishirikishi ‘**waliokuwa**’ na nomino ya mahali, ‘**pembe za chaki**’. Ni lazima kihusishi cha mahali ‘**katika**’ kitumiwe ili tungo hii ikubalike kisarufi. Aidha, katika 13a KF, kukosekana kwa kihusishi ‘**katika**’ mwanzoni mwa tungo hiyo kunaifanya isikamilike kama sentensi ya Kiswahili. Mradi kupandishwa kwa hadhi ya Kiswahili kunahusishwa na katiba ya mwaka wa elfu mbili na kumi, basi ni lazima kihusishi ‘**katika**’ kiwepo. Kosa hili linafanana na lile lililo katika 17a KF ambapo kihusishi hicho ‘**katika**’ kimedondoshwa.

Katika 17a UWK, riba inastahiki kulipwa ‘**kwa**’ au ‘**na**’. Katika muktadha huu, maana inayodhamiriwa ni kwamba wakopeshaji wanapata mikopo kutoka kwa mashirika ya kukopesha na wanaporejesha pesa walizokopeshwa, wanalipa faida kwa mashirika hayo. Kwa hivyo, ni sharti kuweka kihusishi ‘**kwa**’ ilmuradi riba ‘**hailipwi mashirika’** bali ‘hulipwa **kwa** mashirika’. ‘**Lipa**’ ni kitenzi kielekezi ambacho uteuzi wake wa kijalizo hutegemea aina ya nomino kwa sababu kile kinachotolewa ili kulipa kinanufaisha na aghalabu ni ile nomino yenye sifa ya kibinadamu inayoweza kunufaika. Riba hulipwa mtu lakini hulipwa **kwa** ‘**mashirika**’ kwa ajili mashirika hayana uwezo wa kunufaika kwa sababu hayana sifa ya kibinadamu. Katika 43a KF kuna matumizi ya vitenzi vikuu viwili yaani, **‘kuchangia’** na ‘**kupunguza**’. Usahihi

wa tungo hii bila kuwepo kwa kihusishi ungewezekana endapo nomino '**upunguzaji**' ingeundwa kutokana na kitenzi '**kupunguza'** ambapo tungo yenyewe ingesomeka:

> Kunayo haja ya kuwajibika ili kuchangia **upunguzaji** wa ajali za barabarani.

Vinginevyo, ili neno '**kupunguzwa**' lidumu, ni lazima kuweka kihusishi '**katika**' ili tungo isomeke:

> Kunayo haja ya kuwajibika ili kuchangia **katika** kupunguza ajali za barabarani

Kwenye 50a KF, kihusishi cha mahali '**katika**' kimedondoshwa ilmuradi 'utingo walibaki **katika** kituo cha basi' wala sio 'walibaki kituo cha basi'. Dhana inayojitokeza katika 50a ni kwamba utingo ni kituo cha basi ilhali maana inayodhamiriwa ni kwamba utingo hawakuondoka kituoni mwa basi. Kwa hivyo, ni lazima kuweka kihusishi cha mahali baada ya kitenzi '**walibaki**'.

Katika sehemu hii tumeona kwamba kadiri wanafunzi walivyofanya makosa ya kudondosha vihusishi katika maandishi, ndivyo makosa yayo hayo yalivyotokea katika VVK. Kuwepo kwa makosa haya katika VVK hakuwezi kuwa kazi ya wapiga chapa namna baadhi ya makosa ya kitahajia yalivyo bali, ni waandishi wanaostahiki kuwajibikia kasoro hizi. Kadhalika, tunaweza kudai kwamba waandishi wanafanya makosa haya kwa sababu ya mazoea ya watu katika matamshi ambapo wengi hupuuza vihusishi katika matamshi yao kiasi cha baadhi ya watu kudhani kwamba hayo ni matamshi sahihi. Kutumia lugha namna hii huweza kuzoeleka kiasi cha watu (hata wasomi wa lugha) kudhani kwamba haya ni matumizi sahihi.

### 5.3 Kuchopeka Maneno: maandishi ya wanafunzi

Katika sehemu hii, tumechunguza makosa yaliyotokana na kuongeza neno katika tungo na kuathiri usahihi wa kisarufi wa tungo husika. Hali zilizodhihirika kutokana

na uchopekaji huo zilitokana na kuweka neno lisilostahili muktadha huo, kujirudia kimaana na kukosa usare wa kuwasilisha wazo fulani. Vihusishi ni aina mojawapo ya maneno yaliyochopekwa katika tungo na ndivyo vilivyochopekwa zaidi ya aina nyingine za maneno. Makosa mengi ya kuchopeka vihusishi yalihusu '**kwa**' na '**na**'. Tungo zifuatazo zinaonyesha mifano ya makosa ya aina hii:

3. a) Huzingatia ukoo hasa **kwa** ukoo wa baba.
12. a) Watoto hupewa jina **kwa** mambo mengi ambayo hutendeka.
13. a) Tafadhali naomba uniazime **na** kalamu.
19. a) Ni lazima majina yao ya kwanza kuanzia **na** herufi …

Katika 3a, neno '**kwa**' limetumika kuonyesha uhusiano katika '**ukoo**' jambo ambalo sio sahihi. Kwa vile neno '**ukoo**' limeshatajwa tayari, neno linalofaa kuingia mahali palipo na neno '**ukoo**' la pili ni '**ule**' ambalo litakuwa linawakilisha nomino hiyo. Tungo hiyo itakuwa:

Huzingatia ukoo hasa **ule** wa baba.

Katika 12a, kihusishi '**kwa**' kimechopekwa na kupewa jukumu la kuunganisha nomino '**jina**' na '**mambo**'. Kwa sababu lengo lililo hapa ni kuunganisha wala si kuhusisha, basi kiunganishi kilichostahili kuwa hapa ni '**kulingana na'**.

Katika 4a, kihusishi '**kwa**' kimefuatwa na kielezi cha namna yaani, **'haraka**' na kuvuruga usahihi wa tungo yenyewe. Kihusishi hiki hakipaswi kutumiwa pamoja na vielezi vya namna. Mbali na '**haraka**', mifano mingine ya vielezi vya namna ambavyo havistahili kutumiwa pamoja na kihusishi '**kwa**' ni **sana, pole, polepole, sawasawa, taratibu**, **hobelahobela, ovyo** na **sare**. Tukitazama mifano ya sentensi zifuatazo zilizotumia kihusishi '**kwa**' kikiandamana na baadhi ya vielezi hivi tunatambua kwamba zina makosa:

1. Mzigo ulibebwa kwa **polepole.**
2. Mzigo ulibebwa kwa **sawasawa**.
3. Mzigo ulibebwa kwa **taratibu.**
4. Mzigo ulibebwa kwa **ovyo.**

Kwa hivyo, ‘**kwa**’ haistahiki kupachikwa kabla ya vielezi vya namna katika tungo za Kiswahili. Kwa kuzingatia maelezo haya, usahihi wa tungo hizo ni:

1. Mzigo ulibebwa polepole.
2. Mzigo ulibebwa sawasawa.
3. Mzigo ulibebwa taratibu.
4. Mzigo ulibebwa ovyo.

Katika 13a na 19a, vitenzi vielekezi ‘**uniazime**’ na ‘**kuanzia**’ vinafaa kuteua nomino au vielezi ili kukamilisha maana katika sentensi badala ya kuteua kihusishi kama ilivyo kwenye tungo hizo. Nomino ‘**kalamu**’ inayokuja baada ya kihusishi ‘**na**’ ilitosha kuipa tungo hiyo ukamilifu wa kisarufi sawasawa na nomino ‘**herufi**’ ilivyostahili kukamilisha 19a bila kihusishi ‘**na**’. Kwa hivyo, kuchopeka ‘**na**’ baada ya kitenzi kielekezi ni kosa la kisarufi. Kwa kudondosha kihusishi ‘**na**’ kwenye 19a, tungo hii itakuwa:

Tafadhali naomba uniazime kalamu.

Huku kutokubali kufuatwa na kihusishi ‘**na**’ katika tungo ni kawaida kwa vitenzi vingi vielekezi kama vile **idhinisha, changa, amini, nunua, ponza, kata, sukuma, amrisha** na kadhalika. Kijalizo mwafaka cha vitenzi vielekezi huwa ni nomino au vielezi vya namna. Hebu tutazame mifano ya matumizi ya vitenzi vielekezi na vielezi vya namna:

1. Katiba **imeidhinishwa kihalali**.
2. **Tulichanga kikarimu** ili kusaidia yatima.
3. Akifika sasa **atatuamrisha kijeshi** tuondoke.

Katika mifano mitatu iliyo hapo juu, maneno yaliyokolezwa yamedhihirisha ukubaliano kati ya vitenzi vielekezi na vielezi vya namna mfanano vinavyokuja baada ya kila kitenzi. Kutokea kwa makosa haya kunaonyesha ukosefu wa ujuzi miongoni mwa wanafunzi kuhusu jinsi maneno yanavyofaa kuteuana katika sentensi. Ni wazi kwamba uelewa wao kuhusu miundo ya Kirai Kihusishi katika sintaksia ya Kiswahili ni hafifu. Aidha, kutokea kwa makosa haya kunaashiria kwamba wanafunzi hawa

wana upungufu wa kuelewa aina mbalimbali za kategoria ndogo za maneno kati ya kategoria nane kuu za maneno (Nomino, Vitenzi, Vivumishi, Vielezi, Viwakilishi, Vihusishi, Viunganishi na Vihisishi). Wanafunzi wanapoelewa aina ndogo chini ya kila aina katika aina nane za maneno, watajua sheria za kutumiwa kwake na vighairi vinavyofaa kumakinikiwa. Kwa mfano, baada ya kuelewa aina za vihusishi watajua matumizi ya kila aina huku wakitambua aina ambazo hazikubali kuingia katika muktadha fulani. Huu ni mfano wa vighairi lugha ambavyo mwanafunzi anastahiki kumakinikia ili ajiepushe na kufanya makosa katika matumizi ya maneno. Kwa vile makosa yaliyotokea katika MYW yana ukuruba na yale yaliyo katika VVK, tunaweza kuhoji kwamba vitabu vya mafunzo vimeathiri uelewaji wa kanuni za kisintaksia miongoni mwa wanafunzi ambapo waliiga makosa waliyoona katika VVK.

Makosa ya kuchopeka maneno vilevile yalitokea katika maneno ambayo hatukuyaweka katika kategoria za kimuundo bali tuliyachukulia kama msamiati wa kawaida tukizingatia maana za kikamusi za maneno yanayorejelewa. Huu tuliuona kama udhaifu wa kutambua msamiati stahilifu zaidi katika muktadha unaohusika. Tuliongozwa na dhana kwamba maneno yaliyochopekwa hayakustahiki kuwekwa hapo bali ni mengine ambayo tumeyapendekeza. Hapa chini tunaorodhesha tungo ambazo zilichopekwa msamiati ambao haukustahiki katika MYW.

11. a) Mtoto wake wa kwanza akiwa **kijana** anaitwa Wanjohi.
15. a) Kuna jina kama Wefula maanake alipenda **kutoatoa** nguo.
16. a) Watoto **hutajwa** baada ya shujaa aliyefanya mambo mbalimbali.
18. a) Mbwa alibweka **mchana kucha**.
20. a) Njaa **imetanda** nchini.
56. a) Hasa **mila** yangu huwa wanafanya sherehe kubwa sana.

Katika 11a, kutokana na mazoea au kutojua, msamiati wa kijumla ‘**kijana**’ umetumiwa kumaanisha mtoto wa kiume badala ya ‘**mvulana**’ na visawe vyake kama ‘**mvuli**’ na ‘**ghulamu**’. Mwanafunzi huyu hana habari kwamba neno ‘**kijana**’

linatumika kwa jinsia za kiume na kike. Katika 15a, matumizi ya neno ‘**kutoatoa**’ ili kuleta dhana ya kuondoa mavazi mwilini hayasadifu. Msamiati mwafaka hapa ni ‘**kuvuavua nguo**’. Aidha, kutumia neno ‘**hutajwa**’ katika 16a, badala ya ‘**hupewa**’ ili kurejelea utaratibu wa kuwapa watoto majina, ni ishara ya kutokuwa na hazina ya msamiati inayotosha. Wakati wa kusisitiza kielezi ‘**mchana**’, ili kumaanisha mchana wote, tunastahili kuweka neno ‘**kutwa**’ wala sio ‘**kucha**’ kama ilivyo katika 18a. Hata hivyo, kwa sababu neno ‘**kucha**’ lilikuwepo katika zoezi ili wanafunzi walitumie katika kutunga sentensi itakayoeleza maana ya ‘**kucha**’, basi kosa la kuteua msamiati usiofaa linatokea katika neno ‘**mchana**’. Badala ya kuandika ‘**usiku kucha’**, mwanafunzi anarejelea ‘mchana **kucha**’. Kadhalika, katika 20a, msamiati ‘**tanda**’ umehusishwa na njaa badala ya kutumia ‘**enea**’ ilmuradi njaa **haitandi** bali **huenea**. Hatimaye, katika 56a, ‘**mila**’ haifanyi sherehe bali ni kundi la watu linalohusiana kwa mujibu wa mila au tamaduni zao linalofanya sherehe. Kundi hili huitwa ‘**jamii**’ au ‘**kabila**’. Kwa hivyo, uteuzi wa neno ‘**mila**’ ni kosa katika tungo hii.

Utafiti wetu pia ulitambua kwamba kulikuwa na matumizi ya maneno ambayo yalisababisha kujirudia katika tungo. Kujirudia katika maelezo hudhihirisha udhaifu wa kisarufi kwa mhusika. Makosa haya yalidhihirika kwa njia ya kurudia ama neno fulani au kisawe cha neno lililotumika katika tungo. Urudiaji huu ulisababisha uradidi katika tungo. Baadhi ya makosa ya urudiaji yalitokana na kutumia aina moja ya maneno katika tungo. Tungo zifuatazo kutoka katika MYW zinadhihirisha makosa ya namna hii:

14. a) Ni sehemu **ya yenye** ukumbi.
41. a) **Pia** watoto wanaozaliwa wakati wa mvua **pia wao** wana majina yao kama vile Nyambura.
59. a) Katika aya ya pili nilizungumzia **kuhusu** usafi.

Katika 14a, maneno ‘**ya**’ na ‘**yenye**’ yanarejelea dhana moja ya kuhusisha nomino ‘**sehemu**’ kumilikiwa na ukumbi. Ili kuondoa urudiaji huu, ni lazima kimojawapo cha vihusishi hivyo kidondoshwe. Kwa hivyo, tungo hiyo inastahili iwe:

> Ni sehemu **ya** ukumbi.
> au,
> Ni sehemu **kwenye** ukumbi.

Katika 41a, kiunganishi cha kujumuisha **‘pia’** kimetumiwa mara mbili na kusababisha kosa la kujirudia katika maelezo. Vilevile, urudiaji mwingine unaodhihirika hapa ni wa kutumia kiwakilishi cha nafsi ya tatu wingi ‘**wao**’. Kiwakilishi hakipaswi kutumiwa pamoja na nomino kinayowakilisha katika tungo moja kwa sababu viwakilishi huchukua nafasi ya nomino katika sentensi. Katika tungo hii, nomino ‘**watoto**’ imetajwa na wakati huo huo, kiwakilishi chake ‘**wao**’ kutajwa. Matokeo yake ni kwamba kumekuwa na kujirudia kunakoathiri usahihi wa tungo hii. Ili kurekebisha kosa la urudiaji katika tungo hii, ni lazima kudondosha kiunganishi ‘**pia**’ cha pili na kiwakilishi cha nafsi ‘**wao**’ ambapo tungo itakuwa:

41. Pia watoto wanaozaliwa wakati wa mvua wana majina yao kama vile Nyambura.

Urudiaji unaotokea katika 59a, unasababishwa na kutumiwa kwa kihusishi ‘**kuhusu**’ (chenye maana ya ‘**juu ya’**) katika tungo yenye kitenzi kilichonyambuliwa katika kauli ya kutendea. Kauli ya kutendea huleta dhana ya ‘**juu ya’** na kwa hivyo kitenzi ‘**nilizungumzia**’ kimewakilisha dhana hiyo tayari. Kuchopeka kihusishi ‘**kuhusu**’ baada ya kitenzi katika kauli ya kutendea kunasababisha urudiaji. Kwa kudondosha neno ‘**kuhusu**’ tungo itasomeka:

> Katika aya ya pili **nilizungumzia** usafi.

Aidha, kama tunataka kudumisha kihusishi ‘**kuhusu**’ ni lazima kitenzi kiwe katika kauli ya kutenda ambapo tungo itasomeka hivi:

Katika aya ya pili **nilizungumza kuhusu** usafi.

Kwa jumla katika sehemu hii tumedhihirisha jinsi urudiaji katika tungo ulivyosababisha makosa katika tungo. Wanafunzi ama walirudia visawe au maneno yale yale hasa nomino au viwakilishi vyake na matokeo yakawa ni kujirudia katika tungo. Katika kisa kimoja tumeonyesha namna kauli tendea inavyoweza kusababisha urudiaji inapotumika pamoja na kihusishi '**kuhusu**'. Urudiaji ni kosa ambalo linatokana na uhaba wa msamiati au udhaifu wa kujieleza kwa upande wa mwanafunzi. Kuwa na hazina kubwa ya msamiati ni kielelezo katika uandishi wa insha. Wanafunzi wenye msamiati haba hukosa kujieleza kwa njia bunifu katika utungaji wa insha.

### 5.4 Kuchopeka Maneno: vitabu vya kiada

Makosa ya kuchopeka maneno yalipatikana katika vitabu vyote vitatu. Katika tungo zifuatazo tumeonyesha mifano tuliyopata katika kila kitabu kwa kukoleza maneno ambayo yamechopekwa:

19. a) Andika njia **za** mbalimbali za kukwamua uchumi wa nchi ya Kenya. UWK uk. 103
24. a) **Kwa** wakati huu ambapo idadi ya watu duniani inazidi kuongezeka na mataifa yamekuwa na ongezeko la viwanda…UWK uk. 112
34. a) Maana ya muhtasari ni kuandika **kwa** kifupi. UWK uk.169
11. a) Hadithi hizi zilipokezwa kwa njia ya **kiunenaji** kutoka kizazi kimoja hadi kingine. KK uk. 43
14. a) Kisha mkutano ulijadili **kwa** kirefu hoja baada ya hoja mpaka wanachama wakaafikiana. KK uk. 51
4. a) Dharura inapotokea, ijulikane ni aina gani ya dharura na ishughulikiwe **kwa** haraka. KF uk.68
9. a) Husimulia mambo **kwa** kirefu ikitumia lugha ya mjazo na yenye mchanganyiko wa visa… KF uk.79
16. a) Ni kitu **cha** adhimu kwa kila mtu, awe mtoto, kijana au mzee. KF uk.112
36. a) Watu wanafyeka **uwanjani**. KF uk. 202

Katika 19a UWK na 16a KF kuna kosa la kuchopeka kihusishi cha -a unganifu. Tungo hizi zinakiuka kanuni ya sarufi ya Kiswahili kuhusu miundo ya Virai Husishi

(KH). Kirai Husishi hakina muundo wa Kihusishi na Kivumishi (HV) yaani, kihusishi hakistahili kufuatwa na kivumishi katika sentensi ya Kiswahili sanifu. Kirai Husishi kina miundo ya Kihusishi na Nomino au Kiwakilishi chake (HN/W) na Kihusishi na Kielezi (HE). Kihusishi cha - a unganifu hufuatwa na Nomino, Kiwakilishi, Kitenzijina au Kielezi cha mahali katika sentensi na kinapochukuliwa pamoja na hiyo nomino, kiwakilishi au kielezi cha mahali, kinakuwa na uamilifu wa kuvumisha nomino iliyotajwa mwanzo. Hebu tutazame mifano hii:

1. Ni kitambaa **cha watoto**. (H+N)
2. Ni kitambaa **cha wote**. (H+W)
3. Ni kitambaa **cha kuchezea**. (H+T)
4. Ni kitambaa **cha sebuleni**. (H+E)

Mifano yote minne inaonyesha namna kihusishi cha -a unganifu kinavyoteua nomino, kiwakilishi, kitenzijina na kielezi cha mahali kama inavyofuatana katika orodha yaani namba 1, 2, 3 na 4 na tungo zote ni sahihi kisarufi. Katika kila tungo, maneno yaliyokolezwa yana uamilifu wa kuvumisha nomino '**kitambaa**' kwa sababu yanatusaidia kukitofautisha kitambaa kinachorejelewa hapa na vitambaa vingine. Maneno yaliyokolezwa katika kila tungo yanaonyesha miundo mbalimbali ya Kirai Husishi na miundo yenyewe imeandikwa ndani ya mabano mwishoni mwa kila tungo. Katika 19a UWK, kihusishi '**za**' kimeambatanishwa na kivumishi '**mbalimbali**'. Aidha, hali ni hiyo hiyo katika 16a KF ambapo kihusishi '**cha**' kimeambatanishwa na kivumishi '**adimu**'. Hii inakaidi sarufi ya Kiswahili sanifu kuhusu miundo ya Kirai Husishi.

Katika 24a UWK, kihusishi '**kwa**' kimetumiwa mwanzoni mwa tungo. Kihusishi hiki hakipaswi kuwa katika tungo hii. Kuwepo kwake ndiko kunakoifanya tungo yenyewe kuwa na makosa. Katika 9a KF, 14a KK na 34a UWK, kuna kuchopekwa kwa kihusishi ambako kumevuruga sarufi ya tungo hizo. Kihusishi '**kwa**' hakistahili

kutumiwa pamoja na kielezi cha mfanano kama ilivyo katika tungo hizi ambapo vielezi '**kirefu**' na '**kifupi**' vimetumiwa vikifuata kihusishi '**kwa**'. Katika muundo wa kirai kihusishi kilicho na '**kwa**' kama kihusishi, neno linalofuatia lazima liwe nomino. Kwa kuzingatia maelezo haya maneno **'kirefu'** na **'kifupi'** sharti yageuzwe kuwa nomino '**urefu**' na '**ufupi**' ili virai visomeke '**kwa urefu'** na '**kwa ufupi'**. Kama sivyo basi, vihusishi hivyo vidondoshwe moja kwa moja na tungo zitakuwa sahihi. Kwa kuzingatia hoja hizi, 34a UWK itasahihishwa kwa namna mbili zifuatazo:

1. Maana ya muhtasari ni kuandika **kifupi**.
2. Maana ya muhtasari ni kuandika **kwa ufupi**

Katika 4a KF, kihusishi '**kwa**' kimefuatwa na kielezi cha namna yaani, **'haraka**' na kuvuruga usahihi wa tungo yenyewe. Kihusishi hiki hakipaswi kutumiwa pamoja na vielezi vya namna (Hii ni hali ambayo tuliijadili chini ya 5:3: *Kuchopeka Maneno: MYW*).

Katika 11a KK na 36a KF kuna makosa mengine ya kuchopeka vielezi mahali kulikofaa nomino. Katika 11a KK, matumizi ya kielezi cha mfanano '**kiunenaji**' sio sahihi. Kwa hivyo neno linalostahili kuwa hapo ni nomino ili tungo hii isomeke:

Hadithi hizi zilipokezwa kwa njia ya unenaji…

Kielezi '**kiunenaji**' kinabadilishwa ili kuwa nomino '**unenaji**'. Katika 36a KF, kuna mahali kulikochopekwa kielezi cha mahali ilhali kulistahili nomino. Katika tungo hii, kitendo cha '**kufyeka**' hakifai kuathiri kielezi cha mahali. Kwa sababu '**kufyeka**' ni kitenzi kielekezi, ni lazima kiteue nomino au kielezi cha namna. Kwa maelezo haya sasa, tungo hii inastahili kutoa maana ya kufyeka nomino '**uwanja**' au kielezi cha namna, '**polepole**'. Kadhalika, kwa vile '**fyeka**' ni kitenzi kielekezi, kinakubali kuteua vielezi vya namna. Mifano ifuatayo inathibitisha teuzi kubalifu zinayochukuana na kitenzi '**fyeka**':

1. Watu wanafyeka **taratibu**.
2. Watu wanafyeka **haraka**.
3. Watu wanafyeka **kistadi**.
4. Watu wanafyeka **kigoigoi**.

Katika 1 na 2, tumeonyesha mifano ya vielezi vya namna vinakubali kuandamana na kitenzi kielekezi '**fyeka**'. Mifano ya vielezi vya mfanano vikiafikiana na kitenzi hiki inadhihirika katika 3 na 4 hapo juu.

Jambo linalodhihirika kuhusu uchopekaji wa maneno katika VVK ni kwamba waandishi wa vitabu hivi walipungukiwa katika kutekeleza kanuni za sintaksia ya Kiswahili. Kanuni za kisintaksia huongoza jinsi maneno yanavyoteuana na kufuatana katika tungo sahihi katika lugha. Vivyo hivyo, Kiswahili kina kanuni zake za kisintaksia ambazo hazijazingatiwa katika tungo tulizonukuu. Makosa ya kuchopeka msamiati usiofaa yalijitokeza katika tungo zifuatazo kutoka vitabuni:

22. a) Yaani **zinasimamia** kuwa tendo lililokosa kufanyika bado lina nafasi ya kuweza kufanyika. KF uk.143
45. a) **Usibebe** vyakula maktabani. KF uk.211
53. a) Kinachowapa nguvu watetezi wa Kiswahili ni imani kuwa Kiswahili ni lugha maarufu sasa hivi, kulingana na **tarakimu**, inazungumzwa na watu takribani milioni mia mbili. KF uk.227

Katika 22a KF, matumizi ya neno '**zinasimamia'** sio mwafaka. Neno linalofaa kutumiwa ni **'zinamaanisha'.** Katika 45a KF, tendo la kufikisha kitu mahali, katika muktadha huu '**vyakula**' kufikishwa maktabani, halistahili kurejelewa kwa neno '**usibebe**' jinsi ilivyo katika tungo hii. Kwa sababu kihusishi cha mahali '**hadi**' au '**mpaka**' hakijatumiwa katika tungo hii, neno mwafaka lilikuwa '**usipeleke**'. Kwa kuzingatia maelezo haya, 45a KF inafaa kuwa:

**Usipeleke** vyakula maktabani.

Kwa mtazamo wa haraka, neno '**tarakimu**' katika 53a KF, linaweza kudhaniwa kwamba linastahili kutumiwa. Katika *Kamusi ya Kiswahili Sanifu Toleo la 4* na

*Kamusi ya Karne ya 21*, neno '**tarakimu**' linaelezwa kuwa alama ya hisabati inayoandikwa kuonyesha idadi tu. Hata hivyo, maana inayolengwa na mwandishi hapa ni kwamba hii idadi inayotolewa imetoa taarifa za kiuchanganuzi. Kwa sababu hiyo basi, msamiati mwafaka unaoelezea dhana hii ni '**takwimu**'. Kamusi hizi zote zinakubaliana kwamba **takwimu** ni nambari zinazoelezea na kulinganisha ukweli kuhusu matukio ya mambo. Ukweli unaodokezwa katika tungo hiyo ni kwamba Kiswahili ni lugha maarufu na kwa vile umaarufu haupimwi kwa kuchunguza kitu kimoja au upande mmoja pekee bali kwa kuweka kila upande kwenye mizani baada ya kupata habari kupitia kwa tarakimu, '**takwimu**' ndio msamiati sahihi zaidi. Kama ilivyokuwa katika MYW, kulikuwa na uchopekaji uliosababisha urudiaji katika VVK inavyoonyeshwa katika tungo zifuatazo:

2. a) Silabi funge **ni** ile inayoishia **na** konsonanti ilhali silabi huru **ni** ile inayoishia **na** irabu/vokali. UWK uk.3
4. a) Kila mmoja aliulizwa kwenye hojaji **kama ikiwa** angepelekwa kuishi peke yake kwenye kisiwa na kuruhusiwa kubeba kitu kimoja tu, angebeba nini? UWK uk. 8
33. a) Kitabu hiki kinazungumzia **juu ya** maisha ya **mwanake** mmoja kwa jina Siti Binti Saad, ambaye alizaliwa kijijini Fumba huko Zanzibar. KF uk.191
34. a) Alizaliwa katika **hali ya umaskini** KF. uk.191
42. a) Kwa kuendesha gari kwa mwendo usiodhibitika dereva anaweza kusababisha ajali **kwa kitendo hicho**. KF uk. 205

Ujirudiaji upo katika 2a UWK ambapo kihusishi '**na**' kimetumiwa pamoja na kitenzi katika kauli ya kutendea yaani, '**inayoishia**'. Kadhalika, kurudiwa kwa maneno kunadhihirika kupitia kihusishi '**na**', nomino '**silabi**' na kitenzi kishirikishi '**ni**'. Kila neno limetumiwa mara mbili katika tungo hii. Kwa hivyo, kuna urudiaji wa aina mbili yaani, kurudia dhana na maneno. Katika kuisahihisha tungo hii ni lazima kudondosha maneno yaliyorudiwa ambapo tungo inayopatikana inakuwa:

> Silabi funge ni ile inayoisha kwa konsonanti ilhali huru huisha irabu/vokali.

Urudiaji ulio katika 4a unatokana na matumizi ya viunganishi ambavyo vina maana sawa. '**Kama**' na **'ikiwa**' ni viunganishi vya kulinganisha. Vikitumiwa pamoja katika tungo vinasababisha urudufu. Ni lazima kuchagua kimojawapo baina ya viunganishi hivi na tungo itakuwa sahihi kisarufi. Kauli ya kutendea ilitumiwa pamoja na maelezo ya kihusishi '**kuhusu**' katika 33a KF. Kauli tendea huleta maana ya '**juu ya**' kama tulivyoeleza chini ya *5.3 Kuchopeka Maneno:* MYW. Urudiaji unaotokea katika 42a KF, unasababishwa na kuchopeka maneno yaliyokolezwa wino. '**Kuendesha**' ndicho '**kitendo**' kinachorejelewa katika tungo hii na katika tungo maneno yote mawili (kuendesha na kitendo) yametumiwa. Maneno hayo yote yaliyokolezwa yanafaa kudondoshwa ili kuondoa urudiaji katika sentensi husika.

Njia moja ya kuunda nomino za Kiswahili ni kuweka viambishi katika mzizi. Hali hii ya kuunda nomino tunaweza kuirejelea kama unominishaji. Kiambishi awali '**u**-' ni kimoja kati ya viambishi vya unominishaji. Nomino zinazoundwa kwa njia hii huwa na maana ya '**hali ya**'. Kwa mfano, nomino '**upole**' itaelezwa kama '**hali ya kuwa mpole'**. Katika 34 KF, maneno '**hali ya'** yamefuatwa na nomino '**umaskin**i' na kusababisha urudiaji. Madhali umaskini ni hali tayari, haifai kutumia '**hali ya'** palipo na nomino inayoanza kwa kiambishi '**u-**'. Kwa kuzingatia mjadala huu, tungo hiyo inastahili kuwa:

Alizaliwa katika umaskini.
au,
Alizaliwa katika hali maskini.

Katika VVK tuligundua makosa mengine ya kuchopeka maneno yaliyoathiri usare katika tungo husika. Makosa kama haya hayatambuliki kwa urahisi kwa sababu maneno yanayotumiwa na mwandishi huwa yanakaribiana sana. Hata hivyo, tazamo la makini linadhihirisha hitilafu zinazokuwa katika tungo za aina hii kwa sababu ya

kutumiwa kwa maneno yasiyoambatana. Makosa haya yanatokea katika tungo zifuatazo:

> 28. a) Utafiti huo umefika hatua ambayo miche na mizizi ya mimea ya G.M.O ina uwezo wa kuondoa na kuvunja makali ya madini yenye sumu katika maji na **ardhini** kwa ujumla. KK uk.239
> 21. a) Kwa hivyo iwapo kitendo cha kwanza hakitatokea basi **tendo** la pili **halitatendeka**. KF uk. 143

Katika 28a KK, kiunganishi cha kujumuisha kimetumiwa baina ya maneno '**maji**' na '**ardhini**' ambapo '**maji**' ni nomino ilhali **'ardhini'** ni kielezi cha mahali. Huku kutumia kiunganishi baina ya aina mbili tofauti za maneno yaani, nomino na kielezi sio sahihi. Aidha, kitendo cha kutumia nomino '**maji**' kabla ya kutumia kiunganishi kisha kufuatisha kielezi, kinasababisha ukosefu wa usare katika uandishi. Kwa hivyo ili kuleta usare huu, ni budi kugeuza hayo maneno mawili yawe katika kategoria moja kiuamilifu. Namna mbili zote ndizo hizi:

> Utafiti huo umefika hatua ambayo miche na mizizi ya mimea ya G.M.O ina uwezo wa kuondoa na kuvunja makali ya madini yenye sumu katika **maji na ardhi** kwa ujumla.
>
> au,
>
> Utafiti huo umefika hatua ambayo miche na mizizi ya mimea ya G.M.O ina uwezo wa kuondoa na kuvunja makali ya madini yenye sumu **majini na ardhini** kwa ujumla.

Katika tungo zote mbili, usare umeafikiwa baada ya nomino na nomino, na kielezi na kielezi kutumiwa. Katika 21a KF, matumizi ya maneno **'kitendo'** na '**tendo**' yamesababisha ukosefu wa usare. Kama tulivyotaja mwanzoni, hitilafu katika tungo hii imefichama mno. Vilevile matumizi ya vitenzi '**hakitatokea**' na '**halitatendeka**' katika tungo moja kurejelea hali zinazofanana yanasababibisha mkanganyo. Kuna uwezekano wa hitilafu hizi kukosa kuonekana mara moja kwa sababu ingawa '**kitendo**' na '**tendo**' ni maneno yenye maana sawa lakini yanapotumiwa katika tungo moja yanaleta hitilafu namna ambavyo '**hakitatokea**' na '**halitatendeka**' yanavyoleta hitilafu. Mwandishi alistahili kuteua mojawapo ili aafikie usare unaohitajika katika

maandishi rasmi. Mathalani, kwa kuamua kudumisha maneno yaliyotajwa kwanza (kitendo na hakitatokea) basi tungo ingekuwa:

> Kwa hivyo iwapo kitendo cha kwanza hakitatokea basi kitendo cha pili hakitatokea.

Makosa mengine ya kuchopeka yalitokea katika vitenzi. Kwa sababu ya kuwa na kosa moja pekee la aina hii katika MYW, tulilishughulikia pamoja na makosa yaliyotokea katika VVK. Katika sehemu hii tulichunguza makosa yaliyosababishwa na kuweka aina ya kitenzi isiyostahili katika tungo na kuathiri sarufi. Inafaa kukumbuka kwamba kitenzi ndicho kiungo muhimu sana katika kutunga sentensi katika lugha yoyote hivi kwamba hakuna sentensi inayoweza kuwa na sifa ya kuitwa sentensi kama haina kitenzi. Kunazo aina sita za vitenzi kwa kuzingatia majukumu yake katika sentensi.

Aina hizi ni: Vitenzi Vishirikishi Vikamilifu, Vitenzi Vishirikishi Vipungufu, Vitenzi Visaidizi, Vitenzi Vikuu, Vitenzi Halisi na Vitenzi Sambamba. Katika uchunguzi wetu, tuligundua kwamba makosa ya kuchopeka yalihusu vitenzi visaidizi na vishirikishi vipungufu. Tulitambua makosa yafuatayo katika kazi tulizohakiki kuhusu uchopekaji wa vitenzi:

11. a) Ada za shule zikawa **ni** shida. KF uk. 85
24. a) Ni lazima shangazi wa mtoto yule **kuja** kumpatia jina. MYW
28. a) Unapoandika mahojiano: (a) majina ya wahusika au vyeo vyao **huandikwa** upande wa kushoto wa karatasi. KF uk. 163
51. a) Lakini hata kama uliyatimiza haya, **waliweza kusingizia** kuwa gari lina makosa kama ya magurudumu yaliyochakaa au taa zisizofanya kazi. KF uk. 226

Kosa lillilo katika 11a KF ni la kutumia vitenzi vishirikishi viwili katika tungo moja. Kuchopeka kitenzi kishirikishi **'ni'** wakati ambapo '**zikawa**' kipo na ni kitenzi kishirikishi, kasoro ya kisarufi imetokea. Vitenzi vishirikishi viwili haviwezi kutokea katika tungo moja bila kudhuru sarufi kwa sababu haiwezekani kuwa na ushirikishi mara mbili katika sentensi moja. Kwa kutumia '**zikawa**' pamoja na kitenzi '**ni**,'

mwandishi anajaribu kulazimisha **‘ni’** kuwa kitenzi kikuu na ‘**zikawa**’ kinageuzwa kuwa kitenzi kisaidizi. Hii sio sahihi kwa sababu ‘**ni**’ ni kitenzi kishirikishi kila wakati. Ili kuwe na usahihi wa tungo hii, ni lazima kudondosha kitenzi ‘**ni**’ na tungo itakuwa:

Ada za shule zikawa shida.

Kwenye 24a MYW, kitenzi kisaidizi ‘**kuja**’ kimetumiwa kwa njia isivyofaa kwa sababu kinaashiria kwamba mwandishi yuko mahali anapotakiwa kwenda shangazi yaani, nafsi ya kwanza. Matumizi ya kiashiria ‘**yule**’ yanaonyesha kwamba mwandishi hayuko mahali ambapo mtoto yuko na kwa hivyo sio sahihi kutumia ‘**kuja**’. Kadhalika, muundo wa kitenzi hiki sio sahihi kwa sababu kulingana na mazingira yake katika sentensi, kimepewa jukumu la kitenzi kisaidizi ilhali ‘**kumpatia**’ ndicho kitenzi kikuu. Muundo sahihi wa kitenzi hicho unastahili kuwa ‘**aje**’ kutokana na kitenzi cha shina la silabi moja ‘**-ja**’. Hata hivyo, mradi tumesema ya kwamba kitenzi hicho hakifai hapo, neno stahilifu ni ‘**aende**’ kutokana na kitenzi ‘**enda**’. Kwa hivyo tungo hii inastahili kuwa:

Ni lazima shangazi ya mtoto yule **aende** kumpa jina.

Katika 28a KF, neno ‘**huandikwa**’ linalotokana na kitenzi ‘**andika**’ limechopekwa katika hoja ya kwanza kwenye orodha ya hoja zinazostahili kuzingatiwa katika kuandika mahojiano (Tungo hii ilinukuliwa kutoka sehemu ya kitabu iliyokuwa inatoa maelezo kuhusu mambo ya kuzingatia wakati wa kuandika mahojiano). Kwa sababu ya kutumiwa kwa neno ‘**unapoandika**’ katika sehemu iliyo kabla ya kuanza kuorodhesha, neno ‘**huandikwa**’ halistahili kutumiwa. Aidha, matumizi ya kiambishi cha hali ya mazoea ‘**hu-**’ yanakinzana na kitenzi kilicho katika sehemu tangulizi kwenye orodha ambacho kina kiambishi cha wakati ‘**-na-**’ na cha hali ‘**-po**’. Ili

kurekebisha makosa haya mawili, ni sharti kitenzi ‘**yawe’** kitumiwe mahali palipo na ‘**huandikwa**’. Tungo hii itasomeka ifuatavyo kama kauli moja:

> Unapoandika mahojiano, majina ya wahusika au vyeo vyao yawe upande wa kushoto wa karatasi.

Katika 51a KF matumizi ya kitenzi ‘**waliweza**’ na ‘**kusingizia**’ sio mwafaka kwa sababu yanaonyesha kwamba juhudi zilitumiwa katika kusingizia. Kusingizia hakuhitaji juhudi zozote kwa hivyo kuchopeka ‘**waliweza**’ kunasababisha makosa katika tungo hii. Makosa ya kutumia vitenzi visaidizi vibaya yamekithiri katika jamii. Kitenzi ‘**weza**’ ndicho kinachotumiwa kwa njia isiyofaa na watumiaji wengi wa Kiswahili. Kitenzi hiki kinapotumiwa huzua wazo la bidii au juhudi kuhitajika katika jambo fulani. Hata hivyo, katika jamii, watu wengi watasikika wakikitumia kurejelea hata shughuli ambayo haihitaji juhudi yoyote. Mifano maarufu inasikika katika vyombo vya habari kama redio na runinga. Hebu tuangalie mifano ifuatayo:

1. Timu ya taifa **iliweza** kufungwa mabao matatu kwa bila.
2. Katika ajali hiyo, watu wawili **waliweza** kufariki.
3. Jambazi hilo **liliweza** kupigwa risasi.

Tungo hizi zote zinaonyesha kutumiwa vibaya kwa kitenzi ‘**weza**’ kwa sababu ya kuhusishwa na matendo ambayo hayahitaji juhudi zozote kwa upande wa wahusika wanaoathiriwa na matendo yenyewe. Si ajabu kwamba katika KF, matumizi yaya haya yasiyostahili ya kitenzi hiki yametokea. Kwa hivyo, matumizi ya lugha katika jamii, na hasa vyombo vya habari, yanaweza kuwaathiri waandishi wa vitabu. Kwa hakika, inapotokea kwamba makosa haya yanadhihirika katika vyombo vya habari vilivyo na usikilizaji wa kimataifa (na kwa hivyo vinaaminika), uwezekano wa makosa hayo kutokea katika miktadha rasmi ni mkubwa.

## 5.5 Upatanisho wa Kisarufi

Upatanisho wa kisarufi unarejelea namna ambavyo viambishi katika vitenzi hukubaliana na ngeli ya nomino inayorejelewa katika aina za maneno katika tungo. Utajiri mkubwa wa upatanisho wa kisarufi hutokea katika vitenzi zaidi ya aina nyingine za maneno katika Kiswahili. Sababu ya kuwepo kwa hali hii, ambapo vitenzi vinadhihirisha upatanisho wa kisarufi katika Kiswahili ni lugha ambishi sana. Mbali na vitenzi kuna baadhi ya vivumishi na vihusishi ambavyo huambishwa kutegemea ngeli ya nomino inayorejelewa. Tuligundua kwamba kulikuwa na makosa mengi ya upatanisho katika vitenzi kuliko vivumishi na vihusishi.

### 5.5.1 Upatanisho katika vitenzi: maandishi ya wanafunzi

Katika MYW, makosa katika upatanisho wa kisarufi kwenye vitenzi yalidhihirika katika ngeli mbalimbali. Ifuatayo ni mifano ya tungo za wanafunzi zilizosheheni makosa ya upatanisho katika vitenzi:

19. a) Ni lazima majina yao ya kwanza kuanza na herufi **yanayofanana**.
27. a) Wanafunzi wenye kucha ndefu **wameyakata**.
29. a) Darasa **iliyojaa** wanafunzi imebomoka.
31. a) Hali ya watoto kupewa jina huwa inalingana na kitendo ambacho kabila **inahusiana** nacho.
32. a) Kitu kingine **ambayo tunayofuatilia** ni ile saa ya kuzaliwa.
44. a) Kibuyu kile kimejaa maji siwezi **kulibeba**.
53. a) Chakula pia **haikuwa**.

Katika 19a, nomino '**herufi**' imewekwa katika ngeli ya LI - YA kwa kuweka kiambishi '**ya**' katika kitenzi '**yanayofanana**'. Kipatanishi cha wingi wa ngeli hii kimetumiwa katika tungo hii licha ya kwamba nomino '**herufi**' haiko katika ngeli hii bali iko katika ngeli ya I - ZI.  Kwa hivyo, badala ya kiambishi '**ya**', mwanafunzi alistahiki kutumia '**zi**'. Aidha, katika neno lilo hilo '**yanayofanana**', kiambishi cha kirejeshi '**o**' kimelazimika kuchukua kiambishi cha ngeli ya LI - YA kutokana na athari za kuiingiza nomino '**herufi**' katika ngeli ya LI - YA. Kwa hivyo, kosa la pili

linasababishwa na lile la kwanza. Katika 27a, nomino ‘**kucha**’ ambayo ni wingi wa ‘**ukucha**’, inastahili kuchukua upatanisho wa ngeli ya U - ZI lakini imewekwa katika ngeli ya LI - YA kwa kutumia kiambishi ‘**ya**’ katika kitenzi ‘**wameyakata**’. Haieleweki ni vipi mwanafunzi alipatanisha nomino na ngeli sahihi katika kivumishi ‘**ndefu**’ na kushindwa kupatanisha kwa usahihi kitenzi ‘**wameyakata**’. Kosa hili linaweza kuhusishwa na kuchanganya dhana mbili tofauti. Kwanza ni kwamba mawazoni mwake alijua nomino ‘**kucha**’ iko katika wingi kisha akaathirika na mazoea ya kuona ‘**makucha**’ kuwa ndio wingi wa nomino hii na ndipo akatumia kiambishi cha ngeli ya LI – YA katika wingi. Aidha, tunaweza kudai kwamba hili ni kosa linalotokana na mwanafunzi kuwa na ufahamu nusu kuhusu ngeli mbalimbali na namna ya kuzipatanisha katika maneno.

Katika 29a na 31a, nomino ‘**darasa**’ na ‘**kabila**’ ziko kwenye ngeli ya LI – YA lakini zimepatanishwa visivyo kwa kuingizwa katika ngeli ya I – ZI. Nomino zote mbili ziko katika hali ya umoja. Katika 29a, vitenzi ‘**iliyojaa**’ na ‘**imebomoka**’ vimeambishwa kipatanishi ‘**i**’ ambacho ni cha ngeli ya I – ZI katika umoja. Nomino inayorejelewa hapa ni ‘**darasa**’ katika umoja (wingi: ‘**madarasa**’). Katika tungo ya mwanafunzi, inadhihirika kwamba kulingana naye, nomino ‘**darasa**’ haibadilishi umbo katika umoja na wingi na ndiyo maana akatumia kiambishi cha ngeli ya I – ZI katika umoja. Katika kitenzi ‘**iliyojaa**’ athari za kupatanisha ngeli kwa njia isiyofaa zinatokea katika kirejeshi ‘**-o**’ ambapo kiambishi awali ‘**yo-**’ kinatumiwa badala ya ‘**-lo**’. Katika 31a, nomino ‘**kabila**’ imehusishwa na ngeli hiyo hiyo ya I – ZI kama ilivyo katika 29a. Katika wingi, nomino hii huambishwa ‘**ma**-’ na kuwa ‘**makabila**’ ambapo katika upatanisho wake, huchukua ngeli ya LI – YA. Kwa mujibu wa tungo ya mwanafunzi, nomino ‘**kabila**’ haibadiliki katika umoja na wingi na ndiyo maana anaihusisha na ngeli ya I – ZI. Makosa ya kupatanisha katika tungo hizi mbili

yanasababishwa na ujumlishaji wa kanuni inayohusu nomino zilizo katika ngeli ya I – ZI kwamba maumbo yake hayabadiliki katika umoja na wingi na pia nyingi kati ya nomino hizi huanza kwa konsonanti. Kutokana na kuelewa kuwa nomino za ngeli ya I – ZI hudumisha maumbo yake katika umoja na wingi, yaani ni mizizi huru, wanafunzi wamejumlisha kanuni hii katika upatanisho wa kisarufi unaohusu nomino za ngeli hii. Makosa ya wanafunzi yamefanana na kosa lifuatalo katika KF:

24. a) Birika **ingali ina** chai. uk.145

Kwa kutambua kwamba kosa la kupatanisha lililo katika 24a KF linafanana na makosa yaliyofanywa na wanafunzi kuhusu ngeli hiyo ya I - ZI, tunaweza pia kutaja VVK kuwa ndiyo sababu nyingine ya makosa ya kupatanisha katika MYW. Katika 32a na 53a, nomino '**kitu**' na '**chakula**' ambazo ziko katika ngeli ya KI – VI zimepatanishwa na ngeli ya I – ZI. Katika 32a, matumizi ya kiambishi cha urejeshi '-**yo**' yanaashiria kuwa, kwa mujibu wa mwanafunzi, nomino '**kitu**' inapatikana katika ngeli ya I – ZI. Ikumbukwe kwamba kiambishi '**-yo**' katika 32a, kimetokea katika kirejeshi '**amba-'** na vilevile katika kitenzi kinachokifuata, yaani '**tunayofuatilia**' na kusababisha kosa la marudio ya urejeshi katika tungo. Mbali na kosa la kujirudia, kuna kosa la kuweka kiambishi cha upatanisho wa kisarufi ambacho hakistahili yaani '**-yo**' badala ya '**-cho**'. Aidha, katika 53a, kunalo kosa la kutokamilika kwa tungo kwa sababu ya kutumiwa kwa kitenzi kishirikishi bila kuongeza neno linaloonyesha kile kinachoshirikishwa na kitenzi chenyewe. Anaposema '**haikuwa**', swali linalozuka ni '**wapi**?' kwa vile ni lazima kukishirikisha kitenzi hiki '**kuwa**' na mahali au hali. Kwa vyovyote vile, makosa yaliyo katika tungo hii ni ya kutotumia kipatanishi cha ngeli ya KI – VI (ndiyo ngeli ya nomino '**chakula**') katika kitenzi '**haikuwa**' na pia kukosa kukamilisha tungo kwa kutoweka kiambishi cha mahali katika kitenzi '**haikuwa**'.

Bila shaka hili ni kosa ambalo limetokana na mazoea ya wanajamii kutumia kitenzi '–**wa**' vibaya. Ni kawaida mtu kusikika akisema '**Hata mimi nilikuwa**' badala ya '**Hata mimi nilikuwepo**'. Huko kudondoshwa kwa kiambishi cha mahali kunaleta hitilafu katika tungo na hali hii ilijitokeza katika MYW. Kwa kuweka viambishi vya ngeli na mahali, kitenzi '**haikuwa**' kinastahili kuwa: '**hakikuweko**', '**hakikuwepo**' au '**hakikuwemo**'. Wingi wa makosa ya upatanisho wa kisarufi ni dhihirisho kwamba wanafunzi wana maarifa duni kuhusu ngeli za nomino au hawajamakinika katika ngeli za Kiswahili.

### 5.5.2 Upatanisho katika vitenzi: vitabu vya kiada

Makosa ya upatanisho katika vitenzi yalidhihirika kwenye tungo zifuatazo kutoka machapisho:

24. a) Birika **ingali ina** chai. KF uk. 145
38. a) Wahusika ndio wanaotumiwa na msanii **kuyawasilisha** ujumbe wake na pia maudhui. KF uk. 204
41. a) Ijapokuwa ajali husemekana kutokuwa na kinga, wingi wa ajali zitokeazo katika barabara zetu **zinaweza** kuzuiwa. KF uk. 205
48. a) Miviga kama vile shughuli za mazishi au harusi huenda **zikafanana** au **zikatofautiana** toka jamii moja hadi nyingine. KF uk. 215

Nomino '**birika**' katika 24a KF imejumuishwa katika ngeli ya I – ZI kama inavyodhihirika katika vitenzi **'ingali'** na '**ina**'. Katika 41a KF, mwandishi ametumia kiambishi cha ngeli ya I – ZI katika wingi kwenye kitenzi '**zinaweza**'; hii ikiwa ni athari kutoka katika kitenzi '**zitokeazo**'. Matumizi ya kiambishi '**zi**' katika '**zitokeazo**' ni sahihi kwa sababu kiambishi hicho kinapatanisha kitenzi na ngeli ya nomino '**ajali**' katika hali ya wingi. Hata hivyo, kwa vile ni '**wingi wa ajali**' unaorejelewa, sio sahihi kusema '…**zinaweza kuzuiwa**'. Maneno '**wingi wa ajali**' yanachukuliwa kama jamii au kundi na kwa hivyo ni ngeli ya nomino '**wingi**', yaani

U - U inayofaa kupatanishwa kwenye kitenzi. Hii ni hali ya kawaida katika nomino za makundi kama inavyoodhihirika katika mifano ifuatayo:

1a) Muungano wa wanariadha **umebuniwa**.
wala sio
b) Muungano wa wanariadha **wamebuniwa**. *
2 a) Unyenyekevu wa mwanafunzi **ulipongezwa**.
wala sio
b) Unyenyekevu wa mwanafunzi **alipongezwa**. *

Katika mifano hii tunaona namna ambavyo kipatanishi cha ngeli ya nomino ya kwanza katika nomino za makundi kinavyotawala. Katika mfano wa 1a, ni ngeli ya nomino '**muungano**' inayotawala upatanisho jinsi ambavyo ngeli ya nomino '**unyenyekevu**' inavyotawala katika 2a. Kwa hivyo, ni makosa kutumia ngeli ya nomino '**wanariadha**' na '**mwanafunzi**' katika kupatanisha sarufi kwenye vitenzi vya sentensi husika. Kwa mantiki haya basi, usahihi wa 41a KF, unakuwa '… **wingi wa ajali…unaweza kuzuiwa**'.

Katika 48a KF, mwandishi alikosea kwa kukiuka kanuni za wingi wa ngeli ya U – I kuhusu nomino '**miviga**'. Vitenzi '**zikafanana**' na '**zikatofautiana**' vimepewa viambishi vya ngeli ya I – ZI katika wingi na kwa njia hii kuijumuisha nomino '**miviga**' katika ngeli hii. Kama ilivyo katika 41a KF, makosa haya ni athari za ngeli ya nomino '**shughuli**' ambayo ilitajwa kama mfano katika sentensi wala sio kiima katika sentensi. Kiima katika sentensi hii ni '**miviga**' kwa hivyo ni ngeli ya nomino hii inayofaa kuongoza upatanisho wa kisarufi katika tungo hii. Makosa ya upatanisho usiokubalika yaliyo katika tungo hizi tatu yanahusu sehemu ya kiima katika kitenzi. Katika 38a KF, kosa la upatanisho usiokubalika kwenye kitenzi limedhihirika kwenye sehemu ya shamirisho ambapo kiwakilishi cha upatanisho wa kisarufi kinarejelea nomino ambayo inatajwa baada ya kitenzi katika tungo. Katika tungo hii, nomino inayorejelewa ni '**ujumbe**' na iko katika umoja wa ngeli ya U – ZI. Katika kitenzi

‘**kuyawasilisha**’, kiambishi ‘-**ya**’ kimetumiwa kuwakilisha nomino **‘ujumbe’** inayotajwa mara tu baada ya kitenzi. Kwa kufanya hivi, nomino ‘**ujumbe**’ imepatanishwa na ngeli ya LI – YA hali ya wingi.

Kama tunavyoona makosa haya katika kupatanisha yametokea katika VVK. Kwa vile ngeli ni msingi wa sarufi ya Kiswahili, makosa yanapotokea katika upatanisho kwenye VVK huwa ni tatizo kubwa. Hili ni suala linalozua shaka kuhusu maandalizi ya VVK. Makosa katika upatanisho yaliathiri ngeli tano (5). Kuna ngeli 12 katika mtaala wa shule na ngeli tano ni karibu nusu ya ngeli zote. Hii ni idadi kubwa sana kwa kuzingatia kwamba VVK ni nyenzo kitabu cha kufunzia. Ngeli hizi ni I – ZI, LI - YA, KI – VI, U – U na PO/KO/MO. Ngeli ya I – ZI iliongoza kwa wingi wa makosa 13, LI – YA matatu (3),kisha kila moja kati ya ngeli zilizobaki ikawa na kosa mojamoja. Kuna haja ya ngeli hizi kushughulikiwa kwa makini na walimu wakati wa kuwafunza wanafunzi. Mitaala ya marudio inastahili kuandaliwa kwa kutilia mkazo ngeli hizi ili kuwawezesha wanafunzi kumakinika na kuepuka makosa katika upatanisho unaohusu ngeli hizi.

### 5.5.3 Upatanisho wa vivumishi, vihusishi na virejeshi: maandishi ya wanafunzi

Kuna uhusiano wa karibu baina ya nomino na vivumishi kwa sababu vivumishi hufanya kazi ya kutofautisha au kutambulisha nomino katika tungo. Kwa sababu nomino ndizo zinapangwa katika makundi yanayoitwa ngeli, kukosa kuelewa ngeli ya nomino inayosababisha au kuathiriwa na tendo katika tungo, husababisha makosa ya kupatanisha kwenye vivumishi. Sio vivumishi vyote hupatanishwa. Tazama mifano ifuatayo: Vivumishi kama vile **kadhaa, bora, nafuu, safi, nadhifu, karimu** na **hodari**, ni mizizi huru na kwa hivyo havichukui viambishi vya ngeli ya nomino husika. Vingi kati ya vivumishi visivyochukua viambishi vya ngeli ni vya asili ya

kigeni hasa Kiarabu. Ni mizizi ya vivumishi vyenye asili ya Kibantu vichukuavyo viambishi vya ngelikama vile, **-ingi, -ote, -chache, -refu, -pole, -erevu, -chafu na – ingine**. Katika MYW, makosa ya upatanisho usiofaa kwenye vivumishi yalihusu vivumishi vya sifa, vivumishi vimilikishi na vivumishi vya idadi kama inavyodhihirika katika tungo zifuatazo:

17. a) Ugali kwa mboga ni **tamu**.
28. a) Kucha za vidole **zake** ni ndefu.
33. a) Madawa **za** kulevya hudhuru afya **zetu.**
50. a) Mvuvi alivua samaki **nyingi**.
51. a) Kwa kila jambo ulilotenda liwe **nzuri** au **mbaya**.

Katika tungo 17a, nomino '**ugali**' iliyo katika ngeli ya U – U, haijapatanishwa kisahihi katika kivumishi '**tamu**'. Tunaporejelea vivumishi vya sifa katika ngeli hii kiambishi '**m**' hutumiwa katika mizizi ya viambishi hivyo ilmuradi mizizi yenyewe iwe inaanza kwa konsonanti. Tukirejelea mifano kama '**mrefu**', '**mfupi**', **'mchache'**, '**mkubwa**' na '**mzito**' tunaona hali halisi. Maadamu mzizi '**tamu**' unaanza kwa konsonanti, basi katika ngeli hii kiambishi '**m**' kilistahili kutumiwa ili neno lisomeke '**mtamu**'. Katika 51a, nomino '**jambo**', inayotambulishwa na vivumishi '**nzuri**' na '**mbaya**', iko katika ngeli ya LI – YA umoja. Katika vivumishi '**nzuri**' na '**mbaya**', mwanafunzi aliweka viambishi '**n**' na '**m**' ambavyo hutumika katika wingi wa ngeli za U – ZI na I – ZI. Kwa kufanya hivi, nomino '**jambo**'imeingizwa katika ngeli hizo. Kulingana na kanuni ya kupatanisha sarufi katika vivumishi vya sifa katika ngeli ya LI – YA umoja, mizizi inayoanza kwa konsonanti na ina silabi mbili au zaidi, haiwekewi viambishi. Mifano ifuatayo inathibitisha ukweli wa kauli hii:

1. Jina **refu** litaandikwa.
2. Jina **fupi** litaandikwa.
3. Jina **geni** litaandikwa.
4. Jina **gumu** litaandikwa.

Kwa mujibu huu basi, katika tungo ya mwanafunzi mizizi '**zuri**' na '**baya**' ilistahili kubaki vivyo hivyo pasipo na kuambishwa. Ingawa tungo 28a na 33a zina makosa

mengine, katika muktadha wa mjadala wetu kwenye sehemu hii, vivumishi ‘**zake**’ na ‘**zetu**’ (ambavyo vinazitambulisha nomino ‘**vidole**’ na ‘**afya**’) havijaambishwa inavyostahili. Nomino ‘**vidole**’ iko katika ngeli ya KI – VI. Kiambishi kinachopatanisha vivumishi na wingi wa nomino katika ngeli hii ni ‘**vy-**’ na kilifaa kuambishwa kwenye mzizi ‘**-ake**’. Badala ya kiambishi hiki, katika MYW, ni kiambishi ‘**z-’** ambacho kimetumika. Hiki ni kiambishi cha wingi wa ngeli za U - ZI na I - ZI. Katika 33a, nomino inayopatanishwa ni ‘**afya**’ na inapatikana katika ngeli ya I - I na haibadiliki katika umoja na wingi. Katika mzizi ‘**-etu**’ kiambishi ‘**z-**’ kimewekwa na kwa hivyo kudokeza wingi. Kwa mujibu huu basi, neno ‘**afya**’ lina wingi wake na hii sio sahihi kwa sababu afya haihesabiki. Kiambishi kilichofaa kuwepo hapa ni ‘**y-**’ ili iwe ‘… **afya yetu**’ wala sio ‘…**afya zetu**’. Katika 50a, nomino ‘**samaki**’, iliyo katika ngeli ya A - WA, imepatanishwa na nazali **ny-** kwenye mzizi wa kivumishi ‘**-ingi**’. Huu ni upatanisho unaoambatana na ngeli za U - ZI na I – ZI wala sio A – WA.

Jambo linalodhihirika hapa ni kwamba wanafunzi wamejumlisha kila nomino na kuiingiza katika ngeli ya I – ZI ndiyo maana wanatumia vivumishi ‘**tamu**’, ‘**zake**’, ‘**zetu**’, ‘**nyingi**’, ‘**nzuri**’ na ‘**mbaya**’ katika hali zote. Kosa hili halihusishwi na jamii maalum bali ni matumizi maarufu miongoni mwa wanajamii. Kuna mazoea ya watu wengi kuingiza kila nomino katika ngeli ya I – ZI. Kwa mfano, ni kawaida kusikia tungo kama:

*1. Ng’ombe **zote** zinakula mboga.
*2. Mahindi **nyingi** zilikatwa.
*3. Gari **yote** imejaa matope.
*4. Kiatu **yake** imeraruka.
*****5. Vitabu **ndio hizi**.

Mifano hii inadhihirisha jinsi upatanisho wa ngeli ya I – ZI unavyoathiri kila nomino.

Makosa ya kupatanisha vihusishi yalihusu vihusishi vya **-a** unganifu na yalidhihirika katika MYW. Kihusishi cha aina hii huwa na mzizi '**-a**' ambao huchukua kiambishi cha ngeli ya nomino inayorejelewa katika uhusishaji wenyewe. Katika MYW, kulikuwa na tungo zifuatazo zenye upatanisho usiokubalika wa kihusishi hiki:

26. a) Kucha **la** kidole changu limerefuka.
30. a) Kwanza kabisa katika kabila **ya** Wameru mtoto alipozaliwa ilikuwa ni furaha.

Katika 26a, nomino '**kucha**' (wingi wa '**ukucha**') imepatanishwa na kiambishi '**l-**' katika kihusishi '**la**'. Hiki ni kipatanishi cha ngeli ya LI – YA katika umoja na ni kosa kwa sababu '**kucha**' ni nomino iliyo katika ngeli ya U – ZI. Kiambishi mwafaka cha wingi ni '**z-**'. Katika 30a, kiambishi '**y-**' kwenye kihusishi '**ya**' kinaambatana na ngeli za I – I, I – ZI (umoja) na U – I (wingi). Nomino '**kabila**' inapatikana katika ngeli ya LI – YA na kwa hivyo kiambishi kinachofaa ni '**l-**' kuonyesha umoja.

Makosa mengine katika upatanisho yalihusu viambishi vya urejeshi kwa mujibu wa ngeli ya nomino inayorejelewa. Uambishaji huu ulitokea katika vitenzi na penginepo ukatokea katika mzizi '**amba-**'. Katika tungo zifuatazo za MYW, kuna makosa yanayohusu ngeli ya A – WA:

32. a) Kitu kingine **ambayo tunayofuatilia** ni **ile** saa ya kuzaliwa.
35. a) Mama alizaa mtoto wa kwanza na hawa **waliyomfuata** wakafa mfululizo.
36. a) Moshi **tuliyoiona** jana ilionyesha kuchomeka kwa nyumba.
37. a) Maneno **aliyeyasema** yalinidhuru rohoni.

Kutumiwa kwa virejeshi viwili '**amba-**' na '**-yo'** katika 32a hakukubaliki kisarufi. (Kosa hili limejadiliwa chini ya 5.5.1 kuhusu *Upatanisho Katika Vitenzi*: MYW). Mbali na kosa la kutumiwa kwa virejeshi viwili katika tungo hii ili kurejelea nomino moja, kiambishi cha urejeshi kilichotumiwa hakiambatani na ngeli ya nomino '**kitu**' kwani ndiyo inarejelewa katika tungo hii. Kumetumiwa kiambishi **-yo** ambacho hurejelea ngeli mbalimbali kama tunavyoeleza baadaye katika mjadala huu. Nomino

'**kitu**' ilistahili kuambishwa **- cho** kwa sababu iko katika umoja wa ngeli ya KI – VI. Kanuni iliyopo ni kwamba kiambishi cha urejeshi kinachowekwa katika kitenzi, ndicho kinaambishwa kwenye mzizi '**amba**-', ikiwa mwandishi anataka kutumia kirejeshi '**amba-**' katika tungo. Kwa mujibu wa maelezo haya basi, tungo hiyo inaweza kusahihishwa kwa namna mbili zifuatazo:

1. Kitu kingine **ambacho** tunafuatilia ni…

   au

2. Kitu kingine **tunachofuatilia** ni….

Katika tungo ya kwanza '**amba**-' imetumiwa ilhali kwenye tungo ya pili kirejeshi '**-o**' kimetumiwa ndani ya kitenzi kama kiambishi awali. Katika 35a kiambishi '-**yo**-' kilichotumiwa hakiambatani na ngeli ya A – WA ambayo inarejelewa katika tungo hii kutokana na matumizi ya kiwakilishi kionyeshi '**hawa**'. Kiambishi cha wingi katika ngeli ya A – WA ni **'-o-'**. Katika 36a kunayo makosa ya kutopatanisha kitenzi kwa usahihi kwa mujibu wa ngeli na tuliyaangazia katika *5.5.1 kuhusu Upatanisho Katika Vitenzi: MYW*. Mwanafunzi alikiuka kanuni ya kupatanisha kirejeshi na ngeli ya U – I umoja. Nomino '**moshi**' ndiyo inarejelewa katika tungo hii. Kipatanishi chake sahihi ni '-**o**-' wala sio '-**yo**-'. Kiambishi '-**yo**-' hutumika katika ngeli zenye viambishi I na YA. Hebu tuangalie mifano ifuatayo:

1. Mikoba **iliyopotea** ilipatikana. - U-I
2. Nguo **iliyochafuka** imefuliwa. - I-ZI
3. Chai **inayopikwa** itanywewa. -I-I
4. Mayai **yatakayotagwa** yatauzwa. -LI-YA
5. Maji **yanayomwagika** yanatekwa. -YA-YA
6. Maradhi **yaliyosumbua** yametibiwa. -U-YA

Kuna uwezekano kwamba kwa sababu ya kiambishi kipatanishi cha urejeshi **-yo** kutokea katika ngeli nyingi namna inavyodhihirika katika mifano sita ya hapo juu, wanafunzi walijumlisha kanuni hii na kuihusisha kwenye ngeli za A-WA na U-I. Ni kawaida ya watumiaji lugha kujumlisha kanuni inayotokea katika miktadha mingi kwa kuitumia popote na matokeo yake yanakuwa ni makosa katika lugha jinsi

ilivyofanyika katika 35a na 36a. Matumizi yasiyofaa ya kiambishi kirejeshi cha ngeli ya A – WA katika umoja yalidhihirika katika 37a ambapo badala ya kutumia '**-yo-**', (kwani ndicho kiambishi kirejeshi kinachopatana na nomino '**maneno**' katika ngeli ya LI – YA), kiambishi '**-ye-**' kilitumiwa. Hili ni kosa linalosababishwa na matamshi mabaya. Tunaweza kusema kwamba matumizi potofu yaliyozoeleka pamoja na matamshi mabaya katika jamii huigwa na wanafunzi katika maandishi yao na kusababisha makosa katika lugha.

### 5.5.4 Upatanisho katika vivumishi, vihusishi na virejeshi: vitabu vya kiada

Katika VVK, upatanisho usiokubalika katika vivumishi ulitokea katika vitabu vyote vitatu tulivyochunguza yaani UWK, KF na KK. Kwa kutazama mifano hii, tunaweza kuthibitisha kuwepo kwa makosa ya upatanisho katika VVK:

11. a) Kwa kuwa si kila mtu hubobea katika nyanja **hii** ya fasihi basi pana haja kubwa ya kuwa na mhakiki. UWK uk.32
15. a) Utuletee miwa hiyo hapa na **mingineo** uwapelekee wale wengine. KK uk. 59
35. a) Baadaye alichoka kushikilia mambo ya kizamani ya kukaa katika duara **dogo la** mila ngumu zilizozuia ushirika wa mwanamke. KF uk.191
37. a) Nyumba **zee** ilipakwa rangi ingawa haipendezi. KF uk. 203

Katika 11a UWK, nomino '**nyanja**' ambayo ni wingi wa nomino '**uwanja**' imepatanishwa visivyo na kivumishi kionyeshi '**hii**' ambacho kinaashiria ngeli zenye kiambishi 'I' yaani U – I, I – ZI na I - I. Kwa sababu nomino '**nyanja**' iko katika ngeli ya U – ZI wingi, mwandishi alistahili kutumia kivumishi '**hizi**'. Katika 15a KK, kivumishi cha pekee chenye mzizi, '**-ingine-o'**, katika sehemu yake ya pili hakijaambishwa - **y**- jinsi inavyofaa kuwa katika wingi wa ngeli ya U - I. Badala ya '**mingineo**' kulitakiwa kuwa na '**mingineyo**'. Katika 35a KF na 37a KF, nomino '**duara**' na '**nyumba**' za ngeli ya I – ZI, zimepatanishwa na LI – YA katika vivumishi vya sifa. Katika 35a KF, mzizi '**dogo**' haujaambishwa. Huku

kutoambishwa huhusu ngeli ya LI – YA. Kwa vile nomino '**duara**' iko katika ngeli ya I – ZI, kiambishi '**n-**' kinastahili kuwekwa mwanzoni mwa mzizi huo. Hivi ndivyo hali ilivyo katika 37a KF ambapo kivumishi '**zee**' kilifaa kuambishwa '**n**' mwanzoni ili kuafikiana na ngeli ya I - ZI kwa sababu nomino '**nyumba**' inapatikana katika ngeli hii.

Upatanisho usiokubalika katika VVK ulitokea katika vihusishi namna inavyoonekana katika tungo zifuatazo:

1. a) Vifuatavyo ni aina **ya** vipashio vya lugha. UWK uk.2
12. a) Baadhi ya tungo zinahitaji mzinduko na umakini wenye nidhamu **wa** maneno yanayounda sentensi. UWK uk. 32
49. a) Ni nyenzo **ya** kuimarisha umoja na ushirikiano miongoni mwa wanajamii. KF uk. 215

Katika 1a UWK, nomino '**aina**' iliyo katika ngeli ya I – ZI inaashiria wingi kwa sababu aina zenyewe ni mbalimbali. Kiambishi '**y**-' katika kihusishi '**ya**' kinadokeza umoja na kwa hivyo upatanisho huu sio sahihi. Katika wingi, kiambishi mwafaka ni '**z**-' na kwa hivyo, badala ya '**ya**', '**za**' ni kihusishi kinachostahili kutumiwa. Kosa la kupatanisha visivyo kihusishi '**wa**' na nomino '**nidhamu**' inayopatikana katika ngeli ya I – I linadhihirika katika 12a. UWK. Kiambishi '**w**-' hakiambatani na ngeli hii. Hiki ni kiambishi cha ngeli za U na A - WA. Inavyoonekana ni kwamba upatanisho huu ulikuwa ni athari kutoka kwa nomino '**umakini**' ambayo iko katika ngeli ya U – U. Kihusishi mwafaka katika muktadha huu kinafaa kuwa '**ya**'. Katika 49a, KF kuna kosa katika kupatanisha kihusishi na ngeli ya nomino. Nomino '**nyenzo**' ni wingi wa '**wenzo**' na ziko katika ngeli ya U – ZI. Kihusishi '**ya**' ambacho kimetumiwa katika tungo hii, kinaambatana na ngeli za I - I, I – ZI (umoja) na U – I (wingi) wala sio ngeli ya U – ZI. Vihusishi vinavyostahili kupatanishwa na ngeli hii katika umoja na wingi ni '**wa**' na '**za**'. Kwa kuzingatia kwamba nomino '**nyenzo**' iko katika wingi basi upatanisho sahihi ni '**za**'. Hata hivyo, kulingana na maana iliyo katika tungo hii,

sharti nomino hii iwe katika umoja yaani, ‘**wenzo**’ na hivyo basi kipatanishi mwafaka ni ‘**wa**’. Kwa hivyo, usahihi wa tungo hii kisarufi na kimaana unafaa kuwa:

> Ni **wenzo wa** kuimarisha umoja na ushirikiano miongoni mwa wanajamii.

Kwa sababu kosa hili linapatikana katika VVK, tunaweza kudai kwamba waandishi wake walikosa kumakinikia kazi yao au walikuwa na haraka.

Makosa ya utumiaji wa viambishi virejeshi visivyostahili au kudondosha viambishi virejeshi katika tungo yalidhihirika katika VVK. Mifano hii ilipatikana katika UWK:

> 3. a) Taja konsonanti 10 za Kiswahili na utoe mfano wa neno lenye kila konsonanti **ulioitaja**. UWK uk. 3
> 9. a) Andika konsonanti **zinatamkwa** katika viungo vifuatavyo vya kutamkia. UWK uk. 23
> 29. a) Kuwepo kwa chanjo katika enzi hii kumesaidia kupiga vita ndwele kama vile ndui **ambao** iliteketeza roho nyingi hapa Kenya kabla ya uhuru. UWK uk. 136

Nomino ‘**konsonanti**’ ndiyo inarejelewa katika 3a UWK na 9a UWK. Nomino hii iko katika ngeli ya I – ZI na kwa hivyo umbo lake halibadiliki katika wingi na umoja. Hata hivyo, viambishi vyake vinatofautiana umoja na wingi. Katika 3a UWK, nomino hii imerejelea umoja. Kiambishi chake cha urejeshi ni ‘**-yo-**’ wala sio ‘**-o-**’ jinsi inavyoonekana katika tungo husika. Katika 9a UWK, nomino hii imedokeza wingi. Tofauti na hali ilivyo katika tungo nyingine, kosa lililofanywa hapa ni kuacha kiambishi cha urejeshi katika kitenzi kinachorejelewa yaani ‘**zinatamkwa**’. Ili kurekebisha kosa hili, ni lazima kutumia kirejeshi ‘**-zo-**’ katika kitenzi hicho na kinaweza kuwa kiambishi awali ambapo neno litakuwa ‘…**zinazotamkwa**…’ au kiambishi tamati katika kitenzi ambapo kitakuwa ‘…**zitamkwazo**…’

Hapa tunaona kwamba katika namna ya pili ya kusahihisha, kiambishi cha wakati ‘-**na**-’ kinadondoka. Katika 29a UWK, kiambishi cha urejeshi kilichowekwa katika mzizi ‘**amba-**’ hakiambatani na ngeli ya nomino husika. Kiambishi kilichotumiwa

katika tungo hii kuonyesha urejeshi kinapatana na ngeli kama ya A-WA wingi, na ngeli zote za U wala sio ya I – I ambayo ndiyo ngeli ya nomino '**ndui**' inayorejelewa katika tungo hii. Hivyo basi, tungo hii katika usahihi wake inafaa kuwa:

> Kuwepo kwa chanjo katika enzi hii kumesaidia kupiga vita ndwele kama vile ndui **ambayo** iliteketeza roho nyingi hapa Kenya kabla ya uhuru.

Makosa katika upatanisho kwenye VVK yanahusishwa na udhaifu wa waandishi katika kumilisi sarufi ya Kiswahili Sanifu. Ni wazi kwamba walioteuliwa kuandika kitabu hiki hawakuweza kutambua tofauti hii.

## 5.6 Minyambuliko Isiyokubalika

Kwa mujibu wa Obuchi na Mukhwana (2010), kunyambua vitenzi ni kuambika viambishi tamati kwenye vitenzi ili kuvipa vitenzi hivyo hali mbalimbali ambazo huitwa kauli. Kwa hivyo, wanavirejelea viambishi hivi kama viambishi vya kauli ama viambishi vya mnyambuliko wa vitenzi. Hata hivyo, ni muhimu kukumbuka kwamba ingawa vitenzi ndiyo aina ya maneno inayosheheni utajiri mkubwa wa mnyambuliko, kuna aina nyingine za maneno yanayoweza kunyambuliwa. Kwa mfano, nomino kama '**dhiki**', '**huzuni**' na '**aina**' zinanyambulika katika kauli ya kutendesha na kuwa '**dhikisha**', '**huzunisha**' na '**ainisha**'. Aidha, kivumishi '**laini**' kinanyambuliwa na kuwa '**lainisha**', na kiunganishi '**baina**' huwa '**bainisha**' katika kauli ya kutendesha. Mifano zaidi ya nomino zinazoweza kunyambuliwa ni '**amri**', '**elimu**' na '**tamati**'. Mradi, jambo tunalotaka kuweka wazi ni kwamba dhana ya mnyambuliko haistahili kubanwa kwenye vitenzi pekee kwa sababu kuna aina nyingine za maneno ambazo hukubali kunyambuliwa. Matokeo ya minyambuliko ya aina hizo zote za maneno huwa ni kupata kitenzi – neno linalopatikana huwa ni kitenzi kama inavyodhihirika katika mifano yote tuliyotaja hapo juu.

Katika sehemu hii, uhakiki wetu ulizingatia zaidi makosa yaliyotokea katika kunyambua vitenzi. Katika uchanganuzi wetu, tulizingatia vitengo viwili yaani, Mnyambuliko Usioafikiana na Muktadha na pili, Kushindwa Kunyambua.

### 5.6.1 Mnyambuliko usioafikiana na muktadha: maandishi ya wanafunzi

Katika sehemu hii tumejadili makosa yaliyofanyika katika kunyambua vitenzi ambapo ingawa mnyambuliko huo unakubalika katika Kiswahili sanifu mnyambuliko wenyewe ni kosa kwa sababu ya kutokubaliana na muktadha unaorejelewa. Katika MYW tulitambua makosa yafuatayo:

22. a) Mwalimu **aliogopewa** kwa ukali wake.
24. a) Ni lazima shangazi wa mtoto yule kuja **kumpatia** jina.
34. a) Katika kabila langu la Kikuyu, watoto wanapozaliwa huwa anapelekwa kwa babu **kupatiwa** jina.

Kitenzi '**aliogopewa**' katika 22a, kiko katika kauli tendewa na kina asili yake katika kitenzi '**ogopa**'. Hii ni kauli inayokubalika kuhusu kitenzi hiki katika Kiswahili. Hata hivyo, katika muktadha wa tungo hii, maana ya kitenzi hiki haiafikiani na maana inayolengwa katika tungo. Dhana inayolengwa katika tungo hii ni kwamba watu wanamwogopa mwalimu kwa sababu ya ukali wake. Kwa hivyo, mwalimu ni shamirisho kipozi kwa sababu ndiye anapokea athari za moja kwa moja za tendo la kuogopa na hafai kurejelewa kwa kauli tendewa inayotumiwa kudokeza shamirisho kitondo. Mnyambuliko mwafaka hapa ni lazima uwe katika kauli tendwa ambapo kitenzi hiki kitakuwa '**aliogopwa**'. Tungo hii inastahili kuwa:

Mwalimu **aliogopwa** kwa sababu ya ukali wake.

Vitenzi '**kumpatia**' na '**kupatiwa**' katika 24a na 34a mtawalia, vina asili yake katika kitenzi chenye shina la silabi moja '**-pa**'. Vitenzi vingine katika Kiswahili ambavyo ni vya aina hii ni, **-cha**, **-chwa**, **-fa**, **-ja**, **-la**, **-nya**, **-nywa**, **-pwa,** na **-wa**. Vitenzi hivi haviwezi kujisimamia kama maneno hadi viambishwe '**ku-**' mwanzoni. Kwa mfano,

**ku+cha** tunapata '**kucha**' ambalo ni neno lenye maana kamili. Kwa hivyo, kitenzi '**kumpa**' ndilo neno kamili la Kiswahili na lina maana ya '**pokeza mtu**' au '**kabidhi mtu**'. Hapa tunaona kwamba ni lazima kuweka '**m**' ili kurejelea shamirisho kwa sababu ya kumtambua anayepokea kitu kinachorejelewa. Mnyambuliko ulio katika 24a, unarejelea kauli tendea yaani, '**fanya mtu apokee**' na katika muktadha huu ni '**fanya mtoto apokee jina**'.

Kwa kutumia kitenzi '**kumpatia**' dhana inayodhihirika ni ya: '**pata kwa niaba ya** au **badala ya**' na kitenzi chake asilia ni '**pata**'. Kwa sababu ujumbe unaolengwa ni kwamba mtoto anafanywa awe na, au amiliki jina, basi tungo hii ilifaa kuwa:

Ni lazima shangazi wa mtoto kuja **kumpa** jina.

Katika tungo hiyo hapo juu, tunaona kiambishi '**m**' katika kitenzi '**kumpa**' ambacho ni sharti kiwepo ili kudhihirisha shamirisho katika fungutenzi. Hatuwezi kuwa na neno '**kupa**' bila kuweka kiambishi kinachoonyesha ni nani anayepokea athari za kitendo.

Kitenzi '**kupatiwa**' katika 34a, kiko katika kauli tendewa na kinamaanisha '**pata kwa niaba ya**' au '**saidiwa kupata**'. Hapa tunaona kwamba hii ni kauli tendewa ya kitenzi '**pata**'. Kama ilivyo katika 24a, dhana iliyo hapa ni kwamba babu anampokeza mtoto aliyezaliwa jina. Kwa sababu kitenzi '**-pa**' kinamaanisha '**pokea athari za moja kwa moja za tendo**' yaani, kama shamirisho kipozi, kitenzi hiki hakiwezi kunyambuliwa katika kauli tendea na kuwa '**pea**'. Hata hivyo, katika kauli tendewa, kitenzi hiki huwa '**pewa**' na maana yake ni '**pokea**'. Katika tungo hii, kwa sababu babu ndiye mtendaji basi mtoto ni mtendewa na kwa hivyo anafaidika na kitendo cha kutolewa jina wala sio '**kupata kwa niaba ya'**, namna inavyodokezwa katika MYW. Kwa hivyo, tungo hii inastahili kuandikwa kama inavyoonyeshwa hapa chini:

> Katika kabila langu la Kikuyu, watoto wanapozaliwa huwa wanapelekwa kwa babu **kupewa** jina.

Ikumbukwe kuwa tungo hii ilikuwa na zaidi ya aina moja ya makosa na kwa sababu kila kosa lilishughulikiwa katika kitengo chake, katika tungo mpya makosa yote yamesahihishwa.

### 5.6.2 Mnyambuliko usioafikiana na muktadha: vitabu vya kiada

Makosa yafuatayo yalitokea katika VVK kuhusu mnyambuliko usioafikiana na muktadha:

> 18. a) Kila mwananchi akijitahidi na kutekeleza jukumu lake ipasavyo, nchi yetu itanufaika katika **kufufulia** na kuendeleza uchumi wake. UWK uk. 103
> 8. a) … mawingu yanaashiria kukaribia kwa mvua **kunyesha**. KK uk. 32
> 24. a) Usingizi **huupatia** mwili nguvu. KK uk. 222
> 28. a) Utafiti huo **umefika** hatua ambayo miche na mizizi ya mimea ya G.M.O ina uwezo wa kuondoa na kuvunja makali ya madini yenye sumu katika maji na **ardhini** kwa ujumla. KK uk. 239
> 5. a) Halafu siku moja **ikanyesha** mvua kubwa iliyoandamana na radi. KF uk. 73
> 8. a) Wanafunzi **wanasoma** darasani. KF uk. 75
> 47. a) Kama mwandalizi wa shughuli za **uchuguzi** wa viongozi wa Baraza la Wanafunzi shuleni mwenu, andika ratiba itakayofuatwa katika sherehe ya **kuapiza** viongozi wapya wa Baraza la Wanafunzi. KF uk. 213

Neno '**kufufulia**' kwenye tungo 18a UWK linatokana na kitenzi '**fufua**' na liko katika kauli tendea. Kauli hii hudokeza dhana ya kutumia kitu ili kufikia malengo fulani. Mnyambuliko huu sio mwafaka kwa kuzingatia maana inayodhamiriwa. Kitenzi hiki kinafaa kuwa katika kauli ya kutenda yaani, '**kufufua**' ikiwa ndiyo kauli ya kitenzi '**kuendeleza**' katika tungo hii na ambacho kimeunganishwa na '**kufufua**' kwa kutumia kiunganishi cha kujumuisha '**na**'. Huku kuunganishwa kuna maana kwamba vitenzi vyote viwili vinafaa kuwa katika kauli moja badala ya kuchanganya kauli tendea katika neno '**kufufulia**' na kauli tenda kwenye kitenzi '**kuendeleza**'. Tungo hii ikirekebishwa inastahili kuwa:

> Kila mwananchi akijitahidi na kutekeleza jukumu lake ipasavyo, nchi yetu itanufaika katika **kufufua** na **kuendeleza** uchumi wake.

Kama tulivyoeleza katika sehemu ya *5.6.1: Mnyambuliko Usioafikiana na Muktadha:* MYW, kitenzi '**-pa**' kinapotumika kuonyesha kauli tendea hakiwi '**patia**' kama kinavyotumiwa katika 24a KK bali huwa '**-pa'** lakini hutanguliwa na kiambishi kinachorejelea shamirisho, kwa hivyo tutasema 'Usingizi **huupa** mwili…' ikiwa ndiyo njia sahihi ya kuwasilisha dhana inayolengwa katika tungo hii. Katika 24a KK, vitenzi vilivyokolezwa vimedumisha kauli tenda badala ya kuwa katika kauli tendea ambayo ndiyo itawasilisha maana inayokusudiwa katika tungo. Katika 28a KK, kitenzi '**fika**' sio kielekezi na kwa hivyo haifai kukifuatisha nomino '**hatua'**. Ili kukubali kuteua nomino hii katika tungo hiyo, ni lazima kunyambua kitenzi '**fika**' katika kauli tendea. Vitenzi vingi katika kauli tendea huwa vielekezi. Hivyo basi tungo hii itaanza hivi:

> Utafiti huo **utafikia** hatua ambayo…

Kitenzi kingine chenye shina la silabi moja ambacho kilinyambuliwa isivyofaa kulingana na muktadha ni '**-nya**'. Kwa kuambishwa '**ku**-' mwanzoni tunapata neno '**kunya**' jinsi inavyoonekana katika 8a KK na 5a KF. Kati ya maana mbili za kitenzi hiki, moja ni ile ya tendo la mvua kudondoka kutoka mawinguni. Katika kauli tendesha, kitenzi hiki huwa ni '**nyesha**'. Maana ya '**nyesha**' ni 'sababisha mvua kudondoka kutoka mawinguni.' Katika 8a KK na 5a KF, mvua imerejelewa kama inayosababisha kudondoka kwake na hii sio sahihi kwa sababu mvua ndiyo inafanya kitendo hicho. Kuja kwa mvua ni '**kunya**' wala sio '**kunyesha**'. Kwa hivyo, ingawa '**nyesha**' ni mnyambuliko sahihi wa kitenzi hiki, lakini kwa mujibu wa miktadha inayolengwa katika tungo hizi, mvua '**hunya**'. Kwa mantiki hii basi, tungo zote mbili zitasahihishwa ifuatavyo:

> … mawingu yanaashiria kukaribia kwa mvua **kunya**. (8 KK)

Halafu siku moja **ikanya** mvua kubwa iliyoandamana na radi. (5 KF)

Tukiangalia vitenzi vingine vyenye shina la silabi moja na kuviweka katika majaribio ya namna hii, tutaona kwamba tungo hizo mbili ni sahihi. Hebu chunguza mifano hii:

1. Jua lilifanya miche **ikafa.**
2. Mgeni amefika **akanywa** maji.
3. Waumini **walimcha** Mola kwa kusujudu.

Tukiongeza kiambishi '**ku-**' katika kila kitenzi kilichokolezwa tunapata maneno '**ikakufa**', '**akakunywa**' na '**walimkuch**a' na yote sio sahihi kisarufi.

Katika 8a KF, ingawa '**soma**' ni kitenzi kielekezi, kijalizo chake hakifai kuwa kielezi cha mahali namna ilivyo katika neno '**darasani**'. Kitenzi '**soma**' kikiwa katika kauli tenda, kinateua nomino kama vile vitabu, jarida, gazeti, insha, kifungu na kadhalika katika muktadha huu. Ikiwa kielezi kitahitajika basi, sharti kiwe ni cha namna kama vile **polepole**, **haraka**, **kistadi** na kadhalika. Hata hivyo, kwa kuelewa kwamba dhana inayonuiwa hapa ni kwamba tendo la kusoma linafanyikia mahali fulani basi, kielezi cha mahali kinadumishwa katika tungo hii. Ili kudumisha kielezi cha mahali katika tungo hii, ni lazima kitenzi hiki kinyambuliwe katika kauli tendea ambapo tungo hii itakuwa:

Wanafunzi **wanasomea** darasani.

Katika tungo 47a KF, kuna kosa la kunyambua kitenzi katika kauli ya kutendesha kwa kuweka alomofu isiyofaa katika kauli hii. Alomofu za kauli ya kutendesha ni nyingi mno. Obuchi na Mukhwana (2010) wameorodhesha 10 nazo ni: **-ish-**, **-esh-**, **-z-**, **-lish-**, **-lesh-**, **-vy-**, **-ez-**, **-fy-**, **-iz- na -s-**. Katika tungo hii, '**kuapiza**' ni kitenzi kinachomaanisha '**kulaani**' au '**kuombea mtu mabaya'**. Matumizi ya kitenzi hiki katika tungo 47a KF, yanalenga maana ya kitenzi asilia '**apa**' kilicho na maana ya 'taja jina la Mwenyezi Mungu ili kuthibitisha jambo fulani'. Katika kauli ya kutendesha, kitenzi hiki huchukua kiambishi -**ish**- na kwa hivyo umbo lake huwa

'**apisha**'. Kwa kuzingatia kwamba maana ya tungo hii ni kwamba viongozi waliochaguliwa wanathibitisha kwamba watatekeleza majukumu yao kwa uaminifu, basi sherehe hiyo sio ya '**kuapiza**' bali ni ya '**kuwaapisha'**.

Ni dhahiri kwamba baadhi ya makosa kwenye MYW kuhusu kunyambua vitenzi vya shina la silabi moja yamefanana na yale yaliyo katika VVK. Hili ni tatizo la kijamii miongoni mwa watumiaji wengi wa Kiswahili ambao hutatizika katika kunyambua vitenzi vya aina hii. Huenda ni kwa sababu ya matumizi maarufu ya minyambuliko isiyo sahihi ya vitenzi hivi ambapo waandishi wa vitabu walifanya makosa haya. Haya ni mazoea potofu. Ajabu moja katika lugha ni kwamba mitindo potofu inapozuka kwa namna hii, hutokea kuwa maarufu na kuigwa kiasi cha kupendelewa zaidi ya mifumo rasmi. Kwa sababu ya matamshi kuathiri maandishi, makosa haya yanadhihirika kupitia maandishi yao vilevile. Hii ndiyo sababu ya kuwepo kwa makosa katika maandishi.

### 5.6.3 Kushindwa Kunyambua

Katika sehemu hii, tunahakiki makosa yaliyotokana na jaribio la kunyambua neno lakini matokeo yakawa ni maumbo ambayo sio maneno katika Kiswahili sanifu. Makosa ya aina hii yalikuwa machache katika kazi tulizochunguza na mengi ya makosa katika kitengo hiki yalikuwa katika MYW. Makosa mawili ya kwanza yalitokea katika MYW na lile la tatu likatokea katika maandishi ya kiada:

21. a) Naomba **msiwekanie** visasi hata kama mmepigana.
57. a) Hufanya karamu ya kufana ili **kupea mtoto jina.**
35. a) **Ninatamati** kwa kuwatakia kila ufanisi katika Nyanja zote za maisha. UWK uk. 172

Neno '**msiwekanie'** katika 21a, linatokana na kitenzi '**weka**'. Kwa sababu ni kitenzi chenye asili ya Kibantu, mzizi wake ni '**wek-**' kwani '**-a**' ni kiishio cha kitenzi. Katika tungo hii, mwanafunzi alidhamiria kuwasilisha kauli ya kutendeana. Hii ni

kauli ambayo huwa ni muungano wa kauli mbili yaani kutendea na kutendana. Kwa sababu hii, kutakuwa na viambishi viwili vinavyoonyesha kauli navyo vitafuatana katika kitenzi. Hivi viambishi hutokea baina ya mzizi na kiishio cha kitenzi. Viambishi vya kutendea ni: **-i-na-, -e-an-, -li-an-,** na **-le-an-**. Katika tungo ya mwanafunzi, baina ya mzizi **wek-** na kiishio '**-e**' kinachoonyesha kuamrisha, kuna viambishi **-a-ni-** na hivi sio miongoni mwa viambishi vinavyoonyesha kauli ya kutendeana. Viambishi mwafaka katika kauli hii, kwa mujibu wa kitenzi hiki ni '**-e-an-**' na kwa hivyo hicho kitenzi kinastahili kuwa '**msiwekeane**'.

Katika tungo 57a, kuna kosa katika kitenzi chenye shina la silabi moja '**-pa**'. '**Kupea**' sio mnyambuliko kubalifu katika Kiswahili sanifu kwa kuzingatia mantiki ya tungo. Kiambishi '**-e-**' katika kitenzi hiki kinaonyesha kauli ya kutendea lakini kwa mujibu wa maana ya kitenzi hiki, huu ni mnyambuliko kapa. Kauli ya kutendea katika kitenzi hiki ni '**pelea**' yaani, '**kabidhia mtu kitu mahali fulani'** au '**fanya kwa niaba ya**'. Kwa hivyo, kwa sababu hakuna mnyambuliko unaokubali neno '**kupea**', kosa linatokea katika tungo hii.

Neno '**ninatamati**' katika 35a UWK ni kitenzi kinachotokana na nomino '**tamat**i'. Viambishi '**ni**-' na '**-na-**' katika neno hili vinaonyesha mtendaji na wakati uliopo. Baada ya viambishi hivi kuambishwa katika nomino, hiyo nomino imepewa hadhi ya kuwa kitenzi katika tungo hiyo. Kwa hivyo, ni sharti hadhi hii ya kuwa kitenzi iandamane na kauli sahihi ambayo ni kutendesha. Kwa hivyo, hakuna mnyambuliko wa '**ninatamati**' bali '**ninatamatisha**'. Huu mfano ni mmoja wa minyambuliko nadra ya nomino ambapo matokeo yake huwa ni vitenzi. Mifano zaidi ya maneno yanayokubalika kunyambuliwa ingawa si vitenzi ni: Nomino **'tofauti', 'lazima',**

**‘amri’, ‘aina’, na ‘dhiki’**, Vivumishi ‘**salama’, ‘sahihi’, ‘laini’** na **‘sanifu’**, Kiunganishi ‘**baina**’ na Kielezi **‘sawa’**.

## 5.7 Makosa ya Uambishaji

Kwenye sehemu hii tulishughulikia makosa ya kuweka au kukosa kuweka kiambishi, yaani mofu fulani katika neno au mzizi wa neno na kuathiri sarufi katika tungo husika. Kwa sababu uambishaji huu hauhusiani moja kwa moja na ngeli, hatukuuchukulia kuwa upatanisho wa kisarufi. Makosa haya yalitokea katika aina mbalimbali za maneno kama inavyodhihirika katika mifano tuliyorejelea katika MYW na VVK.

### 5.7.1 Makosa ya uambishaji: maandishi ya wanafunzi

Katika sehemu hii, tunahakiki makosa ambayo yanadhihirika katika maneno yaliyoambishwa. Uambishaji huu umetokea kupitia tungo zifuatazo:

33. a) **Ma**dawa za kulevya hudhuru afya zetu.
38. a) Mbona **haunithamini**?
39. a) Mtoto anaweza **kubali** jina au akatae.
42. a) Mwanafunzi alitumia njia ya matusi kumjibu **m**hasidi wake.
45. a) Wa kwanza **ako** na jina binafsi.
47. a) Hawezi **mmalizia** shida zake.
49. a) Mama alifua **ma**nguo.
55. a) Alipelekwa nje na kukalishwa kwa **kiketi**.

Katika 33a na 49a, wanafunzi waliweka kiambishi ‘**ma-**’ kinachoashiria wingi wa nomino katika ngeli ya LI – YA mwanzoni mwa nomino zilizo katika ngeli ya I – ZI. Hizi ni nomino ambazo maumbo yake hayabadiliki katika umoja na wingi. Kwa hivyo nomino ‘**dawa**’ na ‘**nguo**’ hazipaswi kuambishwa zinapogeuzwa katika wingi. Haya ni makosa yanayoashiria ujumlishaji wa kanuni ya kuambisha ‘**ma-**’ mwanzoni mwa baadhi ya nomino ili kuzigeuza katika wingi. Hali ya ukanusho wa nafsi ya pili umoja inadhihirika katika 38a. Kiambishi ‘**u**’ katika kitenzi ‘**haunithamin**i’ ni kiwakilishi cha nafsi ya pili umoja katika kauli yakinifu. Katika hali kanushi, herufi

‘**a**’ kwenye kiambishi kanushi ‘**ha**’ inafaa kudondoshwa na kwa hivyo, tunastahili kusema:

Mbona hunithamini?
wala sio
Mbona h**au**nithamini?

Maandishi haya yameathiriwa na kanuni ya ngeli zilizo na kiambishi U ambapo katika kukanusha, kiambishi ‘**ha-**’ hutangulia ‘**u-**’ namna inavyodhihirika katika mifano ifuatayo:

| **Yakini** | **Kanushi** | **Ngeli** |
|---|---|---|
| 1. Mkono **u**nauma. | Mkono **hau**umi. | U - I |
| 2. Ugonjwa **u**mezuka. | Ugonjwa **hau**jazuka. | U - YA |
| 3. Uteo **u**taundwa. | Uteo **hau**taundwa. | U - ZI |
| 4. Upole **u**limwokoa. | Upole h**au**kumwokoa. | U – U |

Bila shaka kosa lililo katika 38a linalotokana na ujumlishaji wa kanuni hii ya ukanushaji katika ngeli hizi. Wanafunzi wamejumlisha kanuni inayohusu ngeli hizi katika kukanusha nafsi ya pili umoja kwa sababu ya kuona kwamba kiambishi kinachowakilisha nafsi hiyo ni ‘U-‘.

Katika 39a na 47a, kuna vitenzi viwiliviwili ambapo cha kwanza katika kila tungo ni kisaidizi na cha pili ni kikuu. Kanuni iliyopo ni kwamba kitenzi ‘**weza**’ kinapofuatwa na kitenzi kingine katika tungo, ni sharti kitenzi cha pili kichukue kiambishi awali ‘**ku-**’ kwa sababu hicho cha pili ndicho kitakuwa kimebeba ujumbe mkuu katika tungo huku ‘**weza**’ kikiwa kisaidizi. Hata hivyo, vitenzi vyote vikuu katika kila tungo vimekosa kuwekewa kiambishi awali ‘**ku**-’ ambacho husimamia kitendo. Vitenzi hivi ni ‘**kubali**’ na ‘**mmalizia**’. Hili kosa la kudondosha kiambishi ‘**ku-**’ katika kitenzi kikuu baada ya kitenzi kisaidizi ‘**weza**’ ni maarufu sana kwa wasemaji wengi wa Kiswahili. Watu wengi huzoea kuzungumza hivyo na kwa sababu hiyo wanapoandika hudondosha kiambishi hiki. Ili tungo hizi ziwe sahihi kisarufi ni lazima vitenzi viwe ‘**kukubali**’ na ‘**kummalizia**’.

Katika tungo 45a, kitenzi kishirikishi ‘**na**’ kimechukua umbo lenye mzizi ‘**-ko**’ (ako) na katika umoja wa ngeli ya A – WA ‘**yu-**’ huambishwa mwanzoni. Badala yake, kiambishi cha ngeli A –WA katika umoja kimetumiwa katika tungo ya mwanafunzi kwa kuandika ‘**-ako**’. Katika mfano wa 42a, kuna kiambishi ‘**m-**’ katika mzizi huru ‘**hasidi**’ ambayo ni nomino katika ngeli ya A – WA umoja. Hii ni nomino inayoundwa kutokana na kitenzi ‘**husudu**’ na kwa hivyo haistahili kuambishwa ‘**m-**’ katika kuunda nomino. Kanuni ya kuunda nomino kutokana na vitenzi kwa kuweka ‘**m-**’ kwenye mzizi wa kitenzi inahusu vitenzi vyenye asili ya Kibantu kama inavyodhihirika katika mifano ifuatayo:

| **Kitenzi** | **Nomino** |
|---|---|
| lia ------------------------------------- | mlio |
| laza ------------------------------------ | mlazo |
| saka ----------------------------------- | msako |
| tembea -------------------------------- | mtembezi |

Kuambisha ‘**m-**’ katika ‘**hasidi**’ kuunda nomino kumeathiriwa na utaratibu wa kuambisha ‘**m-**’ kiholela. Katika 55a, nomino ‘**kiketi**’ imeundwa kwa kuweka kiambishi ‘**ki-**’ katika kitenzi ‘**keti’** kumaanisha kifaa cha kukalia. Ingawa kuna nomino ‘**kikalio**’ kutokana na kitenzi ‘**kalia**’ yaani, kifaa cha kukalia, na kuna uhusiano wa karibu wa maana baina ya ‘**kalia**’ na ‘**keti**’, ‘**kiketi**’ sio nomino kubalifu katika Kiswahili sanifu. Matumizi ya ‘**kiketi**’ ni athari ya matamshi ya Kibukusu kutokana na kutafsiri neno ‘**kiti**’. Katika Kibukusu ‘**kiti**’ huitwa ‘***sisala***’ ambapo ‘**si-**’ ni kiambishi kinachoonyesha umoja na ni sawa na **‘ki**-’ ya Kiswahili sanifu. Kwa kuelewa jambo hili, wanafunzi waliambisha ‘**ki**-’ katika kitenzi ‘**keti**’ ambacho kina maana sawa na kitenzi ‘**kaa**’ ili kuleta maana ya ‘kile cha kukalia’ na matokeo yake yakawa ‘**kiketi**’. Katika mfano huu, tumeona kwamba wanafunzi wanafanya makosa kwa sababu ya kuhamisha kanuni za lugha ya kwanza na kuziingiza katika Kiswahili.

### 5.7.2 Makosa ya uambishaji: vitabu vya kiada

Katika sehemu hii tunajadili makosa yaliyotokana na kuacha viambishi vinavyostahili kuwepo katika neno au kuongeza viambishi katika maneno. Matukio yote mawili yalisababisha makosa katika tungo inayohusika. Viambishi hutekeleza majukumu ya kisarufi na kwa hivyo kuongezwa kwake pasipostahiki katika neno au kudondoshwa pale panapostahiki, husababisha makosa ya kisarufi katika tungo husika. Ifuatayo ni mifano ya tungo zenye makosa yanayohusiana na uambishaji kutoka VVK:

14. a) Ni kwa nini Rehema **alilalamikia** Kombo? UWK uk. 54
16. a) Kwa kununua hisa za **makampuni** ya nje, serikali itauendeleza uchumi kwa vile itakuwa na kibali cha kufaidika kutokana na faida zinazopatikana kwa **makampuni** kama hayo. UWK uk. 102
3. a) **Unataka** mtu kupiga bongo na kujua ni vipi atamfurahisha rafiki. KK uk. 4
4. a) Hali hii **hunufaisha** wenye kuwaonea gere na wachochezi. KK uk. 4
6. a) **Ma**dawa chungu nzima yamegunduliwa na hospitali na zahanati zimejengwa kila sehemu ili wagonjwa watibiwe. KK uk. 17

Viambishi vilivyoachwa katika 14a UWK, 3a KK na 4a KK vinahusu warejelewa katika ngeli ya A – WA. Kwa mfano, katika 14a UWK, madhali Kombo atasikiliza lawama za Rehema basi ni lazima kiambishi '**m-**' kinachowakilisha mwathiriwa katika ngeli hiyo kitumike katika tungo. Kwa hivyo, usahihi wa kitenzi hiki katika muktadha ni '…Rehema ali**m**lalamikia Kombo'. Katika 4a KK, kwa sababu sentensi iko katika hali ya wingi, kiwakilishi cha urejeleo ni '**wa**' na kwa hivyo inafaa kuwa '… hu**wa**nufaisha wenye kuwaonea gere…' Hali hii ya kuweka kiwakilishi cha mtendwa katika kitenzi ni lazima katika ngeli ya A – WA. Kwa kutazama mifano ifuatayo inayohusisha ngeli nyingine tutatambua tofauti iliyopo:

1. Tutauza mahindi.
   dhidi ya
   Tuta**ya**uza mahindi.
2. Nimejibu swali.
   dhidi ya
   Nime**li**jibu swali.

Mfano mwingine ambapo ‘**ma-**’ imeambishwa kwenye mzizi ili kuunda nomino, unaonekana katika 16a UWK. Nomino ‘**kampuni**’na ‘**dawa**’ ziko katika ngeli ya I – ZI na kwa hivyo, umoja na wingi wake haubadiliki. Kuambisha ‘**ma-**’ ili kuonyesha wingi ni kosa. Kosa hili linafanana na makosa katika 33a na 49a MYW ambapo tuliona wakiambisha ‘**ma-**’ katika maneno ‘**dawa**’ na ‘**nguo**’ na kuishia kuwa na maumbo ‘**madawa**’ na ‘**manguo**’. Kufanyika kwa makosa haya ni tukio linalosababishwa na kuwepo kwa nomino nyingi katika Kiswahili ambazo huambishwa ‘**ma-**’ ili kuonyesha wingi wake. Nyingi kati ya nomino zenye hulka hii ya kuambishwa ‘**ma**-’ ni zile ambazo huanzia konsonanti katika umoja. Tukiangalia mifano ifutayo tunapata ithibati ya madai haya: shati, gari, jimbo, jembe, shamba, shaka, bunge, taifa na kadhalika. Katika mifano ya ‘**kampuni**’, ‘**dawa**’ na ‘**nguo**’ tunaona kwamba nomino zote zinaanzia konsonanti na kwa sababu ya kujumlisha kanuni ya kugeuza katika wingi kwa kuambisha ‘**ma**-’, makosa yametokea. Bila shaka waandishi wa VVK hivi wamepungukiwa na uelewa kuhusu vighairi katika lugha ambapo kanuni inayotumiwa katika muktadha fulani, hukosa kutumiwa katika miktadha mingine. Kila kanuni ina ukadirifu wake hivi kwamba hutumika katika baadhi ya miktadha. Haya ni makosa ambayo tunaweza kudai kwamba yamewaathiri wanafunzi hivi kwamba katika matamshi yao wanaiga makosa waliyoona katika vitabu. Kwa ujumla, katika sehemu hii tumeona kwamba kuweka viambishi visivyostahili au kuacha viambishi vinavyostahili kuwepo katika maneno ndiko kulikoleta hitilafu katika tungo zinazohusika.

### 5.8 Hitimisho

Katika sura hii, tumechambua aina mbalimbali za makosa ya kisarufi kama yalivyotokea katika MYW na VVK tukiongozwa na lengo la pili la utafiti yaani kuchambua makosa ya kisarufi yanayojitokeza katika MYW na VVK. Tumefafanua

makosa yaliyokuwa katika tungo hizo mbalimbali. Imedhihirika kwamba kulikuwa na makosa mengi ya kisarufi katika MYW na VVK kuliko makosa ya kitahajia. Kwa kuzingatia idadi ya makosa ya kisarufi katika VVK, tuligundua kwamba miongoni mwa vitabu vitatu tulivyohakiki, idadi kubwa ya makosa ya kisarufi ilitokea katika KF kikiwa na 51.5% ya makosa yote ya kisarufi katika vitabu vya kiada, kisha UWK kikawa cha pili na 25% na idadi ndogo sana ya makosa ikawa katika KK ambacho kilikuwa na 22.5% ya makosa yote ya kisarufi katika VVK. Vilevile, kwa jumla VVK vilikuwa na idadi kubwa ya makosa ya kisarufi kuliko yale yaliyokuwa katika MYW. Wanafunzi walifanya jumla ya makosa 53 dhidi ya yale ya VVK yaliyokuwa 62. Hii inatilia shaka utaratibu wa kuandaa na kukagua vitabu vya kiada kabla ya kuidhinishwa.

Aidha, tumeonyesha kwamba baadhi ya makosa ya kisarufi katika MYW yalikuwa sawa na yale yaliyokuwa ndani ya VVK na kuthibitisha kwamba wanafunzi wanaweza kuiga makosa yanapotokea katika vitabu vya kiada. Kwa kufanya hivi, tumedhihirisha athari za kuwepo makosa ndani ya VVK katika ujifunzaji sahihi wa lugha ya pili kwa wanafunzi wanaovitumia vitabu hivyo katika mafunzo yao. Kadhalika, kulikuwa na makosa mengine katika sarufi yaliyotokana na kuathiriwa na lugha ya kwanza ya wanafunzi. Licha ya kuwa katika jamiimseto ambayo ina jamii moja kubwa, wanafunzi waliendelea kufanya makosa ya kisarufi yaliyotokana na lugha yao ya kwanza wala sio jamii kubwa iliyo katika eneo la jamiimseto. Ili kuonyesha kwa kina visababishi vya makosa yote ya kitahajia na kisarufi katika MYW na VVK, tumetenga Sura ya Sita ambapo tumejadili vyanzo mbalimbali vya makosa haya.

# SURA YA SITA

# VYANZO VYA MAKOSA KATIKA MAANDISHI

## 6.0 Utangulizi

Sura hii inatathmini vyanzo vya makosa kwenye MYW na VVK kwa ajili ya kutimiza lengo letu la tatu katika utafiti huu. Katika kufanya hivi, tuliyashughulikia makosa kijumla bila kuyatenga katika zile aina mbili kuu tulizozingatia wakati wa kuyahakiki. Sehemu kubwa ya sura hii inaangazia asili za makosa yaliyotokea katika MYW. Hii ni kwa sababu ukweli ni kwamba maandishi rasmi, kama vile VVK, hayatarajiwi kuwa na makosa. Waandaaji wa vitabu vya kiada wanastahili kuwa kielelezo bora kwa wanafunzi wanaosoma vitabu vyao kwa kuhakikisha ya kwamba vitabu havina makosa kwani makosa huathiri ubora wa kazi rasmi na kutatiza uwasilishaji wa ujumbe. Aidha, athari zake katika shughuli ya mafunzo ni kubwa kwani wanafunzi hujifunza kwa kuiga yaliyo vitabuni wanaposoma. Kwa kweli tuligundua makosa katika VVK na kwa sababu hiyo tumejaribu kuonyesha sababu za kutokea makosa hayo vitabuni.

## 6.1 Sababu za Makosa katika Maandishi ya Wanafunzi

Chanzo kimojawapo cha makosa tuliyotambua ilikuwa ni athari za lugha ya kwanza ya wanafunzi. Uchunguzi wetu ulihusisha wanafunzi kutoka eneo la jamiimseto. Walengwa katika utafiti wetu walitoka katika jamii tano (5): Luhya, Luo, Kikuyu, Kalenjin na Teso miongoni mwa jamii za Kenya.

### 6.1.1 Makosa yaliyotokana na athari za lugha ya kwanza

Tuliweza kuyahusisha makosa na jamiilugha maalum kutokana na mifano ya majina ambayo walitaja kutoka jamii zao ndani ya zoezi la insha. Tuliyahusisha makosa ya

aina hii na Kiswahili kuingiliwa na lugha ya kwanza ya wanafunzi. Mengi ya makosa ya namna hii yalikuwa ni ya kitahajia.

#### 6.1.1.1 Makosa ya wanafunzi wa Kikalenjin

Baadhi ya makosa yaliyotokana na athari za Kikalenjin ni:

1. a) Nyumba **hile unatoa** moshi.
2. a) Hii ni **dhairi shairi** kwamba yule mtoto ana baraka nyingi sana.
3. a) Wanafunzi walikuwa na **aya** kuzungumza.
35. a) Kina mama **umpa** mtoto aliyezaliwa jina.

Mifano hii inadhihirisha kuwa wanafunzi Wakalenjin huchanganyikiwa kimatamshi ni wapi watumie na wasitumie kikwamizwa ghuna cha ufizi /**h**/. Kwa sababu hii, wanaichopeka isipofaa na pale inapofaa kuwekwa wanaidondosha. Katika mfano wa 1a, tunaona /**h**/ ikichopekwa katika '**hile**' badala ya kuandika neno '**ile**'. Katika tungo nyingine zote tunaona kwamba /**h**/ ilidondoshwa katika maneno yaliyokolezwa wino. Hili ni tatizo la kimatamshi miongoni mwa wanafunzi wa jamii ya Kikalenjin. Kiini kikuu cha kutokea kwa makosa ya kuchopeka au kudondosha '**h**' katika MYW wa Kikalenjin ni kutokuwepo kwa sauti hii katika fonolojia ya Kinandi na Kikipsigis kwa mujibu wa Toweett (1979). Kwa ajili ya kuthibitisha dai hili tulitafsiri sentensi tatu zifuatazo kwa usaidizi wa wasemaji asilia wa Kikalenjin:

1. a) Nyumba ile inatoa moshi.
   b) *Iyen koin.* (Kikipsigis)
   c) *Mong'u iyeto eng'koin*. (Kinandi)

2. a) Wanafunzi walikuwa na haya kuzungumza.
   b) *Kirenyegei lagokab sukul kong'alal*. (Kikipsigis)
   c) *Kimakokanye kipsimaninik kong'ololso*. (Kinandi)

3. a) Kina mama humpa mtoto aliyezaliwa jina.
   b) *Igochin kamatik kainet lakwet ne kagisiche.* (Kikipsigis)
   c) *Igochin chepyosok lakwet ne kagisich kainet*. (Kinandi)

Katika mifano hii yote hakuna mahali popote ambapo pana sauti /**h**/ katika Kikipsigis na Kinandi na kwa hivyo wanafunzi wa jamii hizi wanatatizika wanapokutana na

maneno yaliyo na sauti hizi. Vivyo hivyo, kwa kuelewa kwamba sauti hii hutumiwa katika Kiswahili wanajipata wakiipachika popote na matokeo ni kwamba wanakuwa na matumizi holela ya herufi **h** katika maandishi yao ya maneno ya Kiswahili ama kuipachika au kuidondosha.

Mfano mwingine wa kosa la hijai lililosababishwa na athari za Kikalenjin ulikuwa katika tungo ifuatayo:

9. a) Siku ya vijana kwenda **chondoni** wanapewa majina kama Maina.

Katika mfano huu neno, '**chondon**i' linastahili kuwa '**jandoni**' na kutokana na athari za matamshi ya Kinandi limeandikwa '**chondoni**'. Hili neno liliundwa kwa kuvuruga neno '**jandoni**' kisha likazoeleka kama neno la Kiswahili sanifu na hapo kuathiri MYW. Kijumla tunaweza kudai kwamba hata wanafunzi waliolitumia neno hili katika maandishi walidhani kwamba ni neno kubalifu katika Kiswahili.

### 6.1.1.2 Makosa ya wanafunzi Wakikuyu

Athari za jamii ya Kikikuyu zilidhihirika katika mifano ifuatayo:

13. a) Mgeni jana alikuja **jiani**.
14. a) Nilihisi **jaa** wakati wa shule.
15. a) Sisi kama Wakikuyu majina **hupokenzwa.**

Kama jamii za Kikalenjin zinavyokanganyikiwa katika kutumia /**h**/, ndivyo jamii ya Kikikuyu inavyokanganyikiwa katika kutambua ni lini watumie nazali. Kwa sababu hii, utawapata wanazidondosha kutoka mahali zinapofaa ziwe na kuzichopeka mahali zisipofaa kuwa. Tukitazama katika tungo 13a na 14a, nazali /**n**/ iliyohitajika kuwepo mwanzoni mwa maneno tuliyokoleza, ilidondoshwa katika MYW wa asili ya Kikuyu. Kwa upande mwingine, hiyo nazali ilichopekwa katika '**hupokenzwa**' kama inavyodhihirika kupitia 15a. Hili ni kosa ambalo lina chanzo chake katika matamshi ya wanafunzi. Mifano mingine ya maneno yaliyokuwa na makosa ya tahajia kutokana

na athari za lugha ya kwanza ya wanafunzi wenye asili ya Kikikuyu ni '**dunguye**' badala ya '**nduguye**', '**abaye**' badala ya '**ambaye**', '**kusund**i' badala ya '**kusudi**', '**mgojwa**' badala ya '**mgonjwa**' na hata mwingine aliandika jina '**Wajiru**' badala ya '**Wanjiru**'.

**6.1.1.3 Makosa ya wanafunzi wa Kiluo**

Wanafunzi kutoka jamii ya Luo walifanya makosa mengi ya kutenganisha. Wakati wa kuchanganua data yetu tuliwahoji wasomi ambao ni wasemaji asilia wa Kiluo. Tuligundua kwamba utenganishaji wa maneno ulitokana na lugha ya Luo ambayo katika kuandika maneno, viambishi hutenganishwa na mzizi. Tulipata tafsiri ya baadhi ya maneno na tungo za Kiswahili kwa Kiluo ili kuthibitisha hali hii kama inavyoonyeshwa katika mifano ifuatayo:

| **Kiswahili** | **Kiluo** |
|---|---|
| 1. a) tulipofika------------------------------- | b) *kane wachopo* |
| 2.a) unapozuru ---------------------------- | b) *soma ilimo* |
| 3. a) Maji yalijaa. -------------------------- | b) *Pii ne opong.* |
| 4. a) Walio macho wameona. ------------- | b) *Joma neno oneno*. Pia, *Jok man gi wang no neno.* |

Mifano hiyo inadhihirisha kwamba Kiluo ni lugha inayotawanya viambishi vya nafsi na wakati kutoka kwenye mzizi. Katika Kiluo, viambishi vya nafsi na wakati huwakilishwa na maneno huru. Huu mtawanyo husababisha mkanganyiko kwa wanafunzi wa Kiluo katika maandishi. Mifano ya tungo zenye makosa ni:

23. a) **Tulipo fika** nyumbani, tulivua nguo zetu.
24. a) **Tulipo zuru** mbuga ya Maasai Mara **tuli waona** wanyama.
26. a) Maji **yali jaa** hadi pomoni.

Makosa ya kutenganisha maneno yameonyeshwa kwa kukolezwa rangi. Kulingana na wanafunzi wenye asili ya Kiluo hayo ni maneno huru. Bila shaka makosa ya wanafunzi hawa ya kutenganisha yalitokana na kuathiriwa na lugha yao ya kwanza ambayo ni Kiluo. Kwa kuzingatia mifano kutoka jamii tulizotaja ukweli wa lugha ya

kwanza ya wanafunzi kuwa chanzo kikuu cha makosa katika maandishi yao ya Kiswahili sanifu unadhihirika. Tunaweza kudai kwamba lugha ya kwanza ya wanafunzi ina mchango mkubwa katika kusababisha makosa katika MYW.

#### 6.1.1.4 Makosa ya wanafunzi wa Kiteso

Utungo ufuatao unadhihirisha mfano wa makosa yaliyotokana na wanafunzi wa Kiteso:

44.a) Mwelimishe mwana huyu **manake** yeye ndiye kizazi **kijao**

Baada ya kuwahoji wasemaji asilia wa Kiteso walithibitisha kwamba msamiati mwingi wa Kiteso hauna irabu mwambatano. Kwa sababu hii matamshi ya wanafunzi wa Kiteso huathiri maandishi yao na kudondosha moja katika irabu mwambatano katika maneno ya Kiswahili.

#### 6.1.1.5 Makosa ya wanafunzi wa Kiluhya

Baadhi ya makosa yaliyotokea katika wanafunzi wa Kiluhya yalihusiana na kuchopeka viyeyusho baina ya irabu mbili zinapotokea katika maneno. Kwa sababau hii waliandika '**awache**' badala ya '**aache**' katika 17a. MYW na '**akataye**' badala ya '**akatae**' katika 19a. MYW. Kadhalika, wanafunzi wa Kiluhya walichopeka irabu '**u**' baada ya nazali '**m-**' kama inavyodhihirika katika 20a. MYW kwa kuandika '**ulimusaidia**' badala ya '**ulimsaidia**'.

Ili kukabiliana na makosa yanayotokana na matamshi mabaya, ni wajibu wa walimu kuwahusisha wanafunzi katika mazoezi mengi ya kusikiliza na kuzungumza ili waige matamshi bora. Kwa kusikiliza vielelezo vya matamshi bora, wanafunzi watayaiga na kusahihisha matamshi yenye dosari. Mathalani, kwa kuwashirikisha wanafunzi katika kutamka maneno katika jozi za mlinganuo finyu, vitanza ndimi na maigizo,

wanafunzi watajenga mazoea ya kutamka vizuri maneno na kwa njia hii wataweza kuyaandika maneno hayo vizuri.

### 6.1.2 Makosa yanayotokana na vitabu vya kiada

Baadhi ya makosa katika MYW yalitokana na atahri za VVK. Hivi ni vitabu wanavyotumia katika mafunzo yao. Kulikuwa na makosa mbalimbali yaliyofanana na yale yaliyokuwa katika baadhi ya VVK na hii ni ithibati kwamba wanafunzi waliiga makosa waliyoona katika vitabu vyao. Hapa tunarejelea baadhi ya mifano ya makosa ya aina hii:

6. a) **Madawa** chungu nzima yamegunduliwa … KK uk. 17
33. a) **Madawa za** kulevya hudhuru afya zetu. MYW

6. a) Kupitia kwa ufahamu, mwanafunzi anafundishwa **jinzi** ya kupanua msamiati wake na hata nyenzo za kujieleza. UWK uk.19
45. a) Huweza kufunzwa na kuelezewa **jinzi** wanavyoweza kumtunza mwana. MYW

8. a) …mawingu yanaashiria kukaribia kwa mvua **kunyesha**. KK uk. 32
61. a) Akizaliwa mvua **u**likuwa **unanyesha**. MYW

24. a) Usingizi wa kutosha **huupatia** mwili nguvu. KK uk. 222
24. a) Ni lazima shangazi wa mtoto kuja **kumpatia** jina. MYW

16. a) Kwa kununua hisa za **makampuni** ya nje… UWK uk.10
49. a) Mama alifua **manguo**. MYW

Kila jozi ya tungo katika jozi hizo tano inatangulia kwa kuonyesha kosa katika kitabu cha kiada na pili ni mfano wa kosa katika MYW linalofana na lile la kwanza katika jozi. Kutokana na kufanana kwa namna hii, hakuna jinsi tutaepuka kuhusisha asili ya makosa haya na VVK. Ni dhahiri kwamba wanafunzi wameiga makosa kutoka VVK.

Makosa mengine yaliyosababishwa na athari za VVK yalihusu kuunganisha maneno kama tunavyoonyesha katika mifano hii:

28. a) Mtoto **watatu** huitwa upande wa mama. MYW
31. a) Nyanya zao walioaga dunia au **waliohai**. MYW

34. a) Jina lile linatumika kwa mtoto **wakiume** na Nasimiyu kwa mtoto **wakike**. MYW
25. a) Haki za binadamu **zakulinda** maisha zina mipaka gani? KF uk. 147
32. a) Mawazo yote yaegemee **nani** lazima yaingiliane na kifungu hicho. KF uk.179
44. a) Wapaze sauti dereva akikiuka **sheriaau** polisi wanapokosa kuwashtaki wenye hatia. KF uk. 206

Bila shaka makosa yanayotokea katika maandishi haya yanaonyesha kwamba wanafunzi wanafanya makosa kwa kuiga namna VVK vinavyoandikwa. Sababu inayowafanya kuiga makosa yaliyo kwenye VVK ni kwamba vitabu ndivyo hazina ya kimsingi ya makala wanayosoma na ni nyenzo muhimu katika mchakato wa kujifunza. Mradi mwanafunzi ameyaona katika vitabu ataamini kwamba ni ukweli na kwa hivyo atayaiga katika matumizi yake ya lugha.

### 6.1.3 Makosa yanayotokana na ujumlishaji unaopita kiasi

Ujumlishaji unaopita kiasi ulikuwa sababu nyingine ya makosa ya kimaandishi katika kazi za wanafunzi. Katika muktadha huu, ujumlishaji unaopita kiasi ni utumiaji wa kanuni zinazohusu muktadha tofauti katika muktadha usiofaa. Hii ni sawasawa na kuhamishia kanuni mahali pasipostahili. Kwa kutazama mifano ifuatayo ya kutenganisha maneno, tutaona jinsi ujumlishaji unaozidi kiasi unavyosababisha makosa:

23. a) **Tulipo fika** nyumbani, tulivua nguo zetu.
24. a) **Tulipo zuru** mbuga ya Maasai Mara, **tuli waona** wanyama.
26. a) Maji **yali jaa** hadi pomoni.

Utenganishaji unaodhihirika hapa unatokana na kujumlisha ile kanuni ya kuandika kitenzi kishirikishi kikamilifu ambacho mzizi wake hauko dhahiri kama tulivyoonyesha hapa chini:

1. Simu **ina** mjazo.
2. Gari **lina** magurudumu mapya.
3. Mgeni **ana** pikipiki.

Katika tungo hizi, tunaona kwamba vitenzi vilivyokolezwa wino ni maneno huru. Ni huku kutenganisha vitenzi vishirikishi vyenye mizizi fiche na nomino inayoshirikishwa navyo kunakowafanya wanafunzi kujumlisha kanuni hii kwa kutenganisha neno lisilopaswa kutenganishwa kwa kuwa hivyo ni viambishi wala sio vitenzi. Kwa mujibu wa wanafunzi katika mfano 23a, '**tulipo**' ni kitenzi kama ambavyo '**ina**', '**lina**' na '**ana**' vilivyo katika mifano 1, 2 na 3. Huku ndiko kujumlisha kanuni ambayo inahusu muktadha tofauti na kuitumia katika muktadha mwingine. Matokeo yake ni kuwa na tungo zenye makosa. Jambo hili linaweza pia kurejelewa kama kuwa na maarifa nusu kuhusu dhana fulani katika lugha.

### 6.1.4 Makosa yanayotokana na athari za kijamii

Baadhi ya makosa katika MYW yalitokana na athari za kijamii. Wanafunzi waliiga mitindo ya lugha iliyozoeleka na wanajamii kiasi cha kudhaniwa kuwa sahihi. Hebu turejelee mifano ifuatayo ya makosa:

11. a) Mtoto wake wa kwanza akiwa **kijana** anaitwa Wanjohi.
38. a) Mbona **haunithamini**?
45. a) Wa kwanza kutoka **ako** na jina binafsi.
57. a) Hufanya karamu ya kufana ili **kumpea** mtoto jina.

Kwa kuzingatia kila mfano, tunagundua kwamba maumbo yaliyokolezwa ni maarufu sana na ni rahisi kusikika kutoka kwa watu. Si ajabu walimu wa Kiswahili kusikika pia wakitumia lugha jinsi hii. Kwa mfano, neno '**kijana**' hutumiwa na watu wengi kurejelea jinsia ya kiume. Kwa sababu hiyo, wanafunzi waliotumia neno hili walikuwa wanalenga maana hiyo. Aidha, watumiaji lugha wengi wanapokanusha nafsi ya pili katika umoja, hutumia viambishi '**hau-**' badala ya '**hu-**' na ndiyo maana wanafunzi wakatumia '**haunithamini**' badala ya '**hunithamini**'.

Kadhalika, umbo '**ako**' hutumiwa na watu wengi katika maongezi yao bila kujua kwamba hili sio neno katika Kiswahili sanifu. Nacho kitenzi chenye shina la silabi

moja ‘**-pa’** hunyambuliwa katika kauli ya kutendea na wanajamii wengi kwa namna inayodhihirika katika tungo 57a yaani ‘**pea**’ na hili ni kosa. Tunaweza kudai kwamba athari za jamii ni sababu ya wanafunzi kufanya makosa katika maandishi. Wanafunzi hujifunza kutoka kwa yale wanayosikia kwa wengine.

### 6.1.5 Makosa ya ulegevu wa kujiandaa

Makosa mengine yanadhihirisha kwamba wanafunzi wana ulegevu katika kujiandaa. Sababu za maandalizi duni zinaweza kutokana na wanafunzi kutokuwa na mazoea ya kusoma kwa mapana ili kustawisha hazina ya msamiati. Mwanafunzi mwenye mazoea ya kusoma kwa mapana, hususan vitabu vya fasihi, huwa na nafasi nzuri ya kustawisha hazina yake ya msamiati na kuelewa matumizi yake sahihi. Mwanafunzi kama huyu huwa na ufahamu wa maneno mengi ya kawaida na hatarajiwi kuyatumia kwa njia isiyofaa. Makosa mengi yaliyohusiana na matumizi mabaya ya maneno yanaweza kuwa ishara ya wanafunzi kukosa kusoma kwa mapana.hii ni baadhi ya mifano maneno.

Mifano ni kama ifuatayo:

18. a) Mbwa alibweka **mchana kucha**.
20. a) Njaa **imetanda** nchini.
56. a) Hasa **mila** yangu huwa wanafanya sherehe kubwa sana.

Maneno yaliyokolezwa wino ni msamiati wa kawaida sana na mwanafunzi wa kidato cha pili hatarajiwi kutatizika katika kuelewa maana yake. Mathalani, katika kusisitiza kielezi cha wakati ‘**mchana**’ tunatumia ‘**kuchwa**’ au ‘**kutwa**’ wala sio ‘**kucha**’. Aidha, neno ‘**tanda**’ huhusiana na giza wala sio ‘**njaa**’. Kadhalika, kukosa kutofautisha maana ya neno ‘**mila**’ na ‘**jamii**’ ni ukosefu wa wanafunzi kusoma kwa mapana. Ni sharti wanafunzi wahimizwe kusoma vitabu vingi katika kidato cha kwanza na pili kama njia moja ya kuwawezesha kupanua hazina yao ya msamiati. Walimu wana wajibu wa kuhakikisha kuwa wanafunzi wana vitabu vya mazoezi ya

kusoma tangu wanapojiunga na kidato cha kwanza ili wapate matini mbalimbali za kusoma.

Mifano mingine ya makosa ya sarufi, hasa yale yanayohusiana na upatanisho wa kisarufi usiokubalika kwa mujibu wa ngeli, yanaashiria kwamba wanafunzi hawajaandaliwa vyema. Ngeli ndio msingi wa sarufi ya Kiswahili na mwanafunzi yeyote ambaye hajamudu ngeli hatakuwa na umilisi wa sarufi ya Kiswahili. Makosa ya aina hii yalikuwa mengi na tunanakili baadhi yake katika kudhihirisha kuwa kuna maandalizi duni kwa wanafunzi:

17. a) Ugali na mboga ni **tamu**.
25. a) Kuni **hii ina** moshi.
28. a) Kucha za vidole **zake** ni ndefu.
29. a) Darasa **iliyojaa** wanafunzi **imebomoka**.
32. a) Kitu kingine **ambayo tunayafuatilia** ni ile saa ya kuzaliwa.
36. a) Moshi **tuliyoiona** jana **ilionyesha** kuchomeka kwa nyumba.
50. a) Mvuvi alivua samaki **nyingi**.

Makosa yote yanayotokea katika tungo hizi yana msingi wake katika ngeli na yanathibitisha kwamba maandalizi ya wanafunzi katika ngeli ni duni. Kwa kutoelewa ngeli za nomino wanashindwa kuzipatanisha kisahihi katika vitenzi na vivumishi. Kuna haja ya kutilia maanani mafunzo ya ngeli za nomino kwa upande wa walimu kwa kubuni mikakati ya kuwaelekeza wanafunzi wamakinike katika ngeli na kuepukana na makosa ya aina hii.

### 6.2 Vyanzo vya Makosa katika Vitabu vya Kiada

Kwa vile vitabu ni maandishi rasmi, havitarajiwi kuwa na makosa. Makosa tuliyopata katika vitabu tulivyochunguza yanaweza kuhusishwa na sababu mbalimbali. Asili mojawapo ya makosa haya ni waandishi wa vitabu hivyo. Kampuni za uchapishaji wa vitabu hujichagulia zenyewe walimu wanaotumiwa katika kuandika vitabu. Hata hivyo, baadhi ya makosa yaliyotokea vitabuni yanazua shaka kuhusu weledi wa

waandishi waliotumiwa na kampuni husika katika kuandika vitabu husika. Hebu tuchunguze mifano ifuatayo iliyopatikana katika VVK:

a) Kila mmoja wao aliulizwa kama **ikiwa** angepelekwa kuishi peke yake kwenye kisiwa na kuruhusiwa kubeba kitu kimoja tu, angebeba nini? UWK uk. 8

5. a) … lazima mtu abuni **kuhusu** mambo ambayo anatambua vyema…UWK uk. 9

34. a) Maana ya muhtasari ni kuandika kwa **kifupi**. UWK uk.169

14. a) Kisha mkutano ulijadili kwa **kirefu** hoja baada ya hoja mpaka wanachama wakaafikiana. KK uk. 51

27. a) kuanzia insha kwa utangulizi wenye kuvutia (sio kamilifu) KK uk. 27

8. a) Wanafunzi **wanasoma** darasani. KF uk.75

9. a) Husimulia mambo kwa **kirefu** ikitumia lugha ya mjazo na yenye mchanganyiko wa visa, matukio, mazingira na wahusika. KF uk. 79

24. a) Birika **ingali ina** chai. KF uk.145

Makosa yote yaliyo katika tungo hizi hayatarajiwi kutokea katika kazi za kitaalamu ambazo zimeandaliwa na jopo la waandishi kama waliohusishwa katika kuandika vitabu vitatu tulivyochunguza. Kulingana na habari zilizo ndani ya kila kitabu, kila kitabu kilikuwa na idadi ifuatayo ya wanajopo walioshiriki katika kukiandika: UWK wawili (2), KK sita (6), na KF wanne (4). Uwezekano upo kwamba baadhi ya waandishi wa vitabu hivi ama ni wanahisa au wamiliki wa kampuni za uchapishaji wa vitabu vyenyewe na kwa hivyo hawahusishi wataalamu wengine katika uandishi wa vitabu vyao kwa kuhofia gharama itakayopunguza faida yao. Aidha, kuna uwezekano kwamba kampuni hazijali sana weledi wa wanajopo na kwa hivyo zinaishia kuteua walimu ambao hawana umilisi wa kutosha katika sarufi ya Kiswahili. Huenda vilevile, uteuzi wa wanajopo ukawa unategemea mambo mengine kama vile uhusiano na kujuana na wakuu katika kampuni na matokeo yake yakawa kuteua walimu ambao hawana ujuzi wa lugha na wakaishia kufanya makosa katika kazi zao. Katika harakati zao za kupunguza gharama ya uzalishaji, machapisho ambayo yanatokea yanakuwa na shehena ya makosa yanayoathiri watumiaji wake.

Makosa mengine katika VVK yana asili yake katika uhariri. Kulikuwa na makosa ambayo yalifaa kuondolewa wakati wa uhariri wa miswada ya mwisho kabla ya kuchapishwa. Ikiwa wahariri wangefanya kazi yao kwa uangalifu basi, makosa haya hayangehusishwa nao ila wapiga chapa. Tunaorodhesha baadhi ya makosa haya:

2. a) **vivumushi** KF uk. 7
10. a) Katika kidato cha kwanza tulieleza maana ya maktaba kuwa mahali ambapo pana vitabu, majarida, nakala mbalimbali na **magezeti** ya kusoma. KK uk.37
20. a) Nilikuwa ninaamini kwamba ni bora kila mtu **ajishuhulishe** na mambo yake bila kujali wengine hadi yaliponipata yaliyonipata. UWK uk. 104
21. a) Tulipaswa kulilia purukushani zetu na **mapuza** yetu. UWK uk. 104
25. a) Haki za binadamu **zakulinda** maisha zina mipaka gani? KF uk. 147
29. a) Walilima mashamba ya wazazi wao, kuenda mtoni na hata **katafuta** kuni kwa pamoja. KF uk. 164
30. a) Majizi yaliyokamatwa yatafikishwa **mahakani** kesho. KK uk. 255
32. a) Kijiji kizima kilipigwa na **butwa** wakati Zawadi alipotimuliwa kutoka kwa kishamba alichohalifu mumewe. UWK uk. 166

Katika tungo hizi maneno yote yaliyokolezwa yamesheheni makosa ambayo yalifaa kushughulikiwa katika hatua ya kuhariri au kupiga chapa. Imedhihirika kwamba kila kitabu kina makosa ya aina hii na ikumbukwe kwamba tumenakili mifano hii michache tu ili kuonyesha hali halisi ya ukosefu wa umakinifu kwa wale waliopewa jukumu la kuhariri na kupiga chapa miswada ya mwisho ya VVK. Kwa hakika, makosa haya hayawezi kuwa na chanzo chake kwa waandishi wa vitabu kwa sababu yanahusiana na kudondosha au kubadilisha herufi katika maneno. Makosa mengine ni ya kuunganisha maneno mawili ili kuwa neno moja.

Kijumla makosa ya aina hii yanaweza kuwa yanatokana na kukosa kuwa makini wakati wa kushughulikia mchakato mzima wa maandalizi ya VVK. Ukosefu wa makini unaweza kuwa zao la kuwa na haraka katika shughuli nzima ya uandalizi wa vitabu kwa kutaka kujinufaisha na mapato ya kuuzia soko kubwa ikiwa ni pamoja na

shule, wazazi na wanafunzi. Kwa sababu ya kuwa na soko lililo tayari la bidhaa zao, wahusika wanakuwa na haraka ya kutayarisha vitabu vyao ili wawe wa kwanza kuwasilisha bidhaa zao kwa wanunuzi.

Kwa kuelewa kwamba kuna utaratibu wa kuidhinishwa kwa machapisho ya shule kabla ya kutumiwa katika mafunzo, tunaweza kudai kuwa utepetevu katika idara inayohusika na ukaguzi wa vitabu vya mafunzo shuleni umechangia kuwepo kwa makosa katika machapisho ya shuleni. Shughuli hii hutekelezwa na Taasisi ya Ukuzaji wa Mitaala nchini Kenya (KICD). Ingawa taasisi hii sio chanzo cha makosa katika machapisho ya kiada lakini inastahili kulaumiwa kwa ukosefu wa uwajibikaji. Jukumu la kutambua kasoro hizi katika vitabu hivi liko chini ya taasisi hii. Kuwepo kwa makosa katika machapisho yaliyoidhinishwa ni ishara kwamba hakukuwa na uwajibikaji kwa wale wanaopaswa kusoma nakala zinazowasilishwa kwao kwa ukaguzi. Kwa hivyo, wale walio na wajibu wa kutambua kasoro kwenye vitabu ili zirekebishwe wamezembea katika kazi yao na kwa njia hii kuruhusu machapisho yenye makosa kuwafikia watumiaji. Ama kwa hakika, ishara zinaonyesha kwamba huenda hata vitabu hivi havikusomwa kabisa na wakaguzi ili kuchunguza viwango vya makosa yaliyo ndani yake.

Ikumbukwe kwamba vitabu vinavyoshindwa kutimiza masharti ya ukaguzi havifai kusambazwa sokoni kwa sababu vinaathiri watumiaji miongoni mwao wakiwa wanafunzi. Hakuna hatua zozote zinazochukuliwa na taasisi ya KICD na Wizara ya Elimu ili kuzuia usambazaji wa vitabu vyenye makosa. Kwa hivyo wauzaji wasiojali athari zake kwa jamii wanapata uhuru wa kuuza bidhaa zao kwa wananchi wasio na habari na kwa njia hii wanaendelea kuzorotesha viwango vya lugha nchini. Kijumla,

kuna ishara ya ukosefu wa kuwajibika katika utenda kazi katika Taasisi ya Ukuzaji wa Mitaala nchini Kenya na Wizara ya Elimu.

### 6.3 Hitimisho

Katika sura hii, tumetathmini vyanzo mbalimbali vya makosa ya kitahajia na kisarufi katika MYW na VVK kwa mujibu wa lengo la tatu la utafiti wetu. Kwa ujumla, tumeonyesha kwamba makosa katika MYW yanatokana na maandalizi duni ya wanafunzi, udhaifu wao wenyewe na athari kutoka kwa wanajamii. Muhimu zaidi, tumeonyesha kwamba makosa mengine katika MYW yanatokana na VVK wanavyosoma ambapo wanaiga mambo yaliyoandikwa vitabuni kwa kutojua kwamba wanayoiga ni makosa katika lugha.

Kuhusu vyanzo vya makosa yaliyo katika VVK, tumedhihirisha kwamba ni matokeo ya udhaifu mkubwa katika mfumo mzima wa maandalizi ya vitabu hivi. Tumeweka wazi hoja kwamba kuna makosa yanayotokana na ukosefu wa uwajibikaji katika mfumo mzima wa uandalizi na uidhinishaji wa VVK. Kila mhusika katika uandalizi wa VVK amechangia kuwepo kwa makosa katika VVK. Baada ya kukamilisha utafiti wetu na kuwasilisha maoni yetu, katika Sura ya Saba tunatamatisha tasnifu yetu kwa kutoa mahitimisho, kuonyesha mchango wa utafiti wetu na kutoa mapendekezo ya utafiti.

# SURA YA SABA

# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI

## 7.0 Utangulizi

Baada ya kumaliza utafiti wetu na kutuwezesha kufikia maamuzi tuliyojadili katika sura chambuzi, tunahitimisha tasnifu yetu kwa kutoa maelezo mafupi kuhusu tasnifu hii. Tumetumia fursa hii kutoa maelezo machache kuhusu makosa tuliyoshughulikia katika utafiti wetu na kuwakilisha idadi ya makosa yalitokea katika MYW na VVK kutumia idadi na asilimia kwa kuzingatia jumla ya makosa katika kila kitengo na idadi ya kurasa kwenye VVK. Hatimaye tumedokeza mchango wa utafiti wetu na kupendekeza mada nyingine zinazoweza kufanyiwa utafiti baadaye.

## 7.1 Muhtasari wa Tasnifu

Katika utafiti wetu tulijishughulisha na kuhakiki makosa ya kitahajia na kisarufi katika MYW wa shule za upili zilizo katika eneo la jamiimseto na kutambua asili mbalimbali za aina hizi za makosa. Aidha, tulihakiki aina hizi za makosa katika baadhi ya VVK. Tulikusanya data kutoka katika MYW kupitia mazoezi matatu ya viasho, jozi za mlinganuo finyu na kuandika insha. Mazoezi haya yalifanywa na wanafunzi wa kidato cha pili walioteuliwa kutoka katika shule 9 za upili katika Kaunti Ndogo ya Likuyani, Kaunti ya Kakamega. Ili kupata data za makosa katika VVK, tuliteua vitabu vitatu vya wanafunzi kutoka kampuni tatu za uchapishaji. Kampuni hizi ni Moran Publishers, Oxford University Press na Kenya Literature Bureau. Kati ya vitabu hivi, kimoja kilikuwa cha wanafunzi wa kidato cha kwanza na viwili vya wanafunzi wa kidato cha pili. Aidha, kati ya vitabu hivi, viwili vilikuwa ni vile vilivyoidhinishwa na Wizara ya Elimu nchini Kenya kupitia Taasisi ya Ukuzaji wa Mitaala Nchini (KICD) ilhali kimoja hakikuwa kimeidhinishwa na wizara hii. Utafiti huu ulichochewa na makosa mengi yanayofanywa na wanafunzi katika

mitihani yao ya Insha (Karatasi ya Kwanza) na Lugha (Karatasi ya Pili) ya K.C.SE. Makosa haya yanachangia kudorora kwa matokeo ya wanafunzi katika somo la Kiswahili katika Mtihani wa Kitaifa wa Kidato cha Nne (K.C.S.E.) katika kaunti ndogo ya Likuyani.

Ili kuafikia malengo ya utafiti huu tuliongozwa na Nadharia ya Uchanganuzi wa Makosa. Nadharia hii ilitusaidia kufuatilia malengo yetu kwa kuchambua data ambayo tulikusanya na sasa hapa chini tunahitimisha tuliyogundua kutokana na kila lengo. Hatimaye tumejaribu kutathmini vyanzo mbalimbali vya makosa katika MYW na VVK.

### 7.2 Hitimisho la Utafiti


Katika sehemu hii tumehitimisha utafiti wetu kwa kuzingatia malengo yetu matatu ya utafiti. Kwa kuongozwa na kila lengo, tumeonyesha jinsi tulivyochambua kila aina ya kosa katika sura yake tukianza kwa makosa katika MYW kisha makosa katika VVK. Kuhusu makosa katika VVK, tumehitimisha kwa kutumia takwimu kulinganisha katika MYW na VVK.

#### 7.2.1 Makosa ya kitahajia

Tulichambua data mahsusi kwa kufuatilia lengo la kwanza kama lilivyo chini ya 1.3 kuhusu makosa ya kitahajia katika sura ya nne. Makosa katika MYW yalidhihirika kwa namna mbalimbali kama vile kudondosha, kuchopeka na kubadilisha herufi katika maneno. Makosa mengine ya kitahajia yalijionyesha kwa kutenganisha neno na kuunganisha maneno tofauti. Makosa ya kudondosha herufi yalikuwa mengi zaidi ya aina zingine za makosa ya hijai yakiwa 15, kuongeza herufi mara 12 huku kuunganisha maneno yakitokea mara 8. Kutenganisha maneno na kuchopeka herufi kila aina kulitokea mara tanotano.

Makosa ya kutenganisha neno yalikuwa mengi katika vitenzi kuliko aina nyingine za maneno pengine kwa sababu vitenzi vina utajiri mkubwa wa uambishwaji. Kijumla, makosa ya kitahajia katika MYW yaliashiria kwamba matamshi ya wanafunzi yaliathiriwa na lugha yao ya kwanza. Kadhalika, tulitambua kwamba VVK vilikuwa na makosa ya kitahajia. Aidha, uchambuzi wetu wa kina ulidhihirisha kwamba makosa mengine ya kitahajia katika MYW yalifanana na yale yaliyokuwa katika VVK. Hii ni ithibati kwamba baadhi ya wanafunzi hufanya makosa ya kitahajia kwa kuiga maandishi katika VVK.

Miongoni mwa VVK, KF kilikuwa na jumla ya makosa kumi (10) ya kitahajia (47.6%) kisha kikafuatiwa na UWK (kimeidhinishwa) kilichokuwa na makosa tisa (9) (42.8%). KK kilikuwa na makosa mawili (2) ya kitahajia (9.6%). (Taz. mchoroduara 7.1)




**Mchoroduara 7.1: Ulinganishaji wa makosa ya hijai katika VVK**
*Asili: Uhakiki wa mtafiti*

Makosa ya kudondosha herufi ndiyo yalikuwa na uwakilishi mwingi katika VVK huku kitabu cha UWK kikiongoza kwa wingi wa makosa ya kudondosha herifi katika maneno. Kuwepo kwa makosa katika VVK kunaonyesha udhaifu wa waandaaji wa

VVK. Hususan, makosa ya kitahajia katika vitabu ni ushahidi tosha kwamba kuna ukosefu wa uwajibikaji katika hatua za uhariri na upigaji chapa katika kampuni za kuchapisha vitabu. Ni katika hatua hizi ambapo miswada husafishwa kwa kuondoa makosa ya kitahajia ili machapisho yanayotolewa yasiwe na dosari za aina hii.

### 7.2.2 Makosa ya kisarufi

Kwa kufuatilia lengo la pili la utafiti, tulichambua data mahsusi yenye makosa ya kisarufi katika MYW na VVK katika sura ya tano. Makosa mengi yalikuwa ni ya kisafufi katika MYW na VVK. Makosa ya kisarufi yalichambuliwa katika vitengo vifuatavyo: kudondosha maneno, kuchopeka maneno, upatanisho wa kisarufi, minyambuliko isiyokubalika na uambishaji wenye makosa. Katika uchanganuzi wetu tuligundua kwamba wanafunzi walifanya makosa mengi yaliyohusiana na upatanisho wa kisarufi kuliko aina nyingine za makosa ya kisarufi. Idadi ya utukiaji wa makosa ya kisarufi katika MYW ilikuwa; upatanisho mara 20, kuchopeka maneno na uambishaji mara 15 kila moja. Makosa ya mnyambuliko yalikuwa saba (7) katika MYW na ndiyo yalikuwa machache zaidi miongoni mwa makosa ya kisarufi. (Taz. Jedwali 7.1)

**Jedwali 7.1 : Makosa ya kisarufi: Utukiaji katika MYW**


| Kuchopeka neno | Kudondosha neno | Mnyambuliko | Upatanisho | Uambishaji |
|---|---|---|---|---|
| 15 | 10 | 7 | 20 | 15 |

*Asili: Uhakiki wa mtafiti*

Makosa ya upatanisho yanahusu ngeli za nomino. Kutokana na sababu kwamba ngeli ndio msingi wa sarufi ya Kiswahili, wingi wa makosa ya aina hii ni ishara kwamba walimu wana jukumu la kuimarisha mafunzo yao kuhusu mada ngeli ili wanafunzi waepuke kufanya makosa ya kisarufi. Makosa ya wanafunzi kuhusu upatanisho wa


kisarufi yalihusu zaidi ngeli za U - ZI, I - I, KI – VI, na LI – YA. Mafunzo yatilie maanani hizo ngeli. Mafunzo bora yataimarisha utendaji wa wanafunzi na katika mitihani ya kitaifa.

Kutokea kwa makosa ya upatanisho wa kisarufi katika VVK ni jambo la kushangaza sana kwa sababu ngeli za nomino ni dhana ya kimsingi na ni muhimu sana katika sarufi ya Kiswahili. Maandalizi ya VVK yanastahili kushirikisha umakinifu mkubwa. Miongoni mwa vitabu vitatu tulivyohakiki, KF kiliongoza kwa wingi wa makosa ya upatanisho kwa kuwa na jumla ya makosa tisa (71%) kisha UWK kikawa na makosa matatu (22%) na KK kikawa na kosa moja (7%). ( Taz. mchoroduara 7.2)




**Mchoroduara 7.2: Ulinganishaji wa makosa ya kisarufi katika VVK**
*Asili: Uhakiki wa mtafiti*

Baadhi ya makosa yaliyojitokeza katika VVK yalipatikana katika MYW na hii ni ishara kwamba huenda wanafunzi waliyaiga makosa katika VVK. Idadi kubwa ya makosa ya kisarufi katika VVK ilihusu uchopekaji wa maneno katika tungo. Idadi ya makosa katika kila kitabu iliwakilishwa ifuatavyo: KF 17 (50%), UWK 10 (29.5%), na KK 7 (20.5%). (Taz. mchoroduara 7.3)




**Mchoroduara 7.3: Ulinganishaji wa makosa kijumla katika VVK**
*Asili: Uhakiki wa mtafiti*

### 7.2.3 Vyanzo vya makosa

Hatimaye, kwa kuzingatia lengo la tatu, tulitathmini vyanzo mbalimbali vya aina ya makosa ya kitahajia na kisarufi kama yalivyodhihirika katika MYW na VVK katika sura ya sita. Kwa jumla, tulibaini kwamba vyanzo vya makosa katika MYW vilikuwa mbalimbali. Kulikuwa na makosa ambayo yalitokana na athari za lugha ya kwanza ya wanafunzi yaliyodhihirika kwa njia ya tahajia ambapo wanafunzi walishindwa kutofautisha vitamkwa ghuna na sighuna katika maandishi yao. Makosa ya namna hii yanaweza kukabiliwa kwa kuwapa wanafunzi mazoezi ya imla mara kwa mara ili watofautishe aina hizi mbili za sauti. Kadhalika, matumizi ya nyimbo na mashairi yaliyo na maneno yanayotatanisha yatawasaidia wanafunzi kufanya mazoezi ya matamshi bora.

Makosa mengine yaliyofanywa na wanafunzi yanaweza kuhusishwa na maandalizi duni ya wanafunzi. Ni walimu walio na jukumu la kuwaandaa wanafunzi kwa kuwafunza kila dhana katika usahihi wake kwa kuzingatia misingi ya kisarufi. Wanafunzi huwaamini walimu wao hivi kwamba chochote wanachoambiwa na

walimu wao hupewa uzito mkubwa. Kwa hakika, wanafunzi huwa hawashuku mafunzo wanayopewa na walimu wao. Wajibu wa walimu ni kuhakikisha kuwa wamefanya maandalizi ya kutosha kupitia kwa utafiti kabla ya kwenda darasani. Wanafunzi wanapopokea dhana ambazo sio sahihi wanaofaa kulaumiwa ni walimu wao.

Aidha, tuligundua kwamba kulikuwa na makosa mengine yaliyoigwa na wanafunzi kutoka VVK kuonyesha kuwa vitabu pia ni asili ya makosa yanayofanywa na wanafunzi. Kwa jumla 50% ya makosa katika MYW yalitokana na athari kutoka VVK. Miongoni mwa VVK, KF kiliwakilisha idadi kubwa zaidi ya makosa katika MYW kwa 48.38%, UWK kikafuatia kwa 30.65% kisha KK kuwa cha tatu kwa asilimia 20.97%. (Taz. Jedwali 7.2)

**Jedwali 7.2: Makosa katika MYW yaliyohusiana na VVK**

| | UWK | KK | KF | JUMLA |
|---|---|---|---|---|
| Idadi | 19/36 | 13/30 | 30/53 | 62/119 |
| % | 30.65 | 20.97 | 48.38 | 100 |

*Asili: Uhakiki wa mtafiti*

Kulikuwa na makosa yaliyosababishwa na mazoea ya wanafunzi kutokana na yale wanayosikia katika mazungumzo ya kawaida ya watu katika jamii.

Makosa tuliyopata katika VVK yalikuwa na asili yake katika wahusika wote kwenye mchakato mzima wa kuandaa vitabu kuanzia kwa waandishi, wahariri hadi wapiga chapa. Makosa yaliyo katika VVK yanapogunduliwa na habari kufikishwa kwa wahusika katika uandalizi wake, yanaweza kukabiliwa kwa kuyasahihisha katika matoleo yanayofuatia. Ili kukabili makosa yaliyo katika nakala ambazo zimechapishwa tayari, kampuni za uchapishaji zinastahili kutoa makala yanayoonyesha marekebisho kwa makosa hayo kisha yasambazwe kwa watumiaji walio na nakala zilizochapishwa tayari. Makala ya marekebisho yanatakiwa

kusambazwa bila malipo kwa watumiaji wa nakala zilizotolewa mwanzo. Kutokea kwa makosa katika vitabu vilivyoidhinishwa ni kumbusho kwamba kuwe na uwajibikaji wa waliojukumiwa wajibu wa ukaguzi wa vitabu. Wajibu wao ni kutambua makosa hayo na kupendekeza kwa kampuni husika ziyasahihishe kabla ya vitabu hivyo kuidhinishwa kutumiwa shuleni. Aidha, ni wajibu wa Wizara ya Elimu kushurutisha kampuni za uchapishaji kuchapisha na kusambaza makala yaliyo na marekebisho ya makosa yanayogunduliwa katika VVK ili zitumiwe sambamba na nakala za awali zilizosheheni makosa. Tulihakiki jumla ya idadi ya makosa katika kila kitabu dhidi ya idadi ya kurasa zenye matini ya kimafunzo na kupata takwimu zifuatazo:

**Jedwali 7.3: Idadi ya makosa katika kila kitabu dhidi ya idadi ya kurasa**

| Anuani ya kitabu | Kurasa | Jumla ya makosa | Asilimia ya makosa (%) |
|---|---|---|---|
| UWK | 178 | 36 | 20 |
| KK | 266 | 30 | 11 |
| KF | 234 | 53 | 23 |

*Asili : Uhakiki wa mtafiti*

Kulingana na takwimu katika Jedwali 7.1, KF kilikuwa na makosa mengi sana licha ya kuwa kinachukua nafasi ya pili kulingana na idadi ya kurasa. Aidha, licha ya kuwa na kurasa nyingi kuliko vitabu vingine, KK kilikuwa na idadi ya chini sana ya makosa.

### 7.3 Mchango wa Utafiti

Kwa maoni yetu, utafiti wetu umetoa mchango kwa kudhihirisha kwamba makosa yanayotokea katika MYW yana vyanzo mbalimbali. Baadhi ya visababishi vya makosa haya ni wanafunzi wenyewe ilhali vingine vina asili nje ya wanafunzi. Aidha, utafiti wetu umeonyesha kuwa licha ya kwamba VVK vinadhamiriwa kuwa vya mafunzo kwa wanafunzi kwa kuwaelekeza, vimesheheni makosa mbalimbali.

Kutokana na kuwepo kwa makosa katika maandishi ya kiada, utafiti wetu umechangia katika kutambua kwamba kuna dosari katika ukaguzi wa vitabu katika taasisi ya kukuza mitaala nchini. Kadhalika, utafiti wetu umeonyesha kwamba makosa yanapotokea kwenye VVK huwaathiri wanafunzi ambao huyaiga katika maandishi yao. Tasnifu hii imewezesha kuweka bayana kwamba kudorora kwa utendaji wa wanafunzi katika Kiswahili kwenye mitihani ya kitaifa ni jambo linaloweza kukabiliwa kwa kukabili vyanzo mbalimbali vya makosa yanayodhihirika katika MYW. Kwa kuelezea njia mbalimbali zinazofaa kutumiwa ili kuwaimarisha wanafunzi, tumeonyesha kwamba tatizo la kudorora kwa matokeo ya wanafunzi linao utatuzi.

### 7.4 Mapendekezo ya Utafiti

Kwa kutambua kwamba hatujashughulikia masuala yote kuhusu mada ya uchanganuzi wa makosa wala hatuwezi, tunapendekeza kwamba tafiti nyingine zifanywe kuhusu suala hili kwa kuzingatia mada mbalimbali.

Uhakiki wa makosa ya upotofu wa dhana katika VVK unaweza kufanywa. Utafiti huu ulishughulikia makosa ya kitahajia na kisarufi wala haukuangalia maelezo yasiyo sahihi kuhusu dhana mbalimbali katika Lugha na Fasihi kama zinavyotokea katika VVK. Tunatambua ya kwamba dhana zinapowasilishwa kwa njia isiyo sahihi katika VVK, wanafunzi na walimu wanaovitumia hupokea mawazo ya kupotosha. Hatimaye huo upotofu hudhihirika katika majibu ya wanafunzi na mawazo hayo hayawezi kukubalika katika mitihani kuwa majibu sahihi. Hii itachangia utendaji duni wa wanafunzi.

Uhakiki wa makosa ya kitahajia na kisarufi kwa kurejelea VVK vya kidato cha tatu na nne unaweza kufanyiwa uchunguzi. Utafiti huu ulishughulikia makosa ya kitahajia na

kisarufi katika vitabu vya kidato cha kwanza na pili. Tunatambua kwamba kila darasa lina zaidi ya kitabu kimoja cha kiada chenye idhini ya Wizara ya Elimu ili kutumiwa katika mafunzo shuleni na kwa hivyo pana haja ya kuhakiki makosa katika vitabu mbalimbali kama vile vitabu teule vya fasihi na hata vya wanafunzi wa shule za msingi.

Pana haja ya kufanya uchanganuzi linganuzi wa makosa katika vitabu vya kiada ili kutathmini ni vitabu gani miongoni mwa vitabu vingi vilivyopo vinavyofaa zaidi kwa mafunzo shuleni kwa sababu ya kuwa na makosa machache zaidi au kutokuwa nayo. Huu ni utafiti utakaowezesha walimu na wanafunzi kutambua vitabu vilivyo bora ili vitumiwe katika mafunzo.

Makosa yanayohusu uakifishaji na matumizi ya herufi kubwa yanastahili kufanyiwa utafiti kwa sababu uakifishaji hutekeleza jukumu muhimu la kumwelekeza msomaji ili kuwezesha mawasiliano kamilifu na sahihi ya kimaandishi. Hatukuzingatia makosa ya uakifishaji katika utafiti huu licha ya kuona makosa ya aina hii yakijitokeza katika maandishi ya wanafunzi.

Mbali na kushughulikia makosa ya kiuandishi kama watafiti wengi walivyofanya mpaka sasa, tafiti nyingine kuhusu makosa ya kiusomaji zinaweza kufanywa. Kuwapa wanafunzi vifungu vya kusoma huku wakirekodiwa, kisha kutambua makosa ya kimatamshi miongoni mwao, kutatoa fursa ya kuhakiki makosa yanayohusu dhana kama shada na kiimbo kwa vile kusoma ni stadi nyingine ya kufunza lugha. Umilisi wa wanafunzi katika lugha haufai kusisitiza stadi ya kuandika tu huku kusoma kukipuuzwa.

Kwa kutambua jukumu muhimu la mwalimu katika kufunza wanafunzi, pana haja ya kufanya utafiti kwa lengo la kutathmini umilisi wa Kiswahili miongoni mwa walimu wa Kiswahili. Utafiti huu unaweza kufanywa katika stadi zote za lugha yaani Kusikiliza, Kuzungumza, Kusoma na Kuandika. Matokeo ya utafiti wa aina hii yatasaidia kutambua mapengo yaliyopo miongoni mwa walimu wa Kiswahili ili kubuni mikakati ya kuyaziba.

**MAREJELEO**

Al - Jabri (2006). *Spelling Errors of Omani EFL Students*. ResearchGate.

A – Zuoud & Kabilan (2013). *Investigating Jordanian EFL Students*. ResearhGate.

Alhaisoni, M. E (2015). *Analysis of Spelling Errors of Beginner Learners of English in the English Foreign Language Context in Saudi Arabia*. University of Hail, Saudi Arabia.

Ashton, E.O. (1944). *Swahili Grammar (including intonation*). London: Longman.

Besha, R.M. (1994). *Utangulizi wa Isimu na Lugha.* Dar es Salaam University Press.

Brown, H. D. (1993). *Principles of Language Learning and Teaching,* Prentice Hall College Div. Amazon.

Burt, M. & Dulay, H. (1974). 'You Can't Learn Without Goofing' katika Richards, J. (Ed.) *Error Analysis: Perspectives on Second Language Acquisition*. Essex: Longman.

Burt, M. Dulay, H. & Krashen, S. (1982). *Language Two*. Oxford: OUP.

Chepkwony J. (1993). *Makosa Yanayofanywa na Baadhi ya Wanandi Katika Matumizi ya Kiswahili.* Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).

Chomsky, N. (1965). *Aspects of the Theory of Syntax*. Cambridge: The MIT Press.

Connor & Ulla, M. (1996). *Contrastive Rhetoric Cross-Cultural Aspects of Second Language Writing.* Cambridge, UK: CUP.

Corder, P. (1967). *Theories of Error Analysis*. Longman, London & New York

Corder, P. (1973). *Error Analysis and Interlanguage*. OUP.

Cystal, D. (1987). *Child Language, Learning and Linguistics: An Overview of the Teaching and Therapautic Profession.* 2nd Edition. Edward Arnold.

Dulay, H., & Burt, M. (1972; 1974). *Creative Contrastive Theory*. Longman, London & New York.

Dixon, R. M.W. (2010). Basic Linguistic Theory Volume 1. Studies in Language 34 (3). Oxford University Press, Oxford.

Elis, R. (1983). *Understanding Second Language Acquisition*. Oxford: OUP.

Ellis, R. (1994). *The Study of Second Language Acquisition*. Oxford: OUP

Elis, R. (1997). *Second Language Acquisition*, Oxford: OUP.

Figueredo, L. & Varhagen, C. K. (2004). Detecting a Problem is Half the Battle: The Relation Between Error Type and Spelling Performance. Scientific Studies of Reading, 8 (4), 337 – 356. Washington, America.

Fries & Pike (1945). *Teaching and Learning English as a Foreign Language.* University of Michigan Press, Ann Arbor.

Gloria, R. P. (1974). Language Use and Language Change in Brunei, Darussalam.

https://www.academia.academia.edu>LAHAJA NI NINI Dominic Mwingisi-Academia.edu

https://www.academia.edu> LAHAJA ZA KISWAHILI Wilson S. Pastory - Academia 8/7/2016

https://www.en.m.wikipedia.org.wiki/swahililanguage.

Imo, M. M. (2008). *Uchanganuzi wa Mofolojia ya Mnyambuliko wa Vitenzi vya Kiteso, Tasnifu ya Uzamili*. Chuo Kikuu cha Moi, Eldoret Kenya. (Haijachapishwa)

Iribemwangi, (2019). *Kiswahili kama Lugha Changizi: Uchambuzi wa Kifonolojia wa Maneno Yaliyokopeshwa Lugha ya Kikikuyu* uk.125-146 - Makala katika: Mwanga wa Lugha: Jarida la Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika Juzuu 3 Na. 1. Chuo Kikuu cha Moi, Eldoret Kenya.

Kadurenge, B. M. (2000). *Mabadiliko ya Kifonolojia Katika Msamiati Unaosharabiwa Kutoka Kiswahili Hadi Kimaragoli, Tasnifu ya Uzamili.* Chuo Kikuu cha Moi, Eldoret, Kenya (Haijachapishwa)

Kattam, R. J. (2014). *M.A Thesis: Nandi Consonants*, Chuo Kikuu cha Moi, Eldoret Kenya. (Unpublished)

Kenya Literature Bureau (2018). *Kiswahili Kitukuzwe, Kitabu Cha Wanafunzi Kidato Cha 2.* Toleo la sita.

Khansir, A. A. (2012). Theory and Practice in Language Studies, Vol.2 No. 5, pp1027 – 1032. Academy Publisher, Finland.

Kiango, J.G. (2008). Sarufi na Vinyambuo Vitenzi vya Kiswahili: Mitazamo mbalimbali Kuhusu Kanuni za Unyambuaji. Katika N. O. Ogechi; N. L. Shitemi na K. I. Simala. Chuo Kikuu cha Moi, Eldoret Kenya.

Kihore, Y. M., Massamba, D.P.B. & Msanjila, Y.P. (2003). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu.* TUKI: Chuo Kikuu cha Dar- es-salam.

Kiramba, L.K. (2008). *Muundo wa Kisintaksia wa Kikundi Kitenzi cha Kimeru*. Tasnifu ya Uzamili: Chuo Kikuu cha Moi, Eldoret Kenya. (Haijachapishwa)

Kisakwah, B. A., (2014). *Uchanganuzi wa Makosa na Muundo Sentensi: Sentensi Sahili za Kiswahili Sanifu na Kisuba.* Tasnifu ya Uzamili: Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Kitsao, J. (2015). *Uchanganuzi wa Makosa ya Kisarufi Katika Insha za Wanafunzi wa Shule za Msingi*. Tasnifu ya Uzamili: Chuo Kikuu cha Pwani. (Haijachapishwa)

Krueger, R.A (1988). *Focus Groups: Practical Guide for Applied Research.* Sage: UK.

Lado, R. (1957). *Linguistics Across Cultures: Applied Linguistics for Language Teachers*, University of Michigan Press: Ann Arbor.

Lado, R. (1957). *Teaching and Learning English as a Foreign Language.* University of Michigan, Ann Arbor.

Lukamika, M. (2015). *Matumizi ya Ngeli Miongoni mwa Wanafunzi wa Kiswahili wa Chuo Kikuu cha Maseno, nchini Kenya*: Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Maseno, Maseno Kenya. (Haijachapishwa).

Longhorn (2011). Kamusi ya Karne ya 21. Toleo Jipya.

Marshall, Catherine & Gretchen, B. Rossman (1999). Designing Qualitative Research 3rd Ed Sage Publication. En.wikipedia.org/wiki/second_language_makala ya Erdogan Vacide (Contribution of error analysis to foreign language teaching - Mersin University: *Journal of the Faculty of Education* Vol 1 issue 2, Dec.2005 pp 261-270)

Massamba, D.P.B., Kihore, Y.M, & Msanjila, Y.P. (2004). *Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili Sanifu.* TUKI, Dar-es-salaam.

Mbaabu, I. (1995). *Usahihishaji wa Makosa katika Kiswahili*. Longhorn: Nairobi.

Mbori, B. J. (1994). *A study of the Noun Phrase Construction Errors Among Ekegusii Speaking Standard Seven Pupils in Kisii District*, M. Phil Thesis, Moi University (Unpublished)

Mdee, J.S., Njogu, K., & Shafi, A. (2011). *Kamusi ya Karne ya 21.* Nairobi: Longhorn Publishers

Mgullu, R.S. (1988). *Uhakiki wa Makala ya Dhana za Mofu, Alomofu na Mofimu* Katika Mulika Na. 20 Dar-es- Salaam.

Mgullu, R.S. (1999). *Mtalaa wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili.* Nairobi: Longhorn Publishers.

Moran Publishers (2004). *Uhondo wa Kiswahili Kitabu Cha Wanafunzi 1.*

Morgan, D.L. (1988). *Focus Group as Qulitative Research*. Sage: United Kingdom.

Msanjila, Y. P., (2005). Problems of Writing in Kiswahili: A Case Study of Kigurunyembe and Morogoro Secondary Schools in Tanzania, *Makala Katika Nordic Journal of African Studies* 14(1):15-25 (2005).

Mugenda, O.M. & Mugenda, A. G. (1990) *Research Methods: Quantitative and Qualitative Approaches.* Nairobi: Acts Press, www.easyelimu.

Mulalu, J.W. (2014). *Sintaksia ya Vijalizi Katika Kikundi Kitenzi cha Kibukusu,* Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Moi, Eldoret. (Haijachapishwa).

Njeng'ere, D. (1996). *A Study of Verb Group Errors in the Written Work of Form Four Students in Kiambu District,* M. Phil Thesis. Moi University, Eldoret. (Unpublished).

Obuchi, M.S. & Mukhwana. A. (2010). *Muundo wa Kiswahili: Ngazi na Vipengele.* Nairobi: A-Frame Publishers.

Ontieri, O. J. (2010). *Uchanganuzi wa Makosa Katika Insha za Wanafunzi wa Shule za Upili: Mfano wa Wilaya ya Nakuru, Kenya,* Tasnifu ya Uzamifu. Chuo Kikuu cha Egerton, Njoro. (Haijachapishwa)

Opijah, A.L. (2014). *Uchanganuzi wa Makosa ya Kiisimu Katika Matumizi ya Kiswahili Miongoni mwa Wanyore,* Tasnifu ya Uzamifu, Chuo Kikuu Cha Moi, Eldoret. (Haijachapishwa)

Oxford University Press. (2013). *Kiswahili Fasaha Kidato Cha 2*. Toleo jipya.

Rapando, M. (2005). *Uchanganuzi wa Makosa ya Kimofo-Sintaksia Katika Kazi za Wanafunzi wa Shule za Upili Jijini Nairobi*, Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Richards, J.C. (Ed.) (1974). *Error Analysis: Perspectives and Second Language Acquisition.* London & New York: Longman.

Richards, J.C. & Renandya, W.A. (Ed.) (2002). *Methodology in Language Teaching*. Oxford Academic, Oxford.

Safa, N. S., & Mohamed, S. M. (2015). Investigating Study of English Spelling Errors: A Sample Study of Iraqi Students in Malaysia. *International Journal of Education & Research* Vol.3 No. 6 June 2015

Selinker, L. (1972). Interlanguage, *International Review of Applied Linguistics*, 10(3), 209-231. Longman, London & New York

Simotwo, S. K. (1992). *An Investigation of Lexico-Semantic Errors of the Learners of English as a Second Language: A Case Study of Standard Seven Nandi-Speaking Pupils in Primary Schools.* M. Phil Thesis, Moi University, Eldoret. (Unpublished).

Smith, B., & Swan, M. (2001). *Learner English – A Teacher's Guide to Interference and Other Problems,* Cambridge University Press.

Stern, H.H. (1983). *Fundamental Concepts of Language Teaching*. Oxford: OUP.

Stewart, D.W. & Shamdasani, P.N. (1990). *Focus Groups: Theory and Practices*. Sage: United Kingdom

Taylor, R. J. (1975). *Linguistic Categorization: Prototypes in Linguistic Theory*, Cambridge University Press.

Toweett, T. (1979). *A Study of Kalenjin Linguistics: Consonant System* (pp 37 - 59), Kenya Literature Bureau: Nairobi.

TUKI, (2019). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu Toleo la Nne*. Dar es Salaam: OUP

Wamalwa, M. N. (1997). *Kusharabiwa Msamiati wa Kiswahili Katika Kibukusu*, Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Moi, Eldoret. (Haijachapishwa).

Wenslaus, M. (2015). *Athari za Lugha ya Kijita Katika Kujifunza Lugha ya Kiswahili kwa Wanafunzi wa Shule za Msingi Wilaya ya Musoma*, Tasnifu ya Uzamili, Mkoa wa Mara, Open University Of Tanzania.

Wesana - Chomi, E. (2003). *Kozi Tangulizi Katika Sarufi Miundo ya Kiswahili,* Chuo Kikuu cha Sebha, Sebha Libya.

# VIAMBATISHO

## Kiambatisho A: Makosa Katika Maandishi ya Wanafunzi

### Makosa ya Kitahajia

1. a) *Nyumba **hile unatoa** moshi.
   b) Nyumba **ile inatoa** moshi.
2. a) *Hii ni **dhairi shairi** kwamba mtoto yule ana baraka nyingi sana.
